**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Saba – Tarehe 10 Novemba, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Tunaendelea na Mkutano wa Tano, Kikao cha Saba leo tarehe 10 Novemba, 2021.

Katibu, tuendelee.

**NDG. ZAINAB ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JUDITH S. KAPINGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge na Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. ZAINAB ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali. Kama kawaida sasa tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI naanza na Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula.

Na. 69

**Agizo la Kizengi kuwa Tarafa**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo la Rais wa Awamu ya Tatu la kuitambua Kizengi kuwa Tarafa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Protas Venant, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala hufanyika kwa mujibu wa mwongozo wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo huu unaelekeza maombi ya kuanzisha maeneo hayo kujadiliwa na kupitishwa kwenye vikao vya kisheria ngazi za Vijiji, Kata *(WDC)*, Wilaya *(DCC)* na Mkoa *(RCC)* kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijapokea maombi ya Kizengi kuwa Tarafa. Hivyo, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Uyui kufuata mwongozo uliotolewa na kuwasilisha maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya tathmini na kufanya maamuzi kwa kadri ya taratibu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nataka niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na miongozo yote ambayo ameitoa hapa swali langu lilikuwa ni ahadi ya Viongozi Wakuu, hayati Dkt. Benjamini Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu ambaye alikuja katika jimbo la Igalula, Kata ya Igalula mwaka 2002 na akatangaza Tarafa ya Kizenji ambapo ilikuwa na Kata Kizengi, Tula na Loya. Tulisimama kufuata miongozo hii kwa sababu Rais alikuwa kashatamka. Sasa, je kama Serikali wana utaratibu gani wa kufuatilia kauli za Rais na kuzifanyia kazi ili tusiweze kuleta mikanganyiko ya kuwa tunaomba mara mbili mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Jimbo la Igalula pamoja na mambo mengine ni kubwa sana na jiografia yake ni kubwa sana. Je, ni nini mkakati wa Serikali kutoa utaratibu wa kuanzisha na kutoa maagizo ya kuanzisha maeneo ya utawala mengine, maombi mapya ili tuweze kuleta hasa maombi ya halmashauri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Protas Venant, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba halmashauri ya Igalula kwa maana ya Jimbo la Igalula

linahitaji kupata Tarafa ya Kizenga, lakini pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali inatekeleza ahadi za viongozi wa kitaifa kwa utaratibu na kwa wakati, lakini kuna miongozo ambayo ni muhimu iweze kufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo Serikali inaitambua na tutaifanyia kazi, lakini watendaji wameelekezwa kufuata mwongozo kwa maana kuanzishwa vikao ngazi ya vijiji, kata, wilaya na mkoa ili sasa wawasilishe maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kadri ya mwongozo na maamuzi yaweze kufanyika. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa kwamba wakiwasilisha mambo hayo mamlaka husika itafanya tathmini na kufanya maamuzi kama tunaweza kuanzisha tarafa hiyo au viginevyo na taarifa rasmi zitapelekwa katika wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; utaratibu huu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la msingi, unaongozwa kwa miongozo ambayo ipo rasmi. Kwa hiyo kama kuna uhitaji wowote wa kuanzisha halmashauri mpya ni lazima tufuate miongozo ile. Kwa hivyo nimpe rai Mheshimiwa Mbunge na viongozi wa halmashauri husika wakafanye utaratibu wa vikao hivyo na kuleta maombi yao *level* ya Wizara. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Fasto. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), sasa namkaribisha Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo.

Na. 70

## Kusaidia Vikundi vya *BMU* Kupanda Mikoko na Kusafisha Fukwe

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvisaidia vikundi vya BMU ili kuendeleza kasi ya upandaji mikoko na kusafisha fukwe kuanzia Pwani ya Bagamoyo, Pangani hadi Tanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari ina mipango ya kuvijengea uwezo wa uelewa ili kujisimamia vikundi vyote vya *BMUs* katika kuendeleza kasi ya upandaji mikoko na kusafisha fukwe za bahari yetu. Jumla ya vikundi 18 vya Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti vimepatiwa mafunzo ya kupanda, kuhifadhi na kusimamia mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vikundi vya *BMUs* vya Mlingotini Bagamoyo vimewezeshwa kupanda miche 7,000 ya mikoko. Vilevile, vikundi vya *BMUs* vya vijiji vya Moa, Ndumbani na Mahandakini Wilayani Mkinga vimepatiwa mafunzo ya usimamizi wa mazingira ikiwemo upandaji wa mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia mradi wa South West *Indian Ocean Fisheries (SWIOfish)* unaoratibiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Vikundi vya *BMUs* vya Bagamoyo na Pangani wamepata uelewa wa kukusanya maduhuli ambapo kiasi cha fedha kinachokusanywa kitatumika katika kuendeleza shughuli za upandaji wa mikoko na usafi wa mazingira. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Waziri anaweza kutueleza ni mafanikio yapi yamepatikana katika mpango huo toka umeanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Bagamoyo imekumbwa na changamoto kubwa sasa hivi ya kumegwa ardhi na maji ya bahari na hasa katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo na maeneo mengineyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inadhibiti hali hiyo isiweze kuendelea.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Muharami kwa juhudi yake ya ufuatiliaji wa mazingira lakini na mabadiliko ya tabianchi katika Jimbo lake la Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ambayo yamepatikana katika miradi hii, moja; ofisi tano za *BMUs* tumejenga katika Wilaya za Bagamoyo na Pangani. Sehemu ambazo zimejengewa ofisi hizo na kuzipatia samani ni pamoja na Saadani, Chalinze; Zingibari, Mkinga; Kipumbwi, Pangani; Dunda, Bagamoyo; na Sudimtama na tumewanunulia viatu na makato kwa ajili ya kusimamia usafi huu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni kweli kwamba Bagamoyo ni moja ya kati ya sehemu ambazo zina changamoto kubwa za mabadiliko ya tabianchi, lakini tayari ofisi yetu imeshapeleka watalaam kufanya upembuzi yakinifu na kufanya *survey* ambayo ni sahihi na watalaam hawa wameshaleta majibu, siku za karibuni hivi basi mradi utaanza kutekelezwa katika eneo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Madini Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Kijiji cha Sakale Kuruhusiwa Kuchimba Dhahabu – Muheza**

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawaruhusu wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Sakale, Kata ya Mbomele, Wilayani Muheza kuanza uchimbaji wa madini ya dhahabu yaliyothibitishwa kupatikana katika kijiji hicho?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uchimbaji mdogo katika eneo la Sakale zilikuwepo kati ya mwaka 2004 na mwaka 2016. Baada ya ziara za viongozi wa Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Muheza, Wizara ya Madini pamoja na *NEMC* na pia Mheshimiwa Mbunge mwenyewe iligundulika kuwa uchimbaji huo unafanyika katika chanzo cha Mto Zigi ambacho ni chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa Muheza na Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya wataalam wa mazingira iliyofanyika mwaka 2018 Oktoba, ilionyesha kuwa athari za kimazingira ni kubwa endapo uchimbaji utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo na kwa kuhifadhi chanzo cha maji katika bonde la Mto Zigi, uchimbaji mdogo wa dhahabu katika Kijiji cha Sakale, Kata ya Mbomele, Wilayani Muheza hauruhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamis.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, ripoti ya *NEMC* ya Oktoba, 2018 ambayo Mheshimiwa Waziri anaitaja, ilielezea wazi kwamba kinachokatazwa ni uchimbaji mdogo na inashauriwa ufanyike uchimbaji aidha wa kiwango cha kati ama mkubwa, kwa sababu hizo za kimazingira ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja. Sasa je, Serikali haioni kwamba kwa vile wananchi wa Sakale, Kata ya Mbomole, Wilaya ya Muheza, hawana uwezo wa kufanya uchimbaji wa kiwango cha kati ama mkubwa inafaa sasa iwasaidie kupata mwekezaji mwenye vigezo vinavyotajwa na ripoti hiyo ili uchimbaji ule uweze kufanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyikiti, la pili; ni ombi kwa Wizara, kwamba tuna maeneo kadhaa mengine katika Wilaya ya Muheza katika Kata ya Pande Darajani katika Kata ya Magila na katika Kata ya Magoroto hasa Kijiji cha Mwembeni ambayo yanaonyesha dalili za kuwa na madini. Je, Serikali inaweza kututumia watalaam wake ili wakafanye tathmini na kuona kama kuna uwezekano wa kuchimba katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Profesa Shukrani, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge Hamis Mohamed Mwinjuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kutoa majibu ya Wizara, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa mwelewa, kwa sababu tulipofanya ziara hii na kukubaliana kwamba uchimbaji mdogo utaleta athari kubwa za mazingira, mara nyingi watu wasingeweza kuamini kwamba mbona kuna mali, lakini tathmini ya kimazingira ilionyesha kwamba uchimbaji mdogo utaleta athari kubwa ambazo yawezekana zisiwe na faida hata kama uchimbaji unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kuelewa kwa Mheshimiwa Mbunge ndiyo maana hata wananchi wote wakaelewa kwamba huenda kama madini haya lazima yachimbwe basi iwe ni kwa uchimbaji wa kati ambao teknolojia yake inakuwa ni ya kuchukua udongo mahali pale na kuchenjulia sehemu nyingine ili kuendelea kulinda vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Wizara itatoa ushirikiano wote ambao wananchi wanauhitaji kwa sababu pale tulikwishatoa leseni za uchimbaji mdogo. Kwa hiyo tutawaomba tu wafuate utaratibu, wao watapata muwekezaji halafu watakuja Wizarani, watafanya *amalgamation* ya uchimbaji mdogo tutazi-*upgrade* kuwa za uchimbaji wa kati na tutawapa miongozo yote inayostahili ili waweze kufanya uchimbaji ambao bado utazingatia kutoathiri chanzo cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili; *GST* ndiyo taasisi yetu ambayo inakwenda kufanya utafiti wa awali na huwa tunapenda kuhimiza utafiti wa awali kwa sababu hautakuwa ule ambao unaleta na wingi wa mashapo kwa kule chini. Sasa hilo linawezekana, tutawaagiza waje. Mheshimiwa Mbunge hata baada ya hapa anaweza akaja pale ofisini kwetu tukaongea na watu wa *GST* na wakapanga namna ya kwenda nawe ili awaelekeze katika maeneo ambayo anataka waweze kufanya utafiti ili huo wa awali uweze kuonyesha kama uchimbaji unaweza kuendelea katika vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kasaka na Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nchi yetu hii imezungukwa sana na wachimbaji wadogo wadogo hasa kwenye maeneo mengi yenye uchimbaji wa madini. Je, ni lini sasa Serikali itarudisha utaratibu uliokuwepo mwanzo wa kutoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo hawa ili kuweza kuwasaidia waweze

kupata vifaa na baadaye waweze kufanya uchimbaji wao uwe mzuri zaidi, tuweze kuwapata walipa kodi wazuri zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Profesa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Masache, Mbunge wa Chunya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wakati wa nyuma Serikali ilitoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo, lakini nipende kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu ule wa ruzuku ama haukueleweka vizuri watu walipokuwa wanachukua na haukuwa na tija yoyote katika kufanikisha malengo yaliyokuwa yamepangwa. Kwa msingi huo Wizara inaendelea kutathimini kuona kama kuna sababu ya kufanya hivyo tena iwe ni wachimbaji wetu wameelewa ili makusudi ya kutoa ruzuku hizo yaweze kufikiwa. Wakati Wizara inafikiria namna ya kufanya hivyo tena tumeona kwamba njia nyingine ambayo inaweza ikawa ni nyepesi ni ya kuyaona mabenki yetu ya ndani, ambapo Mheshimiwa Mbunge ana taarifa kwamba baadhi ya wachimbaji wadogo wadogo katika Jimbo lake la Chunya wamekwishapokea fedha kutoka kwenye mabenki yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huo ni utaratibu ambao tunadhani kwamba *in the interim* kabla ya kufikiria kwamba tunaweza tukawa na wakati mwingine wa ruzuku, basi twende na njia hii ambayo nayo imeanza kuonyesha dalili za kufanikiwa katika kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naiuliza Serikali, Mgodi wa Kiwira kwa muda mrefu sana umesimama, je, ni lini Serikali itaamua kuleta wawekezaji au Serikali kuweka nguvu ili kusudi

Mgodi huu wa Kiwira uweze kutoa ajira, lakini pia kuipatia pato Serikali yetu ya Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Profesa Shukrani.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Kiwira ni kweli tunatamani kwamba ndani ya Serikali uweze kuanza na wakati wa nyuma tumekuwa tunatamani kwamba taasisi zetu mbili *TANESCO* pamoja na *STAMICO* waweze kukaa pamoja na kukubaliana, kwa sababu mgodi ule pamoja na kwamba unatoa tu makaa ya mawe, lakini pia kinatarajia kuwa chanjo kingine cha kutoa nishati na kwa jinsi hiyo inahusisha taasisi zetu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema tu kwamba mwezi Julai, *TANESCO* pamoja na *STAMICO* waliwekeana makubaliano ya kufanya kazi kwa pamoja na hivi ninavyoongea Shirika letu la *STAMICO* lipo katika harakati za ku-*mobilize* mwekezaji ili mgodi ule uweze kuanza. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Profesa Shukrani Manya.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo.

Na. 72

**Kutafuta Teknolojia Mbadala wa Zebaki**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta teknolojia mbadala ili kunusuru afya za wananchi wanaotumia zebaki kwa matumizi mbalimbali?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na taasisi zake, ipo kwenye mpango wa kutafuta teknolojia mbadala na tayari vikao vya pamoja na taasisi zinazohusika na uchimbaji wa dhahabu vinafanyika ili kupata teknolojia isiyohitaji zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu na hivyo kuondoa athari za kiafya kwa jamii na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa elimu juu ya matumizi sahihi, kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa katika siku za usoni matumizi ya zebaki ni dhamira ya Serikali katika kulinda afya ya jamii na mazingira. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amezingatia eneo moja tu la uchimbaji wa dhahabu: Je, Serikali ina mpango gani wa kubadili matumizi ya zebaki inayotumika katika vifaa vya afya ikiwemo katika ujazaji wa jino?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Je, zebaki inayotumika katika huduma za afya kama vile kipima joto kwa maana ya *thermometer* ama wakati wa kujaza jino kwa

maana ya *amalgam,* ina athari gani zinapotumiwa na binadamu; na je, athari hizo zinapatikana baada ya muda gani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili mazuri ya Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, matumizi ya vitu vyenye *mercury* kwenye kutibu meno; moja, kwa *mercury* ipo dozi maalum ambayo kuna mahali inapofikia ndiyo inaweza kuleta athari. Hata hivyo ni kweli kwamba kuna baadhi ya watu wakizibwa meno kwa kutumia *amalgam* hiyo yenye *mercury,* wengine wanapata *allergy.*

Kwa hiyo, wakati mwingine watu wanaweza wakafikiri ni madhara ya *mercury,* lakini ni *allergy* kwa sababu kuna watu wenye *allergy* na baadhi ya mambo. Mpaka sasa, kwa kutibu meno, inatumika na haijaonesha madhara ambayo unadhani yanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *options* mbalimbali za kutumia na utafiti unaendelea kuona namna ya kupata kitu chenye *strength* ile ile ambayo *amalgam* ilikuwa inafanya ili waweze kuitoa, lakini kwa kweli mpaka sasa kitiba haina shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, amezungumzia *thermometer* na vifaa vingine vya tiba ambavyo vina *mercury,* tunafanyaje? Kikubwa ambacho mpaka sasa hata kwenye madini kinafanyika, kwenye vifaa vyote vya tiba na hata dawa, suala kubwa hapa, ni kwa namna gani unafanya *disposing* na *control mechanism* zinavyohaibika na zile *thermometer* unazi-*dispose* kwa namna gani? Ndiyo maana kuna utaratibu maalum wa namna ya ku-*dispose* vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu wa kuhakikisha *thermometer* na vifaa vingine vyote vinavyotumia *mercury* vinakuwa *under control* na vikiharibika ile *disposing mechanism* inafuatwa ili kutunza mazingira na kutunza afya ya binadamu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matumizi ya zebaki, hasa Kanda ya Ziwa, sehemu ambazo wanachimba madini imekuwa ikisababisha ongezeko la wagonjwa wa Kansa ya Shingo ya Uzazi: Je, Serikali imeshafanya utafiti kuthibitisha kwamba zebaki ndiyo chanzo cha ongezeko la magonjwa ya kansa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba hata ukienda *Ocean Road* imeonekana kwamba wagonjwa wengi wenye matatizo ya kansa wanatokea Kanda ya Ziwa. Hayati Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli aliwahi kuagiza ufanyike utafiti ambao bado majibu yake hayajaja ili kuthibitisha nini hasa chanzo cha tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika kwa sasa ni kwamba kwanza kuna sababu nyingi ambazo zinasababisha kansa ya kizazi. Kwa hiyo, hatuwezi kusema *specifically* ni hilo. Kikubwa, tunashirikina na Wizara ya Madini kupitia taasisi yake kuhakikisha sasa wanapochenjua madini, wale wachimbaji wadogo na wakubwa kunakuwepo na *control* ya kutosha kuhakikisha kwamba haiendi kwenye mazingira na vile vile

haiendi kufika maeneo ambayo binadamu wanatumia maji na vitu vingine. Hilo ndiyo tunaendelea nalo kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, sasa ni swali la Mheshimiwa Halima James Mdee.

Na. 73

**Homa ya Ugonjwa wa Mapafu *(Covid-19)***

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza: -

(a) Je, tangu janga la *Corona* lianze ni Watanzania wangapi wamepata maambukizi; wangapi wamekufa; na wangapi wamepona?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa na Serikali na zimefanya nini na wapi katika kukabiliana na janga hili?

(c) Je, nini kinapelekea gharama za kupima *Covid-19* kuwa kubwa na ni dawa gani zilizofanyiwa uchunguzi na kuthibitishwa kuwa zina uwezo wa kuzuia au kutibu *Covid-19?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimeathirika na mlipuko wa Ugonjwa wa *Covid-19.* Hadi kufikia tarehe 25 Oktoba 2021, idadi ya

Watanzania 26,164 ndio waliothibitika kuwa na maambukizi. Kati ya hao, 725 walifariki na 25,330 walipona.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani kiasi cha shilingi bilioni 158 zimetumika kununua vifaa mbambali ikiwemo mitambo 19 ya kuzalisha hewa ya *oxygen* yenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 hadi 300 ambapo mitambo saba tayari imeshasimikwa na 12 ipo katika hatua ya usimikaji. Fedha nyingine zilinunua *PPE,* dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi pamoja na magari 105 ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Sekta ya Afya imepokea kiasi cha shilingi bilioni 466.78 ambazo zitatumika katika kupambana na Uviko-19 ikiwemo kujenga na kusimika vifaa katika majengo ya matibabu ya dharura *(EMD)* 115, ujenzi wa wodi za uangalizi maalum *(ICU)* 67, ununuzi wa magari 253 ya kubebea wagonjwa, magari nane ya damu salama, usimikaji wa mitambo 10 ya kuzalisha hewa ya *oxygen*, vitanda 2,700 kwenye vituo 225 vya kutolea huduma za afya, kununua na kusimika mashine 95 za *X-Ray, CT-Scan* 29, mashine 4 za *MRI* pamoja na kufanya tafiti sita kuhusu tabia za virusi vya korona.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama halisi ya kumpima mgonjwa mmoja ni Dola 135 na Serikali sasa inatoza Dola 50. Hivyo Serikali inachangia Dola 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti mbalimbali zimefanyika duniani kuhusu dawa, ila hadi sasa dawa zilizopo zinatumika kutibu tu madhara yatokanayo na virusi. Hata hivyo kilichothibitika kwa sasa kusaidia kuondoa vifo ni chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali yangu ya nyongeza, siafiki takwimu za Serikali kwa sababu *Covid* ilisambaa nchi nzima na kwa watu 725

ukigawanya tu kwa mikoa 31 maana yake kila mkoa wamekufa watu 23 ambayo haina mantiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la pili, Tanzania tulisitisha kutoa taarifa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, uliza swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naeleza kwanza kwa nini takwimu zake ni za uongo. Kwanza idadi aliyotoa *against* mikoa, lakini pili…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwenye maswali? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, naomba utumie muda mfupi katika kuuliza maswali ya nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kama nchi tulisimamisha mwaka mzima, Machi, 2020 mpaka Machi, 2021 kutoa takwimu. Kwa hiyo, hizi taarifa za takwimu siyo za ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maswali yangu ya nyongeza mawili; la kwanza, moja kati ya changamoto kubwa ilikuwa ni upimaji, kwa sabbau ilikuwa lazima upime ndiyo ujue huyu mtu amekufa na *Covid* ama hajafa na *Covid;* sasa Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana juu ya mkopo wa shilingi bilioni 466 toka *IMF,* lakini hivi vitu alivyoviainisha hapa hakuna hata sentensi moja inayozungumzia ujenzi wa maabara ama uwepo wa maabara kwa ajili ya kupima *Covid* ama virusi vingine vinavyoashiria ama vinavyofanania na hivyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka aniambie, kwa sababu tunaishi na *Covid-19* na virusi vinavyofanania na hivyo vitakuja, ni fedha kiasi gani katika mkopo huu wa shilingi bilioni 466 tutapeleka kwenye eneo la maabara *specifically;* na siyo

hizi maabara sijui *X-Ray,* hizo zinatoa viashiria tu, kwamba kuna homa ya mapafu? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusiana na dawa, nili-*intend* hapa kuuliza, tiba za asili za Tanzania kwa kiwango kikubwa sana zimechangia kutibu madhara yanayotokana na *Covid.* Imesaidia sana; na hizi ni fursa kwa watu wa tiba za asili kwa nchi, kwa ukanda na dunia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Serikali iniambie, mpaka sasa, kwa sababu kila siku mnajibu mnafanya tafiti, mmeshagundua ni tiba gani za asili ambazo ni sahihi kwa Watanzania watakaopata maradhi ama Virusi vya *Covid* ili wakiugua tujue *protocol* ya matibabu ni hii; na siyo sasa hivi kila mtu anakunywa kivyake mpaka tunakunywa sumu? Ni lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie tu rafiki yangu kwamba hii ni sayansi. Kama ni sayansi, inahitaji akili kubwa kuweza kuyaona hayo na siyo hisia za kwenye ma-*corridor.* *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu kwamba Bugando, Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia amepeleka vifaa vya maabara vya kupima *Corona* vyenye thamani ya shilingi bilioni nne na mlinisikia nikisema. Kibong'oto ambayo ndiyo taasisi yetu ya magonjwa ambukizi, imepelekewa vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni sita na maabara inajengwa kwa thamani ya shilingi bilioni 14. Maabara yetu ya Taifa nayo inayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujue *virus* siyo mdudu mpya. Ni mdudu mpya kwenye *genetic makeup* lakini sayansi ni ile ile. Kwa hiyo, maabara ni zile zile, mashine ndiyo zimetofautiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni kuhusu tiba ya asili. Kwanza hatujaacha tiba ya asili. Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 1.2 imeenda *NIMR* kwa ajili ya kuchakata dawa zetu zilizoonekana kwamba zinatusaidia na kuziweka vizuri. Vilevile kwenye fedha hizi ambazo nilikuwa nazitaja, shilingi bilioni 466, imetengwa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya utafiti ule mkubwa na mgumu kwa ajili ya kuja na chanjo yetu ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa ninachoweza kumwambia Mheshimiwa, haya ya kisayansi huwa ni magumu, nawaachia wanasayansi. Unahitaji *super computing system* kubwa kuziona; hii siyo ngwini yaani, unajua. Kwa hiyo tulia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, nimekuona.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami pamoja na majibu mazuri kabisa ya Daktari msomi, mwanasayansi Mheshimiwa Mollel, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tunaona Serikali ikishiriki katika kampeni mbalimbali tunapokuwa na magonjwa haya ya mlipuko na magonjwa mengine. Kwa mfano tuliwahi kuwa na kampeni ya kutokomeza Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu, ni upi mpango wa Serikali kutumia wasanii wetu katika kuhamasisha, lakini pia kutoa elimu zaidi kwa wananchi hasa makundi ya vijana katika kupambana na Ugonjwa huu wa Uviko-19? Kwa sababu tunaona katika awamu hii kama wasanii hawajatumika sana katika eneo hili? Ni upi mpango wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Mbunge ni muhimu sana; na kweli kwa kutumia wasanii wanaweza wakatufikishia vizuri sana ujumbe, lakini kikubwa ambacho kinaendelea sasa hivi ni kuhakikisha kwamba badala ya kutumia wasanii kutoka juu, tunapeleka kabisa huduma iende ikafanyike na jamii yenyewe kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana kwamba, ukiangalia fedha tulizonazo, ukitumia sana wasanii hawa wakubwa, ambao bado tunaendelea kuwatumia na tutawatumia jinsi watakapohitajika, lakini kwa kupeleka kule chini huduma inafika kwa urahisi zaidi kwa lugha inayoeleweka na watu wa jamii iliyoko eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumesema tutakwenda kule na tukifika kule Umasaini tutawatumia wasanii walioko kule, lakini tutatumia redio na lugha zilizoko kule ili waweze kupata kirahisi na ili ujumbe ufike. Ila hatuna lengo la kuwaacha wasanii, isipokuwa tunatafuta namna ya kutumia hela kidogo kwa kufanya kazi kubwa zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, nimekuona.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu maswali ya nyongeza, alisema wamefanikiwa kupeleka vifaa vya maabara kwenye maeneo mawili. Nchi yetu ukichanganya na Zanzibar ina mikoa 31, kwa Bara ni 26: Je, hamwoni kwamba hiki ni kikazi kiduchu kwa tatizo kubwa ambalo limetukumba la *Covid?* Ni lini mtahakikisha hizo maabara zinakuwepo nchi nzima na siyo hizi mbili ambazo zimetokana na pesa ya mkopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo niliyoyasema ni mifano tu. Nataka nimweleweshe Mheshimiwa Mbunge kwamba toka Uhuru tumekuwa na *CT-Scan* mbili tu kwenye nchi hii, kwenye hospitali za mikoa mbili tu, lakini amekuja leo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, tunakwenda kupata 29 ambazo zina gharama kubwa kuliko mashine za kupima *Corona. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka tu kumhakikishia ni kwamba tuna uwezo huo, mpaka leo tunapoongea hivi *Mount Meru Hospital* wanapima, Mbeya wanapima, kila mahali tutafikiwa. Kwa hiyo, usiogope, kazi inapigwa. Sisi tuendelee kusherehekea, karibuni upande huu kumenoga. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel. Tunaendelea sasa na Wizara ya Kilimo, namwita Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe. Karibu uulize swali lako.

Na. 74

**Mpango wa Kuboresha Zao la Chai Nchini**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha zao la chai nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la chai linaingizia Taifa fedha za kigeni zaidi ya dola milioni 60 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja kwa zaidi ya watu 50,000 viwandani na mashambani. Zao hili linalimwa katika Wilaya 12 na Mikoa sita ambayo ni Mbeya, Njombe, Iringa, Tanga, Kagera na Mara ambapo wakulima wadogo wa chai wapatao 32,000 hujishugulisha na kilimo cha zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na jitihada za kuendeleza zao la chai kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija na ubora kwa kutenga fedha za kwa ajili ya utafiti, upatikanaji wa miche bora ya chai, kuimarisha miundombinu, kutoa mafunzo na masoko. Kwa mwaka 2021/2022, Serikali imetenga fedha za maendeleo jumla ya shilingi 400,000,000 kwa ajili ya kuzalisha miche 1,000,000; kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo na kuendeleza mashamba mama manne yanayosimamiwa na Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai *(TSHTDA)* ya Korogwe na Lushoto.

Mhasimiwa Mwenyekiti, kupitia Mradi wa *AGRICONECT* jumla ya *Euro* milioni tano na laki tano zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza zao la chai katika mnyororo wa thamani katika kipindi cha miaka minne inayoishia 2023/2024 katika Wilaya za Rungwe Busokelo, Mufindi na Njombe. Mradi unaotekelezwa na Kampuni za *IDH, TRITI* na *TSHTDA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi 290,722,500 zimetengwa kwa ajili ya kuzalisha miche 750,000, kutoa mafunzo kwa wakulima hususani kanuni bora za kilimo, kuimarisha Vyama vya Ushirika vipatavyo 34 na kuimarisha huduma za ugani. Miche itakayozalishwa imelenga kutumika kuziba mapengo kwa kuanzisha mashamba mapya. Aidha, ufadhili wa *AGRICONEC* na kwa kushirikiana na sekta binafsi, Wizara inaratibu uanzishwaji wa mnada wa chai katika kuhakikisha kuwa chai ya wakulima inapata bei nzuri na soko la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada huo wa chai nchini unatarajiwa kuanza rasmi mwishoni mwa mwaka huu. Wizara

kwa kushirikiana na wadau inakamilisha mkakati wa chai utakaoishia mwaka 2030. Wenye lengo mahususi ya kuongeza tija, uzalishaji wa ubora wa chai, ufanisi katika kutoa huduma za ugani pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Mkakati huu unalenga kuongeza uzalishaji wa chai kutoka tani 33,000 hadi kufikia tani 9,000 chai kavu, ifikapo mwaka 2030 na kuongeza matumizi ya teknolojia katika mnyororo wa thamani na kuimarisha mfumo wa masoko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza niishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri ambayo inafanywa kwenye sekta hii muhimu sana ya zao la chai nchini. Nasi wananchi wa Jimbo la Lupembe kwa taarifa tu ni kwamba wananchi sasa wameanza kulipwa mazao yale vizuri, Serikali pia imetupatia fedha kwa ajili ya barabara za kwenye mashamba ya chai, naipongeza sana Serikali na kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, Mpango wa Serikali sasa ni kwenda mbele kuboresha hili zao la chai, Lupembe tulikuwa na mgogoro wa Kiwanda kwa muda mrefu kwa miaka 17 ambao sasa umefikia mwisho. Tumekubaliana kiwanda kirudishwe kwa wabia, kwa maana ya wakulima pamoja na Serikali. Lakini mpaka sasa mchakato wa ukaguzi wa kile kiwanda ili kiweze kukabidhiwa kwa wananchi haujafika mwisho.

Je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba ukaguzi huu unafanyika haraka na kiwanda kile kiweze kwenda kwa wananchi ambao ni wakulima wa chai? *(Makofi)*

Jambo la pili; ndani ya Bunge lako Tukufu pamekuwa na ahadi ya muda mrefu ya Serikali, ya kuanzisha mnada wa

zao la chai Dar es Salaam ambapo kwa muda mrefu chai yetu nchini inauzwa Mombasa.

Je, ni lini mnada huu wa chai utaanzishwa nchini Tanzania ili kukuza bei ya chai ya wananchi wa Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Enosy, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana na sisi kama Wizara ya Kilimo tunamshukuru kwa dhati kabisa kama Mbunge wa eneo la Lupembe, namna alivyoshiriki katika kuhakikisha kwamba mgogoro uliodumu miaka 17 unafika hatma tunakushukuru sana kwa *support* uliyoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali baada ya huu mgoogro kuwa muda mrefu na mgogoro huu tumeanza kuhangaika nao kwa zaidi ya miaka 17. Hivi sasa tumefikia tamati na tumesaini makubaliano kupitia *Solicitor General* kati ya pande ambazo zilikuwa zinavutana na hivi sasa ninavyoongea, Kamati kutoka Ofisi ya *TR* inafanya tathmini ya kuangalia baadhi ya misitu iliyokuwa sehemu ya mgogoro huo na sasa hivi ninavyoongea wako Lupembe wakifanya kazi hiyo na wameripoti siku ya jana katika Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ni kufanya tathmini ya *investment* iliyowekwa na mwekezaji ili tuone kwamba, hatutaki siku ya mwisho kudhulumu haki ya mtu. Tunataka hii *situation* iondoke na tuweze kufanya tathmini kwa hiyo, tunamuomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda. Sisi kama Wizara tumeshawasiliana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya *TR*, kuhakikisha kwamba mgogoro huu tunaumaliza mapema. Ili mwakani kiwanda kile kianze kazi chini ya

*management* mpya na yule Mwekezaji tuwe tumemalizana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mnada nataka tu nimwambie kwamba dhamira na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba, mnada huu unatakiwa uanze mwaka huu Disemba.

Mheshimiwa Mwenuekiti, nataka nitoe tu taarifa katika Bunge lako Tukufu leo hii hii tumemaliza kikao cha wadau, kwa sababu wazalishaji wa chai walikuwa wanahofu namna ambavyo tunauweka huu mnada na ile *rule book* ambayo tunaipitisha. Tumejadiliana na kuweza kukubaliana juu ya mambo yote ambayo walikuwa na hofu nayo. Sasa tunaenda hatua ya pili mnada wa chai unahitaji kuwepo kwa kusajiliwa kwa *brokers* ambao watafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na gharama tumekubaliana tutawasajili *ma-broker* kutoka nchi ya Kenya na kutoka nchi ya Sri Lanka ili mnada wetu uweze kuwa na *International Picture* na mwisho tutawasajili bure. Leo ndiyo tumekubaliana hivi vitu, nataka nimuombe Mheshimiwa Mbunge na wadau wa chai watupe muda tutahakikisha mnada unatokea, kuna changamoto chai yetu *volume* ni ndogo, tunaongea na wenzetu wa Burundi ili chai yao nayo ipite katika soko la Dar es Salaam tuko katika hatua nzuri. Tunasaini *MOU* na Serikali ya Rwanda kati ya Wizara ya Kilimo ya Tanzania na Wizara ya Kilimo ya Rwanda Juu ya namna ambavyo nao chai yao iweze kupita katika mnada wetu. Kwa hiyo, tuko katika hatua nzuri tumeshakuwa na *rule book,* tumeshamaliza *structure* zote tumeshaweka *platform* na sasa tunaanza kusajili madalali watakaoshiriki katika mnada huu na mnada huu utatokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga simuoni, halafu Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Wilaya ya Hanang' ni wakulima wakubwa sana wa kilimo cha ngano na wanalima haswa, shayiri na waliingia mkataba na *TBL* kwa kipindi kirefu juu ya kuwapa mbegu lakini baadae kuwauzia. Kwa hiyo, kuwa na soko la uhakika lakini pia upatikanaji wa mbegu wa uhakika. Mpaka sasa *TBL* imekaa kimya kwa wakulima na wakulima wamekuwa na taharuki kubwa kwa sababu, msimu umefika na *TBL* wamekaa kimya.

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kuwaondoa hofu wakulima wa shayiri wa Wilaya ya Hanang'? Tunaomba majibu ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halamga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kauli ya Serikali. *TBL* hana *excuse* yoyote kuondoa mfumo wa *contract farming* wa zao la shayiri. Mwaka jana walitaka *ku-withdraw* tulikaa nao tukasaini nao makubaliano na walinunua jumla ya tani 8,000 kutoka katika maeneo yenu na leo nimeongea na *management* ya *TBL* mimi mwenyewe baada ya kupigiwa simu na Mkuu wa Wilaya watarudi kununua. Kwa sababu, mahitaji yao yote ya *incentive package* waliyotaka kwa ajili ya kujenga kiwanda hapa Dodoma Serikali imewapatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie Bunge lako hili Tukufu kuwaambia *TBL* warudi wakasaini mikataba na wakulima wa Kanda ya Kaskazini kwa ajili ya zao la shayiri kwa sababu, kilio chao Serikali ilisikiliza na tuliwapatia *incentive package* walizotaka na watapata msamaha wa kodi, tofauti na mzalishaji yeyote wa kinywaji wanachozalisha atakayeagiza shayiri kutoka nje. Hatutoruhusu kuagiza shayiri kutoka nje kabla ya shayiri ya ndani ya nchi kununuliwa. Huu ndiyo msimamo wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Ndaisaba halafu baadae tutaenda ukumbi wa Msekwa, Mheshimiwa Boniphace Butondo.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Changamoto ya wakulima wa Lupembe kwenye eneo la chai ni sawa na changamoto inayowakabili wakulima wa parachichi kwenye Wilaya ya Ngara. Mathalani upatikanaji wa miche bora ya parachichi, masoko pamoja na bei.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatambua wakulima wa parachichi Ngara lakini pia na kuboresha zao la parachichi Ngara? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza yeye ni mdau wa mazao ya *horticulture* na amekuwa akishirikiana na Wizara katika maeneo mbalimbali. Pili, parachichi ni moja kati ya mazao ambayo kama Wizara ya Kilimo tunayapa *priority* kubwa kama ni zao ambalo linaweza likabeba sekta nzima ya mbogamboga na matunda. Nataka nimuhakikishie tu kama ana *special case* zinazohusu Ngara aje Wizarani tukae, tuweze kutatua kama ambavyo tumekuwa tukitatua matatizo ya wakulima wa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miche ya parachichi sasa hivi kama Wizara kupitia *TOSCI* na *TARI,* tumeanza mpango wa kutambua wazalishaji wa miche binafsi ambao wanazalisha miche ya parachichi na kuwasajili ili kuweza kulilinda zao hili siku ya mwisho lisiweze kujikuta tunaingia kwenye matatizo kama nchi. Kwa hiyo, nataka nimuombe kama ana jambo *specific* aje tukae tuweze kujadiliana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, ukumbi wa Msekwa aulize swali lake la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kilimo cha zao la pamba msimu wake ni kipindi hiki na wakulima katika Wilaya ya Kishapu na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla wameshaanza kulima. Lakini Wizara ninaishukuru kwa sababu wamesaidia usambazaji wa mbegu japokuwa siyo kwa wakati. Je, ni aina gani ya mbegu inayotumika sasa hivi katika msimu huu, kwa ajili ya kilimo cha pamba, kwa maana msimu uliopita mbegu tuliyokuwa tunalima haikuwa na tija kwa maana ya uzalishaji wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia haikuwa himilivu kwa magonjwa mbalimbali. Kwa hiyo, ninataka nipate majibu Wizara inasema ni aina gani ya mbegu ambayo sasa, ni mbegu rasmi na ndio mbegu inayotumika katika kilimo cha msimu wa mwaka 2021/2022? Pia, ni nini mpango wa kuhakikisha kwamba viuatilifu vinasambazwa kwa wakati? Kwa sababu, kumekuwepo wa ucheleweshwaji wa viuatilifu ili mradi kupambana na aina mbalimbali ya magonjwa katika zao la pamba. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza aina ya mbegu tunayopeleka ni *UK*08 ambayo tumekuwa nayo kwa kipindi cha kama miaka mitatu, miaka minne sasa hivi. Changamoto iliyojitokeza mwaka jana tumeitatua kwa kuhakikisha kwamba, mbegu tunazozisambaza safari hii zimeshakuwa *treated* na wakati zinaenda kupandwa tayari mbegu zile zina dawa. Tatizo lililojitokeza mwaka jana ni tatizo ambalo

halihusiani sana na mbegu ni tatizo ambalo lilitokana na mambo makubwa mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, mbegu zilizoenda zilikuwa hazina dawa ya kupandia ambalo tumelitatua mwaka huu. Jambo la pili ambalo lilijitokeza mwaka jana kule kwenye ukanda wa pamba kuna wale machinga, mbegu ambazo sisi tulizihakikisha zinaenda shambani zikalimwe ziliuzwa na wajanja halafu wakulima *waka-replace* kwa mbegu yoyote anayoipata barabarani. Kwa hiyo, tumeamua kutengeneza utaratibu upya, *tume-control* mfumo wa usambazaji na mbegu tumeshaziwekea dawa za awali.

Meshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viuatilifu huu ndiyo mwaka wa kwanza tunaanza na *open stock* ya milioni 2.5. Kwa hiyo, wakulima watakapopanda tunawapelekea na dawa *immediately* ili wasiweze kupata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa maelekezo kuhusu pamba. Tuliamua mwaka huu wakulima wanunue mbegu kwa kujinunulia lakini tumeiona changamoto. Nataka niwaambie wakulima wa pamba na wadau wa pamba, tunafanya jitihada kama Wizara kutafuta fedha *ku-finance* mbegu hizi ili zao la pamba tuweze kuwagawia wakulima dawa na mbegu bure kama tulivyofanya mwaka jana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia, nilikuona. Swali fupi la nyongeza na ndiyo la mwisho kwa nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakulima wa Mkoa wa Kagera kwa muda mrefu wamekabiliwa na changamoto ya mnyauko wa migomba na haikupatiwa ufumbuzi. Hivi sasa kumekuja mnyauko na miche ya kahawa kwa hiyo, mkahawa mkubwa unanyauka. Nataka nipate kauli ya Serikali nini mkakati wao wa kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Kagera na hasa Wilaya ya Kyerwa na Karagwe. Kupambana na

changamoto ya kukauka kwa mikahawa yao kutokana na hiyo homa ya virusi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Anatropia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu ni kwamba wataalam wa *TARI* baada ya Wizara kupokea taarifa juu ya athari ya mnyauko wa kahawa, hivi ninavyoongea leo wana zaidi ya siku Saba wako Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kufanya utafiti na kuweza kutafuta *solution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kutoa jibu fupi ambalo halina uhakika hapa, tusubiri wataalam warudi watatupa majibu lakini tunatafuta *solution*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa ni swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Na. 75

**Hitaji la Masoko ya Kisasa ya kuuzia Samaki – Wilaya ya Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga masoko ya kisasa ya kuuzia samaki hasa katika Kata ya Somanga na Kivinje ambazo upatikanaji wa samaki ni mkubwa ili kuboresha maisha ya wavuvi wa Wilaya ya Kilwa kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kasmazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kata ya Somanga na Kata ya Kivinje ni miongoni mwa maeneo yenye samaki wengi katika Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia mradi wa *IFAD* imetenga fedha kiasi cha shilingi 211,698,940 kwa ajili ya ujenzi wa mitambo ya kuzalisha barafu. Wilaya ya Kilwa ni moja ya maeneo ambayo mitambo ya kuzalisha barafu itajengwa ili kusaidia kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutekeleza mipango ya kuboresha miundombinu ya uvuvi, ikiwemo masoko ya kisasa ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na Kata ya Somanga na Kivinje katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kadri fedha zinavyopatikana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa kwa muda mrefu wavuvi wadogo wadogo kutoka katika Wilaya ya Kilwa na maeneo mengine ya nchi yetu ya Tanzania wamekuwa hawapati mikopo kutoka kwenye mabenki kwa ajili ya kufanyia shughuli zao mbalimbali za kuboresha shughuli za uvuvi.

Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuweza kuwaundia hawa wavuvi wadogo wadogo mfuko maalum ambao wataweza kukopa kwa riba ndogo na hatimae hiyo mikopo iweze kuwanufaisha katika kufanya shughuli zao za uvuvi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Wilaya ya Kilwa kumekuwa na wimbi kubwa la uingiaji wa wafugaji wenye mifugo mingi sana hasa katika Kata za Somanga, Tingi, Kandawale, Njinjo, Mitole, Likawage, Nanjilinji pamoja na Kikole.

Je, Mheshimiwa Waziri ni lini atafika katika Wilaya ya Kilwa ili kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Kilwa kwenda kutatua changamoto mbalimbali zinazotokana na uingiaji wa mifugo mingi katika Wilaya ya Kilwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndulane Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Uvuvi kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo waweze kupata mikopo ya bei nafuu na yenye riba ndogo. Ninaungana na yeye na ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Wabunge wote ambao wanasimamia wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa miaka mitano tulionao Wizarani mwaka 2021-2016 wa kuhakikisha tunaupa nguvu uchumi wa *blue,* jambo hili la kuanzishwa kwa *Fisheries Development Fund* (Mfuko wa Maendeleo ya Uvuvi) ni miongoni mwa jambo lililopewa kipaumbele. Kwa hivyo, Mheshimiwa Mbunge nikupongeze kwamba umelileta jambo ambalo tayari Serikali imeshaliona na kwa hivyo tunakwenda kulianzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la kuingia kwa mifugo. Tayari tumekwenda kufanya ziara na nimpe pole sana yeye na wananchi wote, lakini tumekwenda na tumezungumza na makundi mbalimbali, katika Wilaya ya Kilwa nilifika katika Kata ya Nanjilinji kwenda kuzungumza na

wananchi pale lakini niko tayari kurejea tena ili kusudi tuweze kufika kule kote alipotaja Mitole, Njinjo, Likawage, Kandawale na hata kule Miguruwe na Zinga Kibaoni, ili kuweza kwenda kuzungumza na wananchi kwa niaba ya maombi haya ya Mheshimiwa Mbunge na hatimaye kuweza kupata suluhu ya tatizo hili kubwa ambalo linawasumbua wananchi wa Kilwa Kaskazini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape nimekuona.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na kupongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, chini Rais Samia ya kufufua uchumi wa Mkoa wa Lindi ikiwemo kufufua mazungumzo ya Mradi wa *LNG*, lakini pia na utengaji wa shilingi billion 50 kwa ajili ya kujenga Bandari ya Uvuvi Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni lini mchakato huu wa ujenzi wa hii bandari ambao ni ukombozi mkubwa wa ukanda wetu utaanza? Kwa sababu ahadi iliyokuwepo ni kwamba mchakato huu ungeanza mapema pamoja na kumshukuru Mama Samia kwa kazi hii nzuri lakini lini mchakato huu utaanza wa kujenga bandari hii kwa ajili ya uvuvi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Ulega Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye Mbunge wa Mtama Mkoa wa Lindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze sana kwa swali hili zuri na la kimkakati. Ujenzi wa bandari ya Uvuvi umetamkwa kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, nasi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kwake na msukumo wake wa kuhakikisha kwamba mradi huu wa

kimkakati wa ujenzi wa bandari unafanikiwa na hatimye kuweza kwenda sambamba na ile zana ya uchumi wa *blue*. Tayari wataalamu wetu wameshafanya hatua zote za mwanzoni na imekubalika kitaalamu ya kwamba bandari ile itakwenda kujengwa pale Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa wataalam wapo katika hatua za mwisho kabisa ya kuweza kuli-*demarcate* kuliweka sawa lile eneo linalokwenda kuwekwa bandari ile. Na tunashukuru sana kwa kuwa eneo hili ni eneo la kimkakati la kuelekea kule katika bahari kuu. Hivyo kile kilio cha muda mrefu cha Wabunge wengi na Watanzania wengi cha kwamba nchi hainufaiki ipasavyo na bahari yetu sasa kinakwenda kupata muarobaini wake. Kwa kweli tunamshukuru Mheshimiwa Rais hata kwa zile pesa za kununua meli nane ambapo sisi Tanzania bara tutapata meli nne zitakazo kwenda kuvua upande wa bahari kuu. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuoa Mheshimiwa Saashisha na Mheshimiwa Felista.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, Wilaya ya Hai inawafugaji wengi sana wa ng'ombe wa kisasa, ng'ombe walionenepeshwa lakini pia ng'ombe wale wa kienyeji pia tuna Uwanja wa Ndege wa Kimataifa na tuko tayari kufanya biashara ya Kimataifa ya kuuza nyama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza machinjio ya kisasa katika eneo la *KIA* ili na sisi tuweze kufungua milango ya kibiashara ya kuuza nyama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mafuwe Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wafugaji wa Hai ni wafugaji wa ng'ombe wa kisasa wanafuga katika utaratibu ule wa *zero grazing*, ni katika maeneo yanayofuga vizuri sana na viwanda vidogo vidogo vya maziwa viko pale Hai. Lakini vile vile Hai wanavyo viwanda vya chakula vya mifugo, hongera sana Mheshimiwa Mafuwe na wananchi wote wa Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini tutajenga machinjio ya kisasa, ninaomba Mheshimiwa Mafuwe wewe na waheshimiwa madiwani wenzako katika Halmashauri ya Hai muanzishe mpango huu, na sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tutakuwa tayari kushirikiana nanyi katika kuwapa utaalam na mchango mwengine wowote wa kuhakikisha jambo na wazo hili zuri linatimia pale Hai, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista nimekutaja.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, katika jimbo la kawe Kata ya Mbweni kuna wavuvi wengi wadogo wadogo na upatikanaji wa samaki ni mwingi sana lakini wavuvi wele hawana soko la uhakika pale, hawana sehemu maalum ya kuuzia. Ni lini Serikali itajenga soko la uhakika katika Kata ya Mbweni ili kuinua uchumi wa wavuvi wadogo wadogo na kuinua pato la Taifa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felisha Njau kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika maeneo ambayo yana wavuvi wengi kwenye Jimbo la Kawe wako wavuvi pia. Hapa karibuni nilikwenda kwenye *Beach* ya Kawe kwa maana ya *Kawe Beach,* ambako pale lipo Soko la Wavuvi, tayari tumetoa maelekezo kwa wataalam wetu kwenda kuzungumza na viongozi wa eneo lile wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani kijana Mheshimiwa Lwakatare, kwa

ajili ya kukaa na wavuvi wale na kupanga mpango tuweze kushirikiana na Hamnashauri ya Wilaya ya Kinondoni ambayo ina mapato mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tutashirikiana nayo kuhakikisha kwamba tunatengeneza soko zuri ni mahali pazuri ambako tunaweza kuvua kutengeneza samaki na watu waweze kwenda pale *weekends* ku-*enjoy* samaki wa baharini, ni samaki wazuri sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, sasa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambayo ni Wizara ya mwisho kwa leo, swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge wa Maswa Mashariki.

Na. 76

**Ujenzi wa Barabara ya Kolandoto – Meatu**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kolandoto hadi Meatu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kolandoto – Mwanhuzi (Meatu) yenye urefu wa kilometa 117.57 ni sehemu ya Mradi wa Barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi –

Sibiti – *Oldeani B Junction* yenye urefu wa kilometa 328 usanifu wake ulikamilika mwaka 2017. Serikali inaendelea na jitihada na juhudi za kutafuta fedha ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikiendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 1,240.246 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani na wewe mwenyewe ni shahidi, usanifu umefanyika toka mwaka 2017 mpaka leo tunakwenda miaka mitano, sita bado Serikali inatafuta fedha ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hivi kweli Serikali mko *serious* na ujenzi wa barabara hii? Mheshimiwa Flatei alitaka mpaka kupanda juu ya meza, hivi mnawaambia nini wananchi wa maeneo haya, Serikali mna mpango wa kujenga barabara hii lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Mheshimiwa Waziri wananchi wa Maswa Mjini wanahitaji taa za barabarani kwa mujibu wa maelekezo yako Mheshimiwa Naibu Waziri taa 60 mmetuwekea taa 18 tu mwaka jana, mna mpango gani wa kumalizia taa zilizobaki katika mji wa Maswa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Godfrey.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stanslaus

Haroon Nyongo Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali iko *serious* kuijenga barabara hii ambayo nimeitaja inayoanzia Lalago, Mwanuzi, Hydom, Mbulu hadi Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo la Mwanuzi-Sibiti kwenye bajeti hii tumetenga kuanza na ujenzi na zimetengwa billion 5 na tumetoa kibali lianze kwanza kujengwa daraja linaloitwa Itembe. Lakini katika barabara hiyo ambayo ni muendelezo kipande cha Mbulu Hydom tayari tumeshatangaza barabara kilomita 23 na tunaomba kipande chote kile kitangazwe, kwa hiyo muda wowote tutatangaza kilomita zote 50 ikiwa ni muendelezo wa hiyo barabara kuhakikisha kwamba yote inakamilika. Kwa hiyo, Serikali iko *serious* na ndio maana kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili naomba nimuhakikishie kwamba tuliahidi tutakamilisha hizo taa 60 na nitoe wito ama nitoe maagizo kwa Meneja wa Mkoa wa Simiyu kuhakikisha kwamba zoezi hili linakamilika kama tulivyoahidi kama Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nimemuona Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Flatei halafu baadaye tutakwenda Ukumbi wa Msekwa Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. AIDA J. KHENANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Serikali imewekeza Bandari ya Kabo kwenye Wilaya ya Nkansi lakini changamoto kubwa ambayo inawafanya watu wasitumie bandari ile ni kwa sababu ya kukosa barabara ya kiwango cha lami cha kutoka Lyazumbi mpaka Kabwe na hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ningependa kujua ni lini mtajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naibu Waziri Eng Godfrey majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imewekeza kujenga Bandari kubwa ya Kabwe ili tuweze kufungua Mkoa wa Rukwa na Tanzania kwa ujumla kufanya biashara na DRC Congo, na ndio maana tumejenga bandari mpya kabisa ya Kabwe. Lakini baada ya kujenga tunajua lazima kuwe na barabara, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya kwanza barabara ilikuwa ni finyu.

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa hiyo kazi ya kwanza ni kuipanua ile barabara madaraja tunayabadilisha yote na barabara tunaipanua na magari yote yaweze kupitika. Na baada ya hapo sasa mpango unaofuata ni kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami lakini awamu ya kwanza ni kuipanua kubadilisha madaraja ili magari makubwa yaweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Barabara ya Aliyazumbi Kabwe kama alivyoahidiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu itajengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Massay

**MHE. FLATEI G. MASSAY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imetangaza kilometa 25 nashukuru. Je, bajeti ya sasa ina kilometa 50 ni lini sasa utatangaza kilometa 50 ili kufikia Hospitali ya Hydom barabara ile kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa naibu Waziri majibu mafupi ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba kipande cha kilomita 50 kati ya Hydom na Mbulu tumetangaza kilomita 25 na Wizara tayari imepeleka maombi maalum ili kipande chote kile kiweze kutangazwa na loti nzima ikamilike kwa hiyo tuko kenye hatua nzuri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Cecil Mwambe kutoka Msekwa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza. Kuna wakati fulani sisi wakazi wa Mikoa ya Kusini hasa Mtwara huwa tunafikiri kama huwa hatuonekani na Wizara hii ya Ujenzi, na ninasema hivyo kwa sababu kuna barabara inayotoka Mtwara, Nivata, Newala, Masasi ikipitia Kata za Chikunja, Lukuledi kuelekea Ndomoni Nachingwea mpaka Liweke ilitengewa kipande hichi cha Masasi Nachingwea kilitengewa kiasi cha shilingi billioni 1.5 tu, na tulimuuliza Waziri kwamba anategemea kuanza wapi katika hili alijibu lakini hakuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kufahamu kipindi cha mvua kinakaribia kuanza sasa hivi na baadhi ya maeneo mvua zimeanza kunyesha na barabara hii wakati wa mvua huwa ni usumbufu mkubwa huwezi kufika Newala kirahisi hauwezi kufika Nachingwea kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ilitenga shilingi billioni 1.5 sasa sisi tunataka kufahamu ni lini hasa na Serikali ituambie kinaga ubaga barabara hii inakwenda kutengenezwa na kukamilika sio maneno maneno yanayotokea sasa hivi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mehsimiwa naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe kama ifuatavyo:

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Cecil, Mheshimiwa Cecil

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI – (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti samahani, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Wabunge wa Mtwara, Newala, Masasi na Ndanda kwamba barabara hii ya kilomita 210 ya kuanzia Mtwara Nivata, Ndanda, Newala hadi Masasi tumeshajenga kilomita 50 bado kilomita 160. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko kwenye asilimia zaidi 85 na Benki ya Maendeleo ya Afrika iko tayari kuijenga hii barabara na tunauhakika kufikia mwishoni mwa mwezi wa 11 huu tutakuwa tumekamilisha mazungumzo na tunauhakika kwamba wako tayari kuijenga hii barabara. Na kipande hiki cha Masasi kwenda Nachingwea tayari tumeshatenga billion 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali ya Awamu ya Sita haibabaishi ipo *serious* na kazi hii itafanyika ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante swali la mwisho la nyongeza kwa upande huu Mheshimiwa Ussi Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi swali la nyongeza. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa

barabara ya lami katika Barabara ya Iboni, Bolisa na Gubali katika Jimbo la Kondoa mjini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Pondeza Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa barabara zile ambazo ziko Kondoa mjini barabara nyingi zinahudumiwa na halmashauri kwa zile barabara ambazo zinahudumiwa na Wakala wa Barabara *TANROADS* naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajenga kama zilivyoainishwa kwenye mpango na kama ilivyo kwenye bajeti yetu ambavyo tumepanga, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri inawezekana Mheshimiwa Pondeza ameoa huko Kondoa kwa hivyo usishangae sana. Kwa hiyo, tunamalizia maswali yetu ya mwisho mawili kwa Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali, Mbunge wa Sumve. *(Makofi)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenekiti, nakushukuru, naomba niweke masahihisho naitwa Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali sio Kasala.

Na. 77

**Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba Kuunganishwa na Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza**

**MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza**:-**

Je, ni lini barabara ya kutoka Magu – Bukwimba hadi Ngudu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. *ENG*. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Magu – Bukwimba hadi Ngudu ni sehemu ya Barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu hadi Hungumalwa yenye urefu wa kilometa 71. Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii tangu mwaka 2019. Baada ya kukamilika kwa usanifu Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya Shilingi milioni 596.576 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Kasalali, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa swali la aina hii limeshaulizwa na Mheshimiwa Shanifu Mansour, Mbunge wa Kwimba na swali la aina hii liliulizwa na Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu. Pia mimi mwenyewe niliwahi kuuliza swali la nyongeza kwenye swali la aina hii. Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri aliyetoa majibu leo, ilitoa majibu tofauti na iliyoyatoa leo kwa sababu, ilisema imeshatenga pesa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kilometa 10 katika mwaka huu wa bajeti na katika bajeti hiyo ilionekana. Sasa nataka

kuuliza swali na kufahamu, je, Serikali katika ujenzi wa barabara hii inafahamu ni nini inahitaji kuwajibu watu wa Kwimba na Sumve au tunajibu tu ili muda uishe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; barabara hii imeshafanyiwa usanifu, kama majibu ya Serikali yalivyotolewa na kwa mujibu wa usanifu barabara hii, barabara mpya iliyosanifiwa itapita sehemu tofauti na inapopita barabara ya sasa katika eneo la Nkalalo ambapo kuna ujenzi wa reli ya *SGR.* Kwa sababu kwa mujibu wa ujenzi wa reli hii, hakuna barabara inaruhusiwa inaruhusiwa kupita juu ya reli. Ina maana reli hii ikimalizika kujengwa njia ya kutokea Kwimba kwenda Magu itakuwa imefungwa. Je, Serikali haioni kuna udharura wa kuanza ujenzi wa barabara hii ili kurahisisha usafiri wa watu na mizigo kutokea Kwimba kwenda Magu na kuiunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na Mkoa wa Mwanza kwa barabara ya lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika bajeti tuliyopitisha na bado sijaiondoa, tulitenga bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Katika jibu la msingi nimesema Serikali inaendelea kutafuta fedha na fedha ndio hii kwamba, tutakapopata sasa tutakuwa tunaanza ujenzi kwa sababu, hatujaanza, lakini ipo kwenye mpango na bado mpango huo haujafutwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hakuna majibu tofauti, majibu ni hayo na ndio bajeti tuliyopitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, huu udharura anaousema Mheshimiwa Mbunge, naomba nimhakikishie kwamba, kama Wizara tunalichukua na wataalam

watakwenda kufanya tathmini na kuangalia kama kinachosemwa kina ukweli, basi tutachukua ushauri na kulifanyia kazi kama kutakuwa na udharura huo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Swali letu la mwisho kwa siku ya leo na kwa Wizara hiyo ni la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini.

Na. 78

**Upungufu wa Mabehewa ya Abiria – Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, ni lini tatizo la upungufu wa mabehewa ya abiria na mizigo litatatuliwa katika Kituo cha Mpanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waitara, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* linakabiliwa na uhaba wa mabehewa ya abiria na mizigo. Ili kuondokana na changamoto ya upungufu wa mabehewa katika kituo cha Mpanda na sehemu zingine, Shirika linaendelea na ukarabati wa mabehewa na tayari limesaini mkataba wa ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 37 ya abiria na 600 ya mizigo. Aidha, mwezi Juni, 2021, Shirika limesaini mkataba wa ununuzi wa mabehewa mapya 22 ya abiria utakaotekelezwa kwa kipindi cha miezi 12 na katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022,

Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 18.8 kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa mapya 100 ya mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda, pamoja na wananchi wa Mpanda, kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na zoezi la ukarabati na ununuzi wa mabehewa ya abiria na mizigo. Ni matumaini yetu kuwa pindi mabehewa yatakapowasili nchini na ukarabati kukamilika, tatizo la uhaba wa mabehewa kwa sehemu kubwa litakuwa limepatiwa ufumbuzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nashukuru pia, majibu mazuri yenye kutia matumaini kutoka Serikalini. Hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; nafahamu tulikuwa na behewa la daraja la pili, lakini kwa bahati mbaya behewa hili lilipata ajali ya moto. Ni lini Serikali itaturejeshea huduma hiyo ya behewa la daraja za pili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kituo cha Mpanda kwa bahati mbaya sana wakati wananchi wakisubiri huduma ya usafiri, jengo lao la kusubiria huduma hiyo halipo. Ni lini Serikali pia, itatusaidia huduma hii muhimu ya jengo la kusubiria abiria? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waitara, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapufi, kwa faida ya wananchi wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama tutarejesha daraja la pili katika eneo hili. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge maombi

haya yamepokelewa. Tutazingatia maombi haya hasa katika mabehewa mapya ambayo yanaendelea kununuliwa angalau huduma hiyo iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, tumepokea pia hoja ya pili ya jengo la kusubiri abiria. Hili ni eneo muhimu kwa sababu kama kunakuwa na jua abiria wanahitaji kivuli, lakini pia kama ni wakati wa mvua inapaswa kujikinga. Namwelekeza Mtendaji Mkuu wa *TRC* atembelee eneo hili ufanywe mpango wa haraka kujenga jengo la kusubiria abiria ili wananchi waweze kupata huduma muhimu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara. Muda wetu wa maswali umeisha na hilo ndio swali letu la mwisho, sasa hivi ni wakati wa matangazo:-

Kuna wageni ambao walikuwepo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ambao wamesafiri; ni wageni watatu kutoka Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania ambao ni Ndugu Christine Mensah, Mkuu wa Kitengo cha Siasa wa Ubalozi. Ndugu Taylor Kofil, Afisa wa Masuala ya Siasa wa Ubalozi. Ndugu Chikulupi Kasaka, Msaidizi wa masuala ya siasa wa ubalozi. Hawa wameshasafiri, lakini walikuwepo asubuhi. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni watatu wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Mbunge na Naibu Waziri wa Nishati, ambao ni Ndugu zake kutoka Bukoba, Mkoani Kagera; Ndugu Godfrey Mwemezi, Ndugu Twaibu Juma na Ndugu James Michael. Karibuni sana katika Bunge letu ndugu zetu. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Zahor Haji, ambaye ni kada wa CCM kutoka Ilala, Jijini Dar-Es-Salaam, Ndugu Abdallah Mangara. Karibu sana mgeni wetu kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, ambao ni wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma

*(UDOM),* Ndugu Timotheo Kasmy na Ndugu Joseph Julius. Karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine wawili ni wa Mheshimiwa Erick Shigongo, ambao ni Maafisa Masoko kutoka *Global Publishers* ya Jijini Dar-es-Salaam, Ndugu Keneth Mlawa na Ndugu David Mwakyusa, ambao ni wageni wake hao Mheshimiwa Shigongo. Karibuni sana.

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Kuna wageni watano ambao ni timu ya Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* za Jijini Dar-es-Salaam waliokuja Bungeni kutoa huduma za matibabu na ushauri juu ya magonjwa mbalimbali ikiwemo moyo na saratani.

Waheshimiwa Wabunge, Madaktari hao ni Dkt. Fabian Kamana, Daktari Bingwa wa Moyo na Magonjwa ya Ndani. Dkt. Emmanuel Lugina, Daktari Bingwa wa Saratani. Dkt. Magdalena Denis, Daktari wa Magonjwa ya Ngozi. Dkt. Stephen Kaali, Daktari Bingwa wa Figo, Njia ya Mkojo, Kibofu, Uume na Uke - Dkt. Nathaniel Mtinangi, Daktari Bingwa wa Uzazi, Magonjwa ya Kike na Upasuaji wa Fistula. Karibuni sana Madaktari wetu Bingwa katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni Ndugu Eluleki Haule, mwanafunzi wa darasa la saba aliyeshika nafasi ya kwanza Tanzania kutoka *St. Anne Maria Academy.* Hongera sana na karibu katika Bunge letu. Ndugu Evaristo Haule ni baba yake mzazi huyo mwanafunzi wetu. Ndugu Digta Mlengule, mama yake. Ndugu Amos Joseph, Mwalimu Mkuu wa *St. Anne Maria Academy.* Karibuni sana na hongereni sana kwa kufanikisha na kuwa wa kwanza katika masomo yake kijana wetu na hongereni Walimu pia. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu kutoka Wilaya ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro, Ndugu Abdallah Thabit. Karibu sana Ndugu Abdallah Thabit.

Kuna wanafunzi 70 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni wanafunzi na Walimu kutoka Shule za Msingi za Sokoine, Njoro na Uhuru zilizopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, wakiongozwa na Afisa Elimu wa Manispaa ya Moshi, Ndugu Nicholaus Ngonyani. Wanafunzi wetu karibuni sana katika Bunge letu kutoka huko Moshi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo hapa limeletwa kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu semina mbili. Kuna semina kuhusu hali ya upatikanaji na udhibiti wa dawa nchini itakayofanyika tarehe 11 Novemba, 2021 kuanzia saa 3.00 asubuhi. Semina hii itatolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kesho tarehe 11.

Semina nyingine ni kuhusu hatua iliyofikiwa katika maboresho ya mitaala ya elimu nchini, itakayofanyika tarehe 12 Novemba, 2021 kuanzia Saa 3.00 asubuhi itakayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hizo muhimu bila kukosa.

Katibu, tuendelee.

**NDG. ZAINAB ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge na Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009

**MWENYEKITI:** Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, karibu.

**MHE. DKT. JASSON SRWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na utangulizi. Nakushukuru kwa kutoa idhini ili Kamati iwasilishe Taarifa ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge, pamoja na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii itasaidia Bunge katika ufuatiliaji na udhibiti wa mamlaka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali Serikalini. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza ambayo ni utangulizi, inatoa maelezo ya jumla; Sehemu ya Pili ni maelezo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa; Sehemu ya Tatu ni maoni ya Kamati kuhusu dosari zilizobainika; Sehemu ya Nne ni mapendekezo na maazimio ya kuhitimisha hoja hiyo; na Sehemu ya Tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inasomwa kwa pamoja na jedwali la uchambuzi lililoambatanishwa ambalo ni sehemu ya taarifa hii na linaingia kwenye kumbukumbu za majadiliano ya Bunge, Taarifa Rasmi *(Hansard).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, ili taarifa hii iwe na tija iliyokusudiwa kuna haja ya kurejea maelezo kuhusu madaraka ya kutunga sheria nchini, udhibiti wa kibunge wa sheria ndogo na Kamati ilivyosaidia udhibiti wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madaraka ya Kutunga Sheria. Ibara ya 4 na ya 64 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 77 imelipa Bunge mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania Bara. Pamoja na mamlaka hayo ya Bunge, Ibara ya 67(5) ya Katiba inaliruhusu Bunge kukasimu madaraka hayo ya kutunga sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo; udhibiti huu ni wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola wenye lengo la kuliwezesha Bunge kujiridhisha iwapo madaraka ya kutunga sheria iliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine umefanyika ilivyokusudiwa na Bunge lenyewe. Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Madola hutumia utaratibu huu kwa kuweka kifungu kwenye sheria mama kinachobainisha madaraka yaliyokasimiwa katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kutunga na kudhibiti wa sheria ndogo nchini Tanzania upo katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza. Kifungu cha 37(1) na (2) cha sheria hii kinataka sheria ndogo itangazwe kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika.

Aidha, kifungu cha 38(1) cha sheria hiyo kimeweka sharti la sheria ndogo zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwasilishwa au kuwekwa Mezani Bungeni ndani ya siku sita za vikao vya Bunge vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapishwa kwa gazeti hilo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Kudumu za Bunge pia zimeweka utaratibu wa sheria ndogo zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwasilishwa Bungeni. Baada ya sheria ndogo kuwekwa Mezani, Kanuni ya 43(8) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inataka sheria ndogo hizo zijadiliwe na Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo na uchambuzi ukikamilika Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Mheshimiwa Spika kwa maandishi kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti hayo ya kanuni za Bunge yamezingatiwa na yamemwezesha Mheshimiwa Spika kuagiza Taarifa hii iwekwe kwenye orodha ya shughuli za leo. Naomba niliombe Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye litoe maamuzi na maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namna Kamati Iliyofanya Kazi; katika kutekeleza jukumu la kuchambua sheria ndogo, kamati ilitumia njia na mbinu kuu zifuatazo:-

(1) Kufanya uchambuzi wa awali;

(2) Kuwaalika wadau ili kupata uhalisia wa mazingira ya utekelezaji wake;

(3) Kujadiliana na mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika ili kupata muktadha wa utungaji na utekelezaji wa sheria hiyo; na

(4) Kufanya uchambuzi kwa kuhusianisha, kulinganisha, kuoanisha, kufananisha na kutofautisha matokeo ya uchambuzi wa awali, maoni ya wadau na majadiliano kati ya Kamati na Mamlaka ya iliyotunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia hii na mbinu mbalimbali za uchambuzi wa awali ziliiwezesha Kamati kubaini sheria ndogo zenye dosari za aina tano zifuatazo:-

(1) Kukiuka masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(2) Kuwa kinyume na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi;

(3) Kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria;

(4) Kutoendana na uhalisia; na

(5) Makosa ya uandishi katika majedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau na jamii nzima ndio wanaguswa moja kwa moja na sheria ndogo. Iwapo wadau wasingealikwa, isingekuwa rahisi kujiridhisha na namna sheria ndogo inavyowezesha ustawi wa wananchi ambao ni lengo kuu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilikutana na kujadiliana na mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zilizochambuliwa na kwa lengo la kupata ufafanuzi wa dosari zilizoibuliwa, majadiliano hayo yaliwezesha kamati kufanya uchambuzi inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sehemu inayofuata katika taarifa hii inahusu uchambuzi wa Sheria Ndogo. Sehemu hii italiwezesha Bunge kujadili na hatimaye kufanya maamuzi kwa manufaa ya wananchi. Naliomba Bunge lako Tukufu liendelee kuona Sheria Ndogo haziwi kero kwa wananchi wala kikwazo kwa ustawi wa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili; Uchambuzi wa Sheria Ndogo mnamo tarehe 9 Aprili, 2021 na tarehe 7 Septemba, 2021 Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na nyongeza zake zikiwemo Sheria Ndogo 487.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi Kamati ilitumia vigezo vifuatavyo:-

1. Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

2. Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo inayohusika;

3. Uzingatiaji wa misingi bora ya uandishi wa sheria;

4. Uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu au faini iliyotiliwa maanani; na

5. Usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya Sheria Ndogo inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yanabainisha jumla ya dosari 70. Kwa urahisi wa kufuatilia

dosari hizo, taarifa hii imeambatanisha jedwali la uchambuzi kwa rejea wakati wa mjadala na uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dosari za kuzingatia masharti ya Katiba; nchini Tanzania Katiba ina ukuu wa sheria za nchi na kwa sababu hiyo, sheria zote za nchi ni zao la mgawanyo wa madaraka uliowekwa na Katiba. Hivyo, Bunge haliwezi kuruhusu mamlaka nyingine kutunga Sheria Ndogo zenye masharti yanayokiuka masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni Sheria Ndogo ya Kudhibiti Omba Omba ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya Mwaka 2021 ambapo Kifungu cha 2 cha sheria hiyo kinatafsiri neno "omba omba" kuwa ni mtu yeyote mwenye ulemavu au asiye na ulemavu anayeishi na kutegemea kuomba omba chakula au fedha au vitu vingine kutoka kwa watu wengine kwenye mitaa na maeneo ya wazi yaliyoko ndani ya eneo la Halmashauri. Tafsiri inaainisha watu katika makundi kulingana na ulemavu au kutokuwa na ulemavu. Hii inaweza kutoa mtazamo wa kibaguzi kwa kundi la watu wenye ulemavu kuonekana ni watu wenye hadhi ya ombaomba jambo ambalo siyo halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 na ibara ndogo ya (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweka marufuku kuweka aina yoyote ya ubaguzi katika sheria yoyote. Nanukuu: "*Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama kwa dhahiri au kwa taswira yake.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu halitarajiwi kupuuza matumizi ya Kifungu cha Sheria Ndogo kinachoonyesha hali ya kubagua kundi la watu wenye ulemavu kwa sababu jambo hilo ambalo limekatazwa na Katiba kukinzana kwa masharti ya Sheria Mama na sheria nyingine za nchi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, punguzeni sauti tumsikilize Mwenyekiti

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linaporuhusu mamlaka inayohusika kutunga Sheria Ndogo, hufanya hivyo kwa madhumuni maalum yanayoendana na lengo kuu la Sheria Ndogo au Sheria Mama na sheria nyingine za nchi. Kwa hiyo, uchambuzi umeonesha uwepo wa Sheria Ndogo zenye dosari za kukinzana na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni Sheria Ndogo ya *The Environmental Management Registration and Practice of Environmental of Experts Regulations 2021.* Kanuni ya 32, kanuni ndogo ya (1) imeweka masharti yanayomkataza Ofisa wa Umma aliyesajiliwa kama mtaalamu wa mazingira kufanya tathmini ya mazingira katika miradi hiyo chini ya taasisi yake ili kuepuka mgongano wa maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katazo lililowekwa na kanuni ya 32 linaondolewa na kanuni ya 32 (2) ambayo inamruhusu Ofisa wa Umma aliyesajiliwa kama mwana taaluma wa mazingira kufanya shughuli ya tathmini za mazingira zinazohusu taasisi yake, hali inayoondoa mantiki ya katazo lililowekwa katika kanuni ya 32(1) kuhusu mgongano wa maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaowekwa na kanuni ya 32 (2) ni kinyume na misingi ya kudhibiti mgongano wa maslahi kwa mujibu wa maadili ya watumishi wa Umma. Iwapo Bunge lako Tukufu litaruhusu jambo hilo, basi litakuwa linabariki uvunjaji wa misingi ya mgongano wa maslahi hali ambayo inaweza kuathiri uwajibikaji wa Maofisa wa Serikali walioshiriki katika kufanya tathmini ya athari za mazingira kwa miradi inayotokana na taasisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kutoendana na misingi bora ya uandishi wa sheria. Sheria zinazotungwa na Bunge huzingatia misingi bora ya uandishi wa sheria. Matokeo

ya uchambuzi yameonyesha Sheria Ndogo kukiuka misingi ya uandishi wa sheria. Mfano ni Sheria Ndogo kwa sheria za ada na ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya uandishi katika Sheria Ndogo hizo inahusu kipengele cha 12 cha sheria na jedwali Na. 6 kinachoorodhesha aina ya vitu vinavyopaswa kutozwa ushuru. Idadi hiyo inatofautiana na idadi ya viwango vya ushuru vilivyoorodheshwa. Idadi ya aina za vitu vinavyopaswa kutozwa ushuru ni saba lakini viwango vya ushuru vinavyoainishwa ni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti hiyo inaweza kuwa imesababishwa na kusahaulika kwa kitu kinachotozwa ushuru au kuongezeka kwa kiwango cha ushuru kilichotajwa. Hali hiyo inaweza kuathiri chanzo cha mapato ya Halmashauri kinyume na makusudio ya sheria. Hii na kusababisha utozaji usiotabirika unaotokana na kukosekana kwa mwongozo dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu haliwezi kuona mazalio ya kero kwa wananchi wa Bumbuli au kwingineko nchini bila kuchukua hatua muhimu za kuondoa kero hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni kukosa uhalisia. Utungaji wa sheria ya pamoja na mambo mengine huangalia uhalisia wakati wa utekelezaji ikiwemo hali halisi ya mazingira ya watumiaji na walengwa wa sheria inayohusika. Kamati imebaini Sheria Ndogo kuwa na vifungu visivyo na uhalisia; mfano ni kanuni za uvuvi 2009 ambazo kanuni ya 13 (22) inaelekeza mtu anayetaka kuomba kuuza nje ya nchi au kuingiza bidhaa za samaki zitokanazo za uvuvi, kujaza fomu ya maombi na kuambatanisha cheti cha ukamilifu wa kampuni (*Certificate of Incorporation)* na Katiba au hati ya kanuni za kampuni, *Memorandum and Authorization.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti haya siyo halisia kwa waombaji ambao ni wamiliki wa kampuni, kwani katika hali ya kawaida mtu ambaye sio kampuni hawezi kuwa na

viambatanisho hivyo kwa kuwa ni mahususi kwa makampuni na siyo kwa mtu binafsi. Ni dhahiri kwamba masharti hayo yanakwamisha ushiriki wa watu binafsi katika shughuli za usafirishaji wa samaki na mazao ya samaki nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge haliwezi kutunga sheria inayokasimu utungaji wa Sheria Ndogo zisizo na uhalisia katika utekelezaji wake. Hivyo haliwezi kuruhusu mamlaka inayoruhusiwa kutunga Sheria Ndogo ifanye hivyo kwa kukinzana na uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, makosa ya uandishi wa majedwali ya Sheria Ndogo. Majedwali husaidia kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina wa kifungu au kanuni inayohusika. Inapotokea majedwali ya sheria yana dosari ya kutorejea kanuni sahihi, kurejea kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa kanuni au maudhui kutokana na kifungu wezeshi, inaathiri mantiki, madhumuni na maudhui ya jumla ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa dosari ya uandishi wa majedwali upo katika Sheria Ndogo ya *The Civil Aviation Training Center and Management of Operation Rules.* Jedwali la kanuni hizi linaonyesha kuwa limeanzishwa chini ya kifungu cha 93 ambacho hakipo. Kosa hilo la uandishi linaning'iniza jedwali katika mtiririko wa uandishi wa kuharibu azma ya ufafanuzi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya kutorejea kifungu sahihi inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria inayohusika na wakati mwingine kusababisha mkanganyiko. Kwa kuwa majedwali katika sheria hulenga kutoa ufafanuzi wa zaidi ya maudhui yaliyo katika vifungu, kutokuandika jedwali kwa ufasaha kunasababisha mkanganyiko katika sheria na hivyo kuathiri malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge halitaacha kusisitiza mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria au kanuni ndogo nyingine kuzingatia uandishi bora wa majedwali katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ni maoni. Maelezo niliyoyatoa katika aya zilizotangulia yanadhihirisha kuwa Sheria Ndogo hutungwa mara kwa mara kulingana na mahitaji yanayojitokeza. Hivyo, kuna umuhimu wa utaratibu madhubuti wa kuhifadhi na kulinda heshima ya mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo. Bunge ambalo ni chombo kikuu cha kutunga sheria linaendelea kuwa na wajibu wa kuangalia utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge kupitia Kamati ya Sheria Ndogo yenye jukumu la kuchambua Sheria Ndogo, imetekeleza majukumu yake na kuonyesha matokeo ya uchambuzi kama ilivyofafanuliwa. Katika sehemu hii naomba kubainisha mtazamo wa jumla wa Kamati kuhusu aina tano za dosari za uchambuzi kwa namna ya maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kamati inabainisha maoni katika maeneo makuu matano yafuatayo:-

1. Kutozingatiwa kwa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutozingatiwa kwa misingi inayowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uandishi wa Sheria Ndogo kunaweza kusababisha mifumo, taasisi na muelekeo wa jamii kutoendana na misingi ya Katiba. Ikiwa hivyo, inaweza kusababisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ukiukwaji wa upatikanaji wa haki mbalimbali zikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

2. Kukinzana na masharti ya Sheria Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na Sheria Mama inaathiri tija ya utekelezaji wa sheria. Dosari hiyo ikiendelea masharti yaliyowekwa kwenye Sheria Mama kwa lengo la kuiwezesha mamlaka inayohusika kutunga Sheria Ndogo itakosa maana. Hali hiyo ni kinyume

na misingi ya utungaji wa Sheria Ndogo na Bunge haliwezi kupuuza au kuruhusu misingi hiyo.

3. Kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi bora wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa sheria zote kuendana na misingi ya uandishi bora wa sheria, dosari za Sheria Ndogo kutoendana na utaratibu bora wa uandishi wa sheria siyo jambo la kuachwa katika Sheria Ndogo. Dosari hizo zinaweza kuashiria utekelezaji wa Sheria Mama usio na tija. Bunge halipaswi kuruhusu dosari za aina hiyo kuendelea kuwepo katika Sheria Ndogo.

4. Sheria Ndogo kutokuwa halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo zinapokuwa na maudhui yasiyozingatia hali ya uchumi wa walengwa au urahisi wa utekelezaji wake, inakosa uhalisia. Ni kweli kuwa sheria yoyote isipotungwa kwa kuzingatia uhalisia wa mambo inaweza kutatiza utekelezaji wake. Bunge linapaswa kujiridhisha na kuhakikisha kuwa dosari za Sheria Ndogo za kutoenda na uhalisia zinarekebishwa.

5. Kukosekana kwa usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali ya Sheria Ndogo inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya majedwali katika uandishi wa Sheria Ndogo ni jambo la kuzingatiwa katika uchambuzi wa sheria. Dosari ya kukosekana kwa usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali ya Sheria Ndogo inayohusika inaweza kusababisha mkanganyiko wa maudhui ya sheria inayohusika. Bunge linapaswa kusisitiza usahihi na ufasaha wa uandishi wa jedwali ili kuwezesha ukamilifu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lizingatie maelezo ya jumla niliyoyatoa, ufafanuzi wa matokeo ya uchambuzi wa Maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa

uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja ili Bunge lako liazimie kama ifuatavyo:-

1. Kutozingatiwa kwa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na masharti yanayokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jambo lisiloweza kukubaliwa na Bunge;

NA KWA KUWA, kutofanya marekebisho katika Sheria Ndogo hizo kunaweza kusababisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, kukosekana kwa haki mbalimbali zikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka iliyotunga Sheria Ndogo inayokinzana na sheria na Katiba ifanye marekebisho yanayostahili.

2. Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo au sheria nyingine za nchi.

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zimebainika kuwa na vifungu vilivyokinzana na masharti ya Sheria Mama na sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria Mama inayohusika;

NA KWA KUWA, Sheria Ndogo inayokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi, haiendani na masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria hali inayosababisha kuwa batili kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zenye kukinzana na masharti ya

Sheria Mama na sheria nyingine za nchi zirekebishe Sheria Ndogo hizo.

3. Kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria.

KWA KUWA, uchambuzi umebainisha Sheria Ndogo ambazo hazikuzingatia misingi ya uandishi wa sheria;

NA KWA KUWA, kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi wa sheria kunasababisha tatizo la sheria kutoeleweka kwa urahisi na kutotabirika hali inayoathiri tija ya utungaji wa sheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo hizo zifanye marekebisho.

4. Dosari ya uandishi wa majedwali.

KWA KUWA, imebainika baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari katika uandishi wa majedwali ilhali Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinatambua majedwali kuwa ni sehemu ya sheria;

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaathiri ukamilifu na kukatiza utekelezaji wa sheria inayohusika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali yake zifanye marekebisho.

5. Masharti yasiyokuwa na uhalisia.

KWA KUWA, zipo baadhi ya Sheria Ndogo zenye masharti yaliyokinzana na uhalisia;

NA KWA KUWA, masharti hayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa tija inayokusudiwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizopewa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo zinazobainika kuwa na dosari za kutoendana na uhalisia, zifanye marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi kuwasilisha taarifa hii Bungeni. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika binafsi na Bunge lake Tukufu kwa kuweka utaratibu endelevu unaowezesha taarifa ya Kamati kuwasilishwa Bungeni katika Bunge lake Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kuendelea kuweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatanisho vyake, Sheria ndogo. Hii imesaidia Kamati kufanya uchambuzi wenye ufanisi mkubwa. Pia nawashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara katika Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawashukuru wadau waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao ambayo yameisaidia Kamati kufanya uchambuzi kwa kina katika kanuni hizi. Kipekee nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi *ndc.* kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein *ndc.* na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Mkuta

Masoli, Ndugu Stanslaus Kagisa na Ni Imelda Ntimba Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA TATU, TAREHE 09 APRILI, 2021 NA MKUTANO WA NNE, TAREHE 7 SEPTEMBA, 2021 PAMOJA NA KANUNI ZA UVUVI ZA 2009 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini chini ya Kifungu cha 11 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 ili Kamati iwasilishe **Taarifa yake ya Pili ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.**

**Mheshimiwa Spika,** fursa hii adhimu, inaiwezesha Kamati kulisaidia Bunge katika ufuatiliaji na udhibiti wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini. Naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Taarifa hii itavutia majadiliano kuhusu sheria ndogo zilizochambuliwa. Uhakika huo unatokana na mambo makuu matatu:-

(i) Jinsi hoja mbalimbali zinavyofafanuliwa katika taarifa hii;

(ii) Namna iliyotumika kubainisha dosari na madhara yake; na

(iii) Maoni ya Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hiyo, Kamati imeona umuhimu wa kuonesha mawanda (*scope*) ya maudhui (*content*) ya taarifa hii ili kuwezesha ufuatiliaji wenye ufanisi. Kwa madhumuni hayo, nitangulie kueleza kuwa taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza ambayo ni ya utangulizi inatoa maelezo ya jumla kuhusu madaraka ya kutunga sheria, udhibiti wa sheria ndogo na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya pili ambayo ni maelezo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge, inafafanua matokeo na dosari zilizobainika;

(iii) Sehemu ya Tatu ambayo ni maoni na mapendekezo inaeleza mtazamo wa Kamati kuhusu hoja zilizobainika wakati wa uchambuzi; na

(iv) Sehemu ya Nne inabainisha mapendekezo ya maazimio kuhusu dosari zilizojitokeza na kuhitimisha kwa kutoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, muundo huo wa taarifa pamoja na uwasilishaji wake unalenga kufanikisha mjadala wa Bunge utakaowezesha uamuzi wenye manufaa kwa wananchi. Aidha, ili kuwezesha rejea kwa urahisi, Taarifa hii inasomwa kwa pamoja na Jedwali la Uchambuzi lililoambatishwa ambalo ni sehemu ya Taarifa hii na linaingia kwenye kumbukumbu za majadiliano ya Bunge (Taarifa Rasmi za Bunge). Jedwali hilo linabainisha dosari katika jumla ya sheria ndogo ishirini na tatu (23) ambazo ni sehemu ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo hayo**,** nilikumbushe Bunge hili kuwa ili taarifa hii iwezeshe tija iliyokusudiwa, kuna umuhimu wa kurejea maelezo kuhusu madaraka ya kutunga Sheria nchini, Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo na Kamati inavyosaidia udhibiti wa sheria ndogo. Baada ya ufafanuzi huo ambao ni msingi mkuu wa majadiliano ya Bunge lako

tukufu, Taarifa hii inabainisha matokeo ya uchambuzi ili kuonesha chimbuko la maoni ya Kamati na kubainisha hoja na mapendekezo juu ya uamuzi wa Bunge unaotarajiwa.

## 1.2 Madaraka ya Kutunga Sheria

**Mheshimiwa Spika**, madaraka ya kutunga sheria zote nchini yamewekwa chini ya mamlaka ya Bunge. Ibara ya 4 na 64 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Kama ilivyofanyiwa Marekebisho mara kwa mara), imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mamlaka hayo ya Bunge, Ibara ya 97 (5) ya Katiba inaliruhusu Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Utaratibu huo ni wa kawaida katika utungaji wa sheria. Miongoni mwa sababu za utaratibu huo ni umuhimu wa kuzingatia utaalamu mahsusi unaopatikana katika mamlaka mbalimbali za kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na msingi huo , utaratibu huu ni halali na unafaa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini unatumika kwa madhumuni maalumu tena kwa kuweka mipaka, ukomo au upeo kwa namna yenye udhibiti. Msimamo huu si wa Bunge la Tanzania pekee bali unakubalika na kutumika pia katika mabunge mengine duniani. Kwa kawaida Mabunge duniani yanahitaji kuhakikisha kuwa madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika vizuri bila kuwa kero au kusababisha udhia kwa wananchi. Kuwezesha hilo, Mabunge duniani hutumia utaratibu unaozingatia mambo yafuatayo:-

(i) Madaraka ya kutunga sheria ndogo hukasimiwa kwa mamlaka yenye kuaminika na kukubalika kitaifa;

(ii) Wigo na mipaka ya sheria ndogo inayoweza kutungwa katika utekelezaji wa Sheria Mama (*Principal legislation*) huwekwa bayana;

(iii) Utekelezaji wa madaraka ya kutunga Sheria huelekezwa kuwahusisha wadau;

(iv) Mchakato wa utungaji wa sheria ndogo na matumizi yake hutakiwa kuwezesha sheria ndogo inayohusika ijulikane kwa umma; na

(v) Kujulikana kwa mfumo, utaratibu na mamlaka inayowezesha marekebisho au zuio la kutumika kwa sheria ndogo iwapo kama itahitajika hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, jambo la kwanza hadi la tatu hufanyiwa kazi na Bunge kabla ya mamlaka inayohusika na utungaji wa sheria ndogo haijaanza utekelezaji wa mamlaka hayo. Jambo la nne na tano katika hayo, yanasisitiza msingi wa utaratibu unaotumiwa na Bunge la Tanzania kusimamia sheria ndogo nchini. Kwa mantiki hiyo, hoja inayojadiliwa katika kikao cha leo ni miongoni mwa hoja zinazohitaji ufuatiliaji, majadiliano na uamuzi unaozingatia hali halisi na maisha ya watu inavyostahili.

### 1.3 Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika,** Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ni utaratibu wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola. Utaratibu huu unalenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu iwapo utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine umefanyika ilivyokusudiwa na Bunge lenyewe. Udhibiti huo, hufanyika kwa kulinganisha sheria ndogo na masharti ya sheria kuu (Sheria Mama) pamoja na misingi mingine iliyowekwa na Sheria zilizotungwa na Bunge. Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Madola, hutumia utaratibu wa udhibiti wa sheria ndogo kwa kuweka kwanza kifungu kwenye sheria mama kinachobainisha

madaraka yanayokasimiwa katika sheria ndogo. Kifungu hicho kinaweza kuainisha sheria ndogo inayoweza kutungwa na mamlaka inayopewa madaraka ya kutunga sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, mchakato huo wa utungaji na udhibiti wa sheria ndogo nchini Tanzania umefafanuliwa katika *Sheria ya Tafsiri ya Sheria*, Sura ya 1, (*The Interpretation of Laws Act, Cap.* 1). Kifungu cha 37 (1) na (2) cha Sheria hii kinataka sheria ndogo itangazwe kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika. Aidha, kifungu cha 38 (1) cha Sheria hiyo kimeweka sharti kwa sheria ndogo zinazotangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwasilishwa (kuwekwa mezani) Bungeni ndani ya siku sita za vikao vya Bunge vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapisha toleo la Gazeti lililotangaza Sheria Ndogo hizo. Masharti hayo yamewekewa utaratibu katika mchakato wa Kibunge kwa kufafanuliwa na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 43 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka utaratibu wa sheria ndogo zilizotangazwa katika gazeti la serikali kuwasilishwa Bungeni. Baada ya sheria ndogo kuwekwa mezani, Kanuni ya 43 (8) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inataka sheria ndogo hizo zijadiliwe na Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo. Katika Utaratibu huo, Kifungu cha 11 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kinaelekeza kuwa, Kamati inapokamilisha kazi ya uchambuzi Mwenyekiti wa Kamati anapaswa kumjulisha Spika kwa maandishi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo ya Kanuni za Bunge yamezingatiwa ipasavyo na kukuwezesha kutumia mamlaka uliyopewa chini Kifungu cha 11 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kuagiza Taarifa hii iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Leo. Katika hatua hii, niliombe Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili kwa kina Taarifa ninayoiwasilisha na hatimaye litoe uamuzi kwa maazimio yanayotokana na Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge, Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi za 2009. Majadiliano hayo yazingatie kuwa Kifungu cha

38 cha *Sheria ya Tafsiri ya Sheria*, kimebainisha uwezo wa Bunge kufanya marekebisho katika sheria ndogo au kuibadilisha sheria ndogo inayohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Mantiki ya kuijadili Taarifa hii ni utaratibu na utamaduni wa mabunge duniani kufanya sehemu kubwa ya kazi yake kwa kutumia Kamati zake. Kwa desturi za kibunge, Taarifa hii ni nyenzo ya msingi kwa Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake wa kudhibiti sheria ndogo nchini. Katika kufanikisha wajibu huo wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo inaweza kutumia namna kuu mbili ambazo ni:-

(i) Kuchambua sheria zilizowekwa Mezani; na

(ii) Kuchambua sheria ndogo zinazoendelea kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge, Mkutano wa Nne wa Bunge na pamoja na Kanuni za Uvuvi zilizotangazwa mwaka 2009 zinazoendelea kutumika. Utaratibu huu wa kutumika kwa Sheria Ndogo kabla ya kuchambuliwa na kujadiliwa na Bunge unaruhususiwa katika mfumo wa udhibiti wa sheria ndogo usio wa moja kwa moja (*Indirect control*) ambao Tanzania unaoufuata na kuutumia.

### 1.4 Namna Kamati ilivyofanya Kazi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia ipasavyo masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanayoitaka Taarifa hii kubainisha njia na mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa jukumu la kuchambua sheria ndogo, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitumia njia na mbinu kuu zifuatazo:-

(i) Kufanya uchambuzi wa awali ili kubaini sheria zinazohitaji kufanyiwa uchambuzi wa kina na mambo yatakayopaswa kuzingatiwa wakati wa uchambuzi huo;

(ii) Kuwaalika wadau kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 139 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kupata uhalisia wa mazingira ya utekelezaji wake;

(iii) Kujadiliana na Mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika ili kupata muktadha wa utungaji na utekelezaji halisi; na

(iv) Kufanya uchambuzi kwa kuhusianisha, kulinganisha, kuoanisha, kufananisha na kutofautisha matokeo ya uchambuzi wa awali, maoni ya wadau na majadiliano kati ya Kamati na mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika.

**Mheshimiwa Spika**, njia na mbinu ya uchambuzi wa awali iliiwezesha Kamati kubaini sheria ndogo zenye dosari za aina tano zifuatazo:-

(i) kukiuka masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) kuwa kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo au sheria nyingine ya nchi;

(iii) kutozingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (*drafting principles*);

(iv) kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

(v) makosa ya uandishi katika Majedwali kwa mfano kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu vinavyoyaanzisha.

**Mheshimiwa Spika**, usikilizaji wa maoni ya wadau (*Public hearing*) uliiwezesha Kamati kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge. Mbinu hiyo imejengwa katika msingi kwamba sheria ndogo ndizo zinazofafanua utekelezaji wa Sheria iliyotungwa na Bunge, hivyo zinawagusa moja kwa moja wadau na jamii

nzima. Kwa sababu hiyo, bila ya kuwaalika wadau, isingelikuwa rahisi kujiridhisha ipasavyo na namna sheria ndogo inavyowezesha ustawi wa wananchi ambao ni lengo kuu la serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hatua hii naomba kukiri kuwa wadau waliofika mbele ya Kamati wametoa ushirikiano wenye tija na kufanikisha utekelezaji wa majukumu uchambuzi wa Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilikutana na kujadiliana mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizochambuliwa na Kamati. Majadiliano hayo yalilenga kupata ufafanuzi wa hoja zilizoibuliwa na Kamati. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa majadiliano na ushirikiano kutoka kwa mamlaka hizo yaliwezesha Kamati kufanya uchambuzi inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sehemu inayofuata ya taarifa hii italiwezesha Bunge kujadili inavyopaswa na hatimaye kufanya uamuzi wenye tija na manufaa kwa wananchi na maisha yao. Nitumie fursa hii kulisihi Bunge lako tukufu liendelee na msisitizo wake wa kuona sheria ndogo haziwi kero kwa wananchi wala kikwazo cha ustawi na maendeleo yao. Msisitizo huu unatokana na sheria ndogo kugusa moja kwa moja shughuli za watanzania walio wengi zikiwemo:-

(i) Kilimo cha mazao ya biashara na chakula;

(ii) Ufugaji na Uvuvi;

(iii) Biashara za mama lishe na baba lishe;na

(iv) Uchimbaji wa madini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli hizo kwa uhai na maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla, Bunge lina kila sababu ya kuwa na jicho kali katika sheria ndogo. Lengo ni kuondoa kero mbalimbali na hatimaye kuchochea maendeleo ya shughuli hizo kwa ustawi wa watu na taifa kwa ujumla.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA PAMOJA NA KANUNI ZA UVUVI ZA MWAKA 2009

### 2.1 Ufafanuzi kuhusu Sheria zilizochambuliwa

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 9 Aprili, 2021 na tarehe 7 Septemba, 2021, Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na nyongeza zake zikiwemo jumla ya **Sheria Ndogo Mia Nne Themanini na Saba (487)**. Mchanganuo wa sheria ndogo hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria Ndogo za Halmashauri *(By- Laws)* – **16**;

(ii) Kanuni za Wizara *(Regulations)* – **28**;

(iii) Amri *(Orders)* – **219**;

(iv) Matangazo *(Notices)* – **203**;

*(v) Rules* – **13;**

(vi) Matamko (Declaration) – **7**; na

(vii) Hati Rasmi (*Instruments*) – **1**.

### 2.2 Vigezo vilivyotumika katika uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo liliongozwa na masharti ya Kifungu cha 11(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kifungu hicho kinaitaka Kamati kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo zimekidhi na kuendana na maelekezo ya Katiba, Sheria Kuu ya Sheria Ndogo inayohusika pamoja na sheria nyingine za nchi. Katika kujiridhisha huko, wakati wa Uchambuzi Kamati ilitumia vigezo vitano kama ifuatavyo:-

(i) Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Kutokinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika;

(iii) Uzingatiaji wa misingi bora ya uandishi wa sheria (*drafting principles*);

(iv) Uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini ulivyotiliwa maanani; na

(v) Usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika. Mfano, kurejea kanuni kwa sahihi, kutorejea Kanuni ambazo hazipo, kurejea Kanuni inayohusika pamoja na maudhui ya Jedwali kuendana na vifungu vinavyoyaanzisha Jedwali.

## 2.3 Hatua za Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** hatua za uchambuzi wa sheria ndogo unaoripotiwa leo, ziliiwezesha Kamati kujikita katika kubaini kama sheria zilizotungwa zimetokana na madaraka ya Bunge na iwapo madaraka hayo hayakutumika tofauti. Mchakato ulianza kwa kuingiza uchapishwaji wa sheria ndogo kwenye Kumbukumbu za Bunge. Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, tarehe 9 Aprili, 2021 na tarehe 7 Septemba, 2021 , kupitia utaratibu wa hati za kuwasilisha mezani, sheria ndogo hizi zikiwa sehemu ya nyongeza ya matoleo ya gazeti la serikali ziliwasilishwa mezani, Bungeni. Baadaye sheria ndogo hizo zilipelekwa kwenye Kamati ya Sheria Ndogo ambapo uchambuzi wake ulianza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge kuwa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo yameisaidia Kamati kuja na taarifa hii itakayoliwezesha Bunge kuamua inavyostahili.

## 2.4 Matokeo ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanabainisha jumla ya dosari sabini (70) zinazoripotiwa katika taarifa hii. Kwa urahisi wa kufuatilia dosari hizo, Taarifa hii imeambatisha

Jedwali la Uchambuzi kwa rejea wakati wa mjadala na uamuzi. Naomba Jedwali hilo liingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge na hasa kuhusu kuweka mtiririko mzuri wa mchakato wa udhibiti wa Sheria Ndogo zilizochambuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, mchanganuo wa dosari hizo unaonesha kuwa:

(i) Sheria Ndogo moja (1) imebainika kuwa na dosari ya kutozingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Jumla ya sheria ndogo Sita (6) zimebainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika na sheria nyingine za nchi;

(iii) Sheria ndogo kumi na nane (18) zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi bora ya uandishi wa sheria (*drafting principles*)

(iv) Sheria Ndogo Nane (8) zimebainika kuwa na dosari za kuweka masharti yasiyo na uhalisia hivyo, kutokuwa na urahisi wa utekelezaji wake; na

(v) Jumla ya sheria ndogo Tisa (9) zimekutwa na dosari ya uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika jambo linaloathiri utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo baadhi ya Sheria Ndogo zinajumuishwa katika aina zaidi ya moja ya dosari. Kwasababu hiyo jumla ya idadi ya Sheria Ndogo inaweza isifikiwe kwa kujumlisha idadi katika mchanganuo huo.

### 2.4.1 Dosari ya kutozingatia masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika**, nchini Tanzania, Katiba ina ukuu wa sheria za nchi na kazi zake kuu na za msingi ni pamoja na kugawa madaraka kati ya dola na jamii pamoja na mgawanyo wa

madaraka miongoni mwa mihimili ya serikali. Kwa sabbu hiyo, sheria zote za nchi ni zao la mgawanyo wa madaraka uliowekwa na Katiba. Kutokana na ukuu wa Katiba, Bunge haliwezi na haliruhusiwi kutunga sheria au kuweka masharti ya sheria yanayokinzana na Katiba. Hali kadhalika, Bunge halina uwezo wa kuruhusu mamlaka nyingine kutunga sheria ndogo yenye masharti yanayokiuka masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo ubnaoripotiwa leo, yanadhihirisha sheria ndogo moja (1) yenye dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba. Sheria hiyo ni **Sheria Ndogo za Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 2021 (GN. NA. 287/19 Machi, 2021)** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura 287)**.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 2** kinatafsiri neno "**ombaomba**" kuwa ni mtu yeyote, mwenye ulemavu au asiye na ulemavu anayeishi kwa kutegemea kuombaomba chakula au fedha au vitu vingine kutoka kwa mtu mwingine kwenye Mitaa na maeneo ya wazi yaliyoko ndani ya eneo la Halmashauri. Tafsiri inaainisha watu katika makundi kulingana na ulemavu au kutokuwa na ulemavu. Tafsiri hii inaweza kutoa mtazamo wa kibaguzi kwa kundi la watu wenye ulemavu kuonekana ni watu wenye hadhi ya ombaomba jambo ambalo si halisia.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 12 (1) na (2) ya Katiba inasomeka:
"*Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.*"
*"Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake."*

**Mheshimiwa Spika**, aidha, **Ibara ya 13(2)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia imeweka marufuku kuweka aina yoyote ya ubaguzi katika sheria yeyote. Ibara hiyo inasomeka kama ifuatavyo:
*"Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake."*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa shauku hiyo, Bunge lako tukufu halitarajiwi kupuuza matumizi ya kifungu cha sheria ndogo kinachoonesha hali ya kubagua kundi la watu wenye ulemavu kwasababu jambo ambalo limekatazwa kwenye Katiba.

### 2.4.2 Kukinzana na masharti ya Mama na sheria nyingine za nchi

**Mheshimiwa Spika**, Bunge linaporuhusu mamlaka inayohusika kutunga sheria ndogo, hufanya hivyo kwa madhumuni maalumu yanayoendana na lengo kuu la Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Kwa sababu hiyo, sheria ndogo yoyote inayotungwa inapaswa kuendana pia na masharti yaliowekwa na Sheria nyingine za nchi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya sheria zilizochambuliwa zilikuwa na maudhui yanayotofautiana na masharti ya Sheria Mama au Sheria Nyingine za Nchi. Jumla ya sheria ndogo Sita (6) zilibainika kuwa na dosari ya kukinzana Mama na Sheria nyingine za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa sheria ndogo hizo ni *The Environmental Management (Registration and Practice of Environmental Experts) Regulations, 2021 (GN. NA. 267/19, Machi 2021) ambazo zimetungwa* chini Sheria ya *The Environmental Management Act,* (Sura 191). Uchambuzi umebainisha kuwa, **Kanuni ya 32(1)** imeweka masharti yanayostahili, yanayomkataza mtumishi wa umma aliyesajiliwa kama mtaalamu wa mazingira kufanya tathmini ya mazingira katika miradi iliyo chini ya taasisi yake ili kuepuka mgongano wa maslahi. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini, katazo lililowekwa na **Kanuni ya 32(1),** linaondolewa na **Kanuni ya 32 (2)** ambayo inamruhusu Ofisa wa umma aliyesajiliwa kama mwanataluuma wa mazingira kufanya shughuli za tathmini za mazingira zinazohusu taasisi yake. Ruhusu hii inaondoa mantiki ya katazo lililowekwa katika Kanuni ya 32(1) kuhusu mgongano wa maslahi

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu unaowekwa na **Kanuni ya 32(2)** ni kinyume na misingi ya kudhibiti mgongano wa maslahi kwa mujibu wa ya Kanuni za Maadili ya Watumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa Bunge lako tukufu litaruhusu utaratibu unaowekwa na Kanuni hiyo, basi litakuwa linabariki uvunjaji wa misingi ya mgongano wa maslahi hali ambayo inaweza kuathiri uwajibikaji kwa maafisa wa serikali walioshiriki katika kufanya tathmini ya athari za mazingira kwa miradi inayotokana na taasisi zao.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile dosari ya kukinzana na matakwa ya sheria nyingine za nchi imebainika katika Kanuni za ***The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2021 (GN. NA. 389/14, Mei 2021)*** ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Mazingira (***The Environmental Management Act***). **Kanuni ya 2** imetafsiri maneno "***hazardous substance"*** kwa kuongeza maneno "***liquid"*** na ***"solid"*** ambayo hayamo katika tafsiri iliyotolewa na **Kifungu cha 3** cha sheria mama. Aidha Kanuni hiyo imetumia neno ***gaseous*** badala ya neno ***gas*** lililotumika katika sheria mama.

**Mheshimiwa Spika**, matumizi ya tofauti maneno na ilivyotafsiriwa katika sheria iliyotungwa na Bunge yanaweza kufifisha kusudio la sheria mama. Aidha, uandishi wa namna hii ni kinyume na masharti kifungu cha 39 cha Sheria ya Tafsiri kinachotaka kuwa maneno yanayotumika katika sheria ndogo kuwa na maana sawa na maneno yaliyotumika katika sheria mama.

### 2.4.3 Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazotungwa na Bunge huzingatia misingi bora ya uandishi wa sheria. Hivyo, kipimo cha kuangalia uandishi bora wa sheria kilizingatiwa wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo. Matokeo ya uchambuzi yameonesha jumla ya Sheria Ndogo kumi na nane (18) zina dosari kuhusu misingi ya uandishi wa sheria. Mfano ni katika **Sheria Ndogo Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri**

**ya Wilaya ya Bumbuli, 2021 (GN. NA. 275/19 Machi, 2021)** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290).**

**Mheshimiwa Spika,** dosari ya uandishi katika sheria ndogo hizo inahusu **kipengele cha 12** cha **Jedwali la 6** kinachoorodhesha aina ya vitu vinavyopaswa kutozwa ushuru. Idadi ya aina za vitu inatofautina na idadi ya viwango vya ushuru. Idadi ya aina za vitu vinavyopaswa kutozwa ushuru ni saba (7) lakini viwango vya ushuru vilivyoainishwa kwa vitu hivyo ni vinane (8).

**Mheshimiwa Spika**, tofauti hiyo inakanganya tafsiri ya sheria ndogo hiyo katika matumizi kwakuwa tofauti hiyo inaweza kuwa imesababishwa na kusahaulika kwa kitu kinachotozwa ushuru au kuongezeka kwa viwango vya ushuru visivyotakiwa.

**Mheshimiwa Spika**, uandishi huo unaweza kuathiri chanzo cha mapato ya Halmashauri kinyume na kusudio la sheria hii. Vilevile inaweza kusababisha utozaji usiotabirika unaotokana na kukosekana kwa muongozo dhahiri. Hali hiyo inaweza kuzaa kero kwa wananchi wa Bumbuli iwapo haitarekebishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna yoyote ile Bunge lako tukufu halipaswi na kamwe haliwezi kuona mazalio ya kero kwa wananchi wa Bumbuli au kwingineko nchini pasipo kuchukua hatua muhimu kuondoa kero hizo.

### 2.4.4 Kukosa Uhalisia

**Mheshimiwa Spika**, Utungaji bora wa Sheria pamoja na mambo mengine hujielekeza pia katika kupima uhalisia wakati utekelezaji, ikiwemo hali halisi na mazingira ya watumiaji na walengwa wa sheria inayohusika. Kamati imebaini jumla ya sheria ndogo nane (8) zina vifungu visivyo na uhalisia katika utekelezaji wake. Mfano wa Sheria Ndogo zenye vifungu vya aina hiyo ni **Kanuni za Uvuvi, 2009** zilizotungwa chini ya **(Sheria ya Uvuvi, 2003).**

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 13 (22)** ya Kanuni hizo, inaweka masharti kwa mtu anayetaka kuomba kuuza nje ya nchi au kuingiza bidhaa za samaki zitokanazo na uvuvi kujaza fomu ya maombi itakayokuwa na viambatisho vilivyotajwa katika kanuni hiyo. Viambatisho hivyo ni:

(i) Cheti cha Usajili (*Certificate of registration*);

(ii) Kidokezo cha Msajili kuhusu ufafanuzi wa Kampuni (*Extract from Registrar*);

(iii) Cheti cha Ukamilifu wa Kampuni *(Certificate of Incorporation)*;

(iv) Katiba na Hati ya Kanuni za Kampuni (*Memorandum and Articles of Associations)*;

(v) Uthibitisho wa Uraia (*Proof of Citizenship*);

(vi) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (*Tax Identification Number (TIN)*); na

(vii) Cheti cha Uthibitisho wa Kutodaiwa Kodi (*Tax Clearance Certificate*).

**Mheshimiwa Spika**, masharti ya kuwasilisha nyaraka zilizotajwa yanakosa uhalisia katika utekelezaji wake kwa waombaji ambao si wamiliki wa kampuni. Kwa hali ya kawaida, mtu ambaye si Kampuni hawezi kuwa na viambatisho vitatu kati ya vilivyotajwa. Viambatisho hivyo ni Cheti cha Ukamilifu wa Kampuni *(Certificate of Incorporation)* na Katiba na Hati ya Kanuni za Kampuni (*Memorandum and Articles of Associations)* ambavyo ni mahsusi kwa kampuni na si mtu binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kwamba, sharti la kumtaka mtu binafsi kuwasilisha nyaraka hizo linakwamisha ushiriki wa watu binafsi katika shughuli za usafirishaji wa samaki na mazao ya samaki nje ya nchi kutokana na kutokuweza kukidhi masharti hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge linapotunga Sheria na kuruhusu mamlaka nyingine itunge sheria ndogo, linatarajia mamlaka inayohusika itafanya hivyo kwa namna yenye maana kwa jamii. Kamwe, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi haliwezi kuachia mamlaka zilizoruhusiwa na sheria ya Bunge zitunge sheria ndogo zisizoakisi shabaha na madhumuni ya sheria mama.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine wa sheria ndogo zilizobainika kuwa na vifungu visivyo na uhalisia ni Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, 2021 **(GN. NA. 275/19 Machi, 2021)** ambazo pia zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290).**

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9(8)** kinaweka wajibu kwa **mnunuzi yeyote** kutoa taarifa sahihi ya mazao aliyonunua na kuonesha risiti aliyolipia ushuru pamoja na kibali cha kununulia mazao kwa Afisa Mwidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo. Maneno "**Mnunuzi yeyote**" yanayotumika katika Kifungu cha 9(8) hayajatafsiriwa kuonesha ni mnunuzi wa kiwango gani cha mazao anayeguswa.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo maneno **"mnunuzi yeyote"** yatatafsiriwa kama yalivyo katika sheria ndogo hizi, yanaweza kusababisha kero kubwa kwa wananchi. Kero hiyo inaweza kuwa kubwa kwa wananchi wanaonunua mazao kwa matumizi ya nyumbani, kwa kulazimika kuonesha risiti za ununuzi wa mazao.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge haliwezi kutunga sheria isiyoendana na busara ya kawaida. Aidha, Bunge haliwezi kutunga sheria inayokasimu utungaji wa kanuni kwa kiwango cha kukinzana au kukosa uhalisia katika utekelezaji wake. Hivyo haliwezi kuruhusu mamlaka iliyoruhusiwa kutunga Sheria Ndogo ifanye hivyo kwa kukinzana na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,** mfano mwingine wa sheria ndogo zilizobainika kuwa na vifungu visivyo na uhalisia ni Kanuni zizazoitwa ***The Wildlife Conservation (Wildlife and Forest***

***Conservation Service) Regulations, 2021*** **(GN. NA. 589/9 Julai, 2021)** ambazo zimetungwa chini ya ***The Wildlife Conservation Act***.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa **Kanuni ya 24** inaweka masharti ambayo utekelezaji wake unaweza kuwa na changamoto. Kanuni hiyo inaweka sharti linalomkataza mtu anayetekeleza majukumu yaliyo chini ya Kanuni hizi asijihusishe na ajira nyingine ya aina yeyote ambayo inamuingizia kipato.

**Mheshimiwa Spika,** masharti yaliyowekwa na Kanuni hiyo hayaoneshi mantiki ya zuio hilo au mgogano unaoweza kusababishwa na askari muhifadhi kuwa katika ajira nyingine inayomuingizia kipato. Kwa msingi huo, masharti hayo yanazuia pia mhusika kuwa katika ajira binafsi ambazo hazihusiani majukumu ambayo yanasimamiwa na Kanuni hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge haliwezi kuona sheria ndogo zinaweka masharti ambayo hayaendani na lengo la sheria iliyotungwa na Bunge ambayo kimsingi imelenga kulinda maliasili za nchi na si kuathiri maisha binafsi ya wahusika wanaotekeleza sheria za uhifadhi wa maliasili nchini.

### 2.4.5 Makosa ya Uandishi wa Majedwali ya Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika,** uandishi fasaha wa majedwali husaidia kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina wa kifungu au kanuni inayohusika. Majedwali katika sheria au sheria ndogo yatakuwa na maana iwapo yatawekwa kwa namna inayorejea kwa usahihi kifungu au kanuni wezeshi (*enabling provision*). Inapotokea Majedwali ya sheria yana dosari ya kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni au Maudhui ya Jedwali kutofautiana na kifungu wezeshi au vifungu vingine vya sheria au sheria ndogo inayohusika, inaathiri mantiki, madhumuni na maudhui ya jumla ya sheria.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Kamati yameonesha kuwa jumla ya sheria ndogo tisa (9) zimekuwa

na dosari kuhusu uandishi wa majedwali. Mfano wa dosari hizo unaonekana katika sheria ndogo ya ***The Civil Aviation (Training Centre) and Management and Operations, Rules (GN. NA. 179/5 Februari, 2021)*** iliyotungwa chini **Sheria ya *The Civil Aviation Act*, (Sura 80).** Jedwali la Kanuni hizi linaoneshwa kuwa limeanzishwa chini ya **Kanuni ya 9(3)** ambayo haipo. Kosa hilo la uandishi linaning'iniza Jedwali katika mtiririko wa uandishi na kuharibu azma ya ufafanuzi uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinatambua Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria inayohusika na wakati mwingine kusababisha mkanganyiko.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa pili wa dosari za uandishi wa majedwali unadhihirika katika **Kanuni za Uvuvi, 2009** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Uvuvi, 2009. Fomu Na. 13 (a)** katika **Jedwali la Kwanza** inayohusu maombi ya kuharibu mazao ya uvuvi yaliyokamatwa, imekosea rejea kwa kutaja kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 50(4),** hata hivyo maudhui ya kanuni hiyo yanahusu fomu ya kufifilisha kosa (*compounding of offence*) na utekelezaji wa masharti (*Compliance Form*).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Majedwali katika sheria hulenga kutoa ufafanuzi zaidi wa maudhui yaliyo katika vifungu, kutokuandika majedwali kwa ufasaha kunasababisha mkanganyiko katika sheria na hivyo kuathiri malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili tukufu halitakuwa tayari kuruhusu mamlaka zinazokabidhiwa uwezo wa kutunga sheria ndogo, zitumie uwezo huo kwa namna isiyowezesha lengo na madhumuni ya sheria mama. Kwa msingi huo, Bunge halitaacha kuzisisitiza mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga kanuni au sheria ndogo nyingine kuzingatia uandishi bora wa Majedwali katika sheria.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI

### 3.1 Maelezo

**Mheshimiwa Spika,** maelezo niliyoyatoa katika sehemu za taarifa zilizotangulia, yanadhihirisha kuwa sheria ndogo hutungwa mara kwa mara kulingana na mahitaji yanayojitokeza. Hali hiyo inaonesha umuhimu wa utaratibu madhubuti wa kuhifadhi na kulinda heshima ya mamlaka ya kutunga sheria nchini. Bunge ambalo ni chombo kikuu cha utungaji wa sheria linaendelea kuwa na wajibu wa kuangalia utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Bunge hufanya kazi kwa kutumia Kamati zake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo yenye jukumu la kuchambua sheria ndogo, imetekeleza majukumu yake na kuonesha matokeo ya uchambuzi kama ilivyofafanuliwa. Katika sehemu hii, naomba kubainisha mtazamo wa jumla wa Kamati kuhusu aina tano za dosari zilizobainishwa katika Taarifa hii kwa namna ya maoni ya Kamati yanayotokana na uchambuzi.

### 3.2. Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya uchambuzi, Kamati inabainisha maoni katika maeneo makuu matano kama ifuatavyo:-

#### 3.2.1 Kutozingatiwa kwa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

**Mheshimiwa Spika**, kutozingatiwa kwa misingi inayowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uandishi wa sheria ndogo ni jambo linaloweza kusababisha mifumo, taasisi na mwelekeo wa jamii kutoendana na misingi ya Katiba. Hali hiyo, ni kinyume na masharti ya Katiba ambayo ndilo chimbuko la sheria zote za nchi. Ikiwa hivyo, inaweza kusababisha, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ukiukwaji

wa upatikanaji wa haki mbalimbali zikiwemo haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

### 3.2.2 Kukinzana na masharti ya sheria mama

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya sheria ndogo kukinzana na sheria mama inaathiri tija ya utekelezaji wa Sheria. Dosari hiyo ikiendelea, masharti yaliyowekwa kwenye sheria mama kwa lengo la kuiwezesha mamlaka inayohusika kutunga sheria ndogo yatakosa maana. Hali hiyo ni kinyume na misingi ya utungaji wa sheria na Bunge haliwezi kupuuza au kuruhusu kupuuza misingi hiyo.

### 3.2.3 Kutozingatiwa kwa Misingi ya Uandishi bora wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa sheria zote kuendana na misingi ya uandishi bora wa sheria, dosari za sheria ndogo kutoendana na utaratibu bora wa uandishi wa sheria, si jambo la kuachwa katika sheria ndogo. Dosari hizo zinaweza kuashiria utekelezaji wa sheria mama usio na tija. Bunge halipaswi kuruhusu dosari za aina hiyo ziendelee kuwepo katika sheria ndogo.

### 3.2.4 Sheria ndogo kukosa uhalisia

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ndogo zinapokuwa na maudhui yasiyozingatia hali ya uchumi wa walengwa au urahisi wa utekelezaji wake, inakosa uhalisia. Ni ukweli kuwa sheria yoyote isipotungwa kwa kuzingatia uhalisia wa mambo inaweza kutatiza utekelezaji wake. Bunge linapaswa kujiridhisha na kuhakikisha kuwa, dosari za sheria ndogo za kutoendana na uhalisia zinarekebishwa.

### 3.2.5 Kukosekana kwa Usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika

**Mheshimiwa Spika**, matumizi ya majedwali katika uandishi wa sheria ndogo ni jambo la kuzingatiwa katika uchambuzi wa sheria. Dosari ya kukosekana kwa usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika

inaweza kusababisha mkanganyiko wa maudhui ya sheria inayohusika. Bunge linapaswa kusisitiza usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ili kuwezesha ukamilifu wa sheria.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HOJA NA MAPENDEKEZO

### 4.1 Maelezo

**Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie maelezo ya jumla niliyoyatoa, ufafanuzi wa matokeo ya uchambuzi na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Hoja hii inahusu eneo muhimu la utekelezaji wa sheria ambalo lisipoangaliwa kwa umakini linaweza kuwa mazalia ya kero, bughudha na manung'uniko katika jamii.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** sasa naomba kutoa hoja ili Bunge lako liazimie kama ifuatavyo:-

#### 4.2.1 Kutozingatiwa kwa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

**KWA KUWA**, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na masharti yanayokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo lisiloweza kukubaliwa na Bunge,

**NA KWA KUWA**, Kutofanya marekebisho katika sheria ndogo hizo kunaweza kusababisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, kukosekana kwa haki mbalimbali zikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayokinzana na masharti ya Katiba, ifanye marekebisho inavyostahili.

### 4.2.2 Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo au sheria nyingine za nchi.

**KWA KUWA,** baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria mama inayohusika,

**NA KWA KUWA,** sheria ndogo inayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, haiendani na masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria, hali inayoisababisha kuwa batili kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zirekebishe sheria ndogo hizo.

### 4.2.3 Kutozingatia Misingi ya Uandishi Bora wa Sheria

**KWA KUWA,** uchambuzi umebainisha sheria ndogo ambazo hazikuzingatia misingi ya uandishi bora wa sheria,

**NA KWA KUWA,** kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi kunasababisha tatizo la sheria kutoeleweka kwa urahisi na kutotabirika, hali inayoathiri tija ya utungaji wa sheria,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo hizo zifanye marekebisho.

### 4.2.4 Dosari ya Uandishi wa Majedwali

**KWA KUWA**, imebainika baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari katika uandishi wa majedwali, ilihali Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinatambua majedwali kuwa sehemu ya Sheria,

**NA KWA KUWA,** dosari hizo zinaathiri ukamilifu na kutatiza utekelezaji sheria inayohusika,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho.

#### 4.2.3 Masharti yasiyo na uhalisia

**KWA KUWA,** zipo baadhi ya sheria ndogo zenye masharti yanayokinzana na uhalisia,

**NA KWA KUWA**, masharti hayo yanaweza kuathiri utekelezaji na tija iliyokusudiwa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizopewa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari za kutoendana na uhalisia zifanye marekebisho.

**MWISHO**

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa sheria ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (Sheria Ndogo) kwa wakati, pia uratibu mzuri wa uwasilishaji wa Jedwali la Uchambuzi kwa Wizara husika ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari. Hali hii kwa muda

wote imekuwa ikiiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza katika sheria ndogo. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

**5.1.1 Mawaziri**

1. Mhe. Mashimba Ndaki – **Waziri wa Mifugo na Uvuvi;** na

2. Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) – **Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI)**.

**5.1.2 Naibu Mawaziri**

1. Mhe. David Silinde (Mb) – **Naibu Waziri - Ofisi ya Rais TAMISEMI**;

2. Mhe. Hamad Hassan Chande, (Mb) – **Naibu Waziri - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**;

3. Mhe. Abdallah Ulega, (Mb) – **Naibu Waziri - Mifugo na Uvuvi**;

4. Mhe. Patrobas Katambi, (Mb) **– Naibu Waziri - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira;**

5. Mhe. Stephen Byabato, (Mb) – **Naibu Waziri - Wizara ya Nishati;**

6. Mhe. Eng. Kundo Andrea Mathew, (Mb) – **Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;**

7. Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, (Mb) – **Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto**;

8. Mhe. Mary Francis Masanja, (Mb) – **Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii**

### 5.1.3 Wadau

**Mheshimiwa Spika**, aidha niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati mnamo tarehe 11 hadi 12 Agosti, 2021 na tarehe 13 na 15 Oktoba, 2021 kwa ajili na kutoa maoni katika sheria ndogo tano zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati. Maoni yao kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina katika Kanuni hizo. Naomba kipekee niwatambue wadau kama ifuatavyo;

1. Chama cha Wafamasia Tanzania (*The Pharmaceutical Society of Tanzania*);
2. Chama cha Wataalamu wa Mazingira Tanzania **((*Tanzania Environmental Experts Association*)(TEEA))**;
3. Chama cha Wavuvi Tanzania **(*Tanzania Fisheries Union*)(TAFU))**;
4. Chama cha Wavuvi Wadogo wadogo, Minazi Mikinda **(CHAWAWAMI)**; na

5. Chama cha Ushirika wa Wavuvi Mwalo wa Kigodeko ***(Kigodeko Fisheries Cooperative)***.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge, Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi, 2009 na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*):-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – **Mwenyekiti;**
2. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, (Mb) – **M/Mwenyekiti**;
3. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb);
4. Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, (Mb);
5. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb);
6. Mhe. Sylvia Francis Sigula, (Mb);
7. Mhe. Emmanuel Mageni Kasalali, (Mb);
8. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, (Mb);
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, (Mb);

10. Mhe. Judith Salvio Kapinga, (Mb);
11. Mhe. Santiel Erick Kirumba, (Mb);
12. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb);
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, (Mb);
14. Mhe. Esther Edwin Malleko, (Mb);
15. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb);
16. Mhe. Esther Lukago Midimu, (Mb);
17. Mhe. Minza Simon Mjika, (Mb);
18. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb);
19. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb);
20. Mhe. Nicholaus George Ngassa, (Mb);
21. Mhe. Humphrey Hesron Polepole, (Mb);
22. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, (Mb);
23. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, (Mb); na
24. Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, (Mb).

**Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndg. Mkuta Masoli na Ndg. Stanslaus Kagisa, wakisaidiwa na Bi. Imelda Ntimba Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 5.2 Kutoa hoja

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**
10 Novemba, 2021

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Jasson Rweikiza kwa taarifa hiyo. Sasa tuanze moja kwa moja na mjadala wa jumla na nitaanza na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na baadaye Mheshimiwa Edwin Swalle na Mheshimiwa Simaye Hassan Sadiki wajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami ningependa sana kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika mjadala huu wa Sheria Ndogo juu ya mabadiliko au mapungufu ambayo tumeyaona katika uchambuzi tulioufanya ndani ya Kamati yetu. Leo sitakuwa na mengi sana ya kusema isipokuwa ni kukumbushana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya msingi ambayo yamekuwa mara kwa mara tunapoleta taarifa zetu hapa yamekuwa yanatokea. Jambo la kwanza ambalo kwangu mimi ninaona ni la kwanza kwa umuhimu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo nyingi zinazoandikwa zimeendelea kuwa sheria zinazokinzana na hali halisi kwa maana ya utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano, ipo sheria ambayo ndani ya taarifa yetu inaonekana inahusu Sheria ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria ile yameelezwa masharti ambayo mvuvi au mfanyabiashara wa samaki anatakiwa kuyatimiza ili aweze kupata vibali kwa ajili ya kufanya biashara hiyo, lakini kwangu mimi na wenzangu ndani ya uchambuzi wetu tumelitazama jambo hili katika upanda wake hasa katika lile hitaji la kumfanya huyu anayeomba kibali kwa ajili ya kufanya biashara hiyo aweze kuwa na vitambulisho muhimu ikiwemo kile cheti

kinachoonesha uthibitisho wa yeye kuwa amezaliwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria zetu za nchi sasa hivi ni wazi zimeweka kwamba mwananchi ili aweze kuthibitishwa mojawapo lazima awe na kitambulisho cha uraia, lakini bado sheria hii inataka kuangalia zaidi ya kile kitambulisho chake cha uraia, kwa maana ya kuthibitisha kama ambavyo wenzetu nchi nyingine wanafanya, tukitolea mfano kwa mfano Japan kule ambapo mtoto au mimba tu inapotungwa tayari mzazi anapewa kitabu na kijiji kinamsajili kwa maana ya kwamba sasa kuna kiumbe kipya tunamtarajia katika maeneo hayo. Sheria ambayo katika Tanzania haipo na wala haizungumzwi hivyo, masharti yenyewe yalivyowekwa ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande mwingine imeelezwa hapa sheria hii inamnyima haki yule mvuvi wa kawaida aliopo pale Kigoma aweze kufanya biashara hii. Kwa sababu inamtaka mvuvi huyo aweze kufungua kampuni, lakini kwa kufungua kampuni maana yake pia anatakiwa awe na *tin number*. Sasa Bunge lako linajua hali za wavuvi wetu, lakini pia ni moto wa Serikali yetu kuona jinsi gani inawasaidia wale wanyonge wa Tanzania ili waweze kujikomboa katika hali ya umaskini walionayo. Sasa leo hii mtu mwenye mifuko yake miwili ya samaki naye pia anatakiwa awe na hivyo vibali jambo ambalo kwa kweli kama kamati tuliona haliendani na hali halisi ya maeneo yetu haya ambayo tunaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu pia lipo jambo la sheria zetu hizi kusahau msingi wa uandishi au utungaji wa sheria zetu yaani *drafting principles.* Mara kwa mara tunaposimama Bungeni hapa tunaendelea kukumbusha Serikali, wakati mwingine sheria hizi si jambo la dharura ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maana ya kwamba wanatakiwa wakae chini, watunge sheria wakiwa wametulia, wakague katika *principles* kama zimetimia, lakini kila siku zinapokuja sheria kumekuwa na mapungufu hayo kwa hiyo kwangu la msingi zaidi narudi tena kuikumbusha Serikali,

utaratibu wetu ulivyo upo wazi, sheria hizi wanaanza wao wenyewe katika Ofisi za *Attorney General* huko kuzitengeneza siamini kwamba sheria hizi labda zinaandikwa na mtu mmoja na kwamba zinafika hapa iwe sisi kazi yetu badala ya kusimamia maendeleo ya nchi iwe kazi yetu kuangalia na kugundua makosa yakiwemo yale ambayo yanatakiwa ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu yawe yanaangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia yapo matatizo mengine ambayo sheria hizi zinakosewa sana na katika jambo kubwa ambalo kwa wanasheria tunasema hizi ni *fundamental error* katika uandishi au tafsiri ya sheria ya kukosea kuweka vifungu vinavyohusika au vifungu halisi katika sheria. Kwa mfano, yapo baadhi ya majedwali yanaonekana katika uandishi huu, mtu kwa mfano jedwali la kwanza la sheria linanukuu kipengele au kanuni ya tatu ya sheria wakati Kanuni halisi ya jedwali hilo labda ni kanuni ya nne. Kwa hiyo imekuwa mara kwa mara jambo hilo linatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria kwa mfano nikizungumzia kwa sheria hii ya samaki maana yake kwa yeye ambaye anataka kwenda kutafuta hivyo vibali maana yake akienda akitumia sheria hii ni wazi anakuwa yuko nje ya utaratibu na anaweza akajikuta sheria yenyewe pia haiwezi kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo mwisho kwa umuhimu naomba niikumbushe tena Serikali lakini hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuendelea kukumbuka kwamba nchi hii katika sheria zake zinaanzia kwenye Katiba ambayo ndiyo Sheria Mama na ndiyo mwongozo wake, lakini siyo Katiba peke yake, lakini pia kwa Sheria Ndogo zinaanzia kwenye Sheria Mama ambayo inampa mamlaka yule ambaye anakwenda kutunga Sheria Ndogo hizi, lakini mara nyingi sana kumetokea matatizo ya kwamba waandishi wetu wanasahau kwenye uandishi mamlaka hayo au kutambua mamlaka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu kutambua mamlaka pia tumeona katika baadhi ya sheria, zikiwemo sheria zile zinazozungumzia masuala ya mazingira kwamba unakwenda unakuta sheria ambayo inapewa *references* haifanani kabisa na sheria ambayo imeletwa mbele yetu kama Kamati yako ya Sheria ya Bunge. Kwa hiyo, kwangu nilianza kusema kwamba leo nasimama kuendelea kuikumbusha Serikali yapo mambo ya msingi ambayo ni lazima yaendelee kuangaliwa katika utunzi wa Sheria Ndogo hizi na katika mambo hayo ya msingi zaidi ni kuendelea kukumbuka wapi mamlaka imetolewa, lakini pia zile *principles* za *drafting* za sheria zetu pia kuangalia kwamba sheria zenyewe zinaendana na hali halisi ya maisha ya Watanzania ambao wanakwenda kuathirika kwa namna moja au nyingine na sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja ya Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Swalle, baadae Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan wajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuwa mchangiaji wa pili kwenye taarifa hii ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono taarifa nzuri ya Kamati ya Sheria Ndogo na niipongeze sana Kamati kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya uchambuzi wa Sheria 487.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili pia nimshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kuipa muda wa kutosha Kamati ya Sheria Ndogo na hii inaashiria kwamba Ofisi ya Mheshimiwa Spika inatambua na kujali madhara ya Sheria Ndogo ambazo ndiyo zinatumiwa kwenye shughuli za kila

siku za wananchi wetu wa Tanzania. Wakiwemo wale wavuvi na watu wa chini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea kwenye taarifa ya Kamati kama ambavyo imesomwa na Mwenyekiti wa Kamati, ukitazama kwa ujumla unaweza ukapata picha kwamba katika uchambuzi ambao Kamati imefanya kumekuwa na kosa ambalo mara nyingi linafanywa na mamlaka za utunzi wa hizi Kanuni au Sheria Ndogo. Hii inapelekea kwamba mtazamo wa utunzi wa Kanuni hizi wakati fulani unaangalia kuwa na lengo la kukataza, lengo la kuzuia, lengo la kutoa adhabu na lengo la kukataza watu wasifanye shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana miongoni mwa Kanuni ambazo zimebainika kuwa na dosari ni Kanuni ya Wanyamapori na Uhifadhi kwenye Kifungu cha 24. Kanuni hii ambayo inahusu ajira za Wahifadhi Wanyamapori ilikuwa inataka mtu akiajiriwa kwenye Uhifadhi wa Wanyamapori asifanye shughuli nyingine yeyote ya kumuingizia kipato chake halali. Kanuni hii kama ingeachwa kama ilivyo tafsiri yake ni kwamba mtu anayefanya kazi ya ulinzi kwenye hifadhi hataweza kufanya hata shughuli zingine za kumuingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati inakuwa je, kama asifanye shughuli yoyote ya kumuingizia kipato ina maana kwamba haruhusiwi kuwa na duka lake binafsi, ina maana kwamba haruhusiwi kuwa na shamba lake binafsi. Kwa hiyo, Kanuni hii ilikuwa haitoi taswira sawa sawa kwamba asifanye shughuli nyingine binafsi maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Kamati imeona hii dosari kwamba kwa mujibu wa Katiba yetu ukisoma kuanzia Ibara ya 12 hadi ya 30 ni wazi kwamba Watanzania wanayo haki ya kufanya kazi na wana haki ya kupata ujira. Kwa hiyo, ni maoni ya Kamati kwamba Kanuni hii ilikuwa na dosari hiyo kwa hiyo pamoja na kuzuia shughuli maalum ya ulinzi, lakini Mlinzi ana haki ya kufanya shughuli zingine za kumuingizia kipato kama raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine kwenye Kanuni ya Misitu inayohusu uzalishaji, usafirishaji na uuzaji wa mkaa mbadala. Waheshimiwa Wabunge wote mnajua dunia sasa hivi inatazama uhifadhi wa mazingira na siku za karibuni Mheshimiwa Rais alikuwa kwenye mkutano mkubwa duniani unaozungumza kuhifadhi mazingira, maana yake ni kwamba kuelekea kwenye kanuni za kutengeneza mkaa mbadala ni kitu muhimu cha kuhimiza wananchi wetu watengeneze mkaa mbadala badala ya kuharibu maliasili ya misitu kwa maana mkaa wa asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kanuni hii ya Tisa ukitazama kwenye maudhui yake inatoa katazo au inatoa mamlaka kwa Mhifadhi wa Misitu kwamba anaweza kusitisha leseni ya mtu anayefanya kazi ya uzalishaji wa mkaa mbadala au usafirishaji au uuzaji na haitoi akisitisha hicho kibali, atasitisha kwa muda gani na haielezi atarudishiwa kwa namna gani akikidhi masharti ya kibali husika. Kwa hiyo, hii pia ilikuwa ni dosari kubwa tunadhani ni wakati sasa Kanuni zetu nyingi ziwe ni Kanuni za kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za maendeleo badala ya kukataza na kutoa adhabu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho na la muhimu napenda pia kuishauri Serikali kwamba inapoendelea kutunga hizi Kanuni na Sheria Ndogo ndogo tuwe na mtazamo zaidi wa kutunga Sheria na Kanuni za kuwezesha shughuli za wananchi kuendelea badala ya kuwa na sheria ambazo kazi yake kubwa ni kukataza, kuzuia na kutoa adhabu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba hata Mawaziri walipokuja kwenye Kamati ya Sheria Ndogo wakati wote ilipobainika dosari ya kufanyia marekebisho walikuwa tayari na kutoa ushirikiano mkubwa sana kwa ajili ya ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsate sana Mheshimiwa Edwin Swalle tunaendelea na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki baadaye atafuata Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan na baadaye Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda na Mheshimiwa Aida Khenani wajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa fursa ya kuchangia jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zimetungwa kwa ajili ya ku-*regulate human conduct* sasa kwa kawaida sheria yeyote inakuwa inaongoza matendo halisi ya mwanadamu, sheria nazo katika utungwaji wake zimekuwa zimekuwa zimewekewa misingi maalum itakayoongozwa katika uandishi wake au maandalizi yake. Sheria Ndogo inapokuwa inaenda kinyume na utaratibu wa Katiba, sheria inapokuwa inaenda kinyume na utaratibu wa Sheria Mama maana yake sheria hiyo inakosa uhalisia katika matumizi yake. Sheria inapokosa uhalisia katika matumizi yake moja kwa moja itakuwa ni batili na haina uhalali wowote kisheria katika kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini, siyo kitu cha busara kwa changamoto zinazojitokeza katika utunzi na uandaaji wa Sheria Ndogo kuletwa hapa Bungeni kila mara na kuweza kujadiliwa. Matatizo haya na changamoto hizi zinazojitokeza takribani Mabunge ya miaka yote kasoro zinazojitokeza ni zilezile. Kamati ya Sheria Ndogo inachukua jitihada za msingi kuisisitiza Serikali juu ya kuzidisha umakini kabisa wakati wanapoandaa hizi sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linalosikitisha zaidi katika utungaji wa sheria hizi siyo halali kwa Bunge hili kutaka Sheria Ndogo hizi kuingizwa hapa kabla ya kuanza kutumika huko hii ni kwa mujibu wa Tafsiri ya Sheria (*The Interpretation of Law Act)*, Kifungu Namba 37 na 38 (1) maana yake sheria inapokuja hapa Bungeni kuijadiliwa kwanza inakuwa tayari imeshatumika huko kwa wananchi kama wananchi kuumia tayari wameshaumia sana, sasa tutakapokuwa tunakosa u-

*serious* wakati tunapoandaa hizi sheria maana yake nini, moja kwa moja tunaenda kuangamiza wananchi ambao ndio walengwa halisi zinazokoenda kuwasimamia katika utumikaji wa hizi sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Sheria Ndogo kukosa uhalisia ni tatizo moja kubwa sana. Nakupa mfano sheria nyingi zilizokuja Bungeni kipindi hiki cha Bunge la Mkutano wa Tatu na la Bunge la Mkutano wa Nne zimekosa uhalisia katika matumizi. Nakupa mfano, kuna Sheria Ndogo ya kudhibiti ombaomba ya Wilaya ya Chunya iliyotungwa mwaka 2021 ukisoma hiyo sheria tafsiri yake inaweka wazi inatafsiri ombaomba kwa kumtambua kama mtu ambaye kaanza na ulemavu kitu ambacho ni kinyume kabisa na utaratibu wa Katiba. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano inahamasisha umoja, mshikamano na usawa kwa binadamu, lakini ukiisoma hiyo sheria kwa undani zaidi utakuja kubaini kwamba ubaguzi ni sehemu inayopewa kipaumbele. Nakupa mfano, ukiangalia Kifungu cha 10 katika hiyo sheria kinasema wazi kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ana mamlaka ya kumfukuza ombaomba kumrejesha Wilaya alikotoka na katika Mkoa alikotoka kwa kumkabidhi kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia mantiki ya hicho kifungu ni nini, unaweza kujiuliza hivi Mkurugenzi anapopata mamlaka ya kumrejesha ombaomba kwao hivi maombaomba wote wanaoenda Chunya maana yake Chunya hakuna ombaomba au sehemu nyingine ndizo zenye kutoa ombaomba na kupeleka Chunya hiyo moja, lakini unaweza kujikuta kwamba sheria hii mantiki yake ya kutungwa ni nini, tunaelewa *hypothetically* tunajua mantiki yake ya kutungwa ni nini, lakini lazima izingatie mahitaji ya watu kwa sababu suala la ombaomba siyo Tanzania tu, tunapokuja kumtungia sheria kwamba ombaomba, tumeshamuita ombaomba leo hii tunatengeneza sheria tukimkamata tunampiga faini ya Shilingi Laki Mbili maana yake nini, sasa huyu ombaomba au ni mtu mwenye uwezo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombaomba duniani kote wapo hata kule Marekani, ombaomba wapo tofauti ni majina tu, sisi tunawaita ombaomba kule wanaita nini *homeless people!* maana yake unga wa ngano, chapati ya unga wa ngano na andazi vyote ni kitu kimoja vinatumia jamii ya unga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kinaonyesha wazi kwamba sheria hizi haziendani na uhalisia halisi wawatanzania soma Sheria ya Uvuvi *(The Fisheries Regulatory Act,* ya *2009)* utaona wazi kwamba hii sheria haiakisi mahitaji ya wananchi walio chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano, ndani ya hiyo Kanuni hiyo unakuja kukuta kwamba miongoni mwa sifa ambazo mtu anatakiwa awe nazo wakati anapoamua kusafirisha samaki nje ya nchi, anatakiwa awe na *certificate of incorporation* sambamba na hilo awe na *article* na *Memorandum of Association* ya kampuni. Haya ni masuala ya kampuni *ideological* tunaimani kwamba *once the company is registered become legal entity* lakini kuna tofauti uhalali tunaoipa kampuni kutekeleza majukumu ya kibanadamu tunaiweka kwa misingi ya kwamba iwe na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa. Lakini hatuwezi tukamchukua binadamu kuwa na hadhi sawa na kampuni vitu hivi ni masharti ambayo hayawezi yakatekelezeka kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoweka mazingira haya lazima tuangalie wale watu wa tabaka la chini. Sheria hii imeenda mbali zaidi cha kushangaza zaidi kwamba wavuvi wamewekewa kina maalumu cha kuweza kuvua tuchukulie mathalani Ziwa Tanganyika lina maji ambayo hayatashuka mita 50, kina cha kwenda chini, lakini sheria ile imeweka mipaka mwisho uvuvi kuvua ni mita 20 kitu ambacho vipi nyavu zao zitakuwa zinavuta hawa samaki wa juu juu tu. Katika mita 150 ambazo zinatakiwa zivuliwe, wewe unaweka mita 20 wewe unayeweka mita 20 maana yake umeacha samaki katika mita 130 hizo umeziacha huru sasa hawa samaki wanauwezo wa kwenda sehemu yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba lile ziwa Tanganyika sisi tuna-*share* na wenzetu nchi kama vile Congo, sasa tunaposema tunawaacha wale samaki sisi, tumejitungia sheria ngumu, sheria ambazo haziwezi kutekelezeka, Congo wao wakienda kule wao watawavua, samaki siku zote hasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki kwanza hana *passport* atakapotaka kwenda Kongo, kwamba aende akakate *passport*, aende akaonane na uhamiaji ndipo aende kule, yeye ana uwezo wa kwenda hajijui sasa hivi yuko wapi anaingia wakati wowote na kutoka wakati wowote. Sasa tujaribu kuweka sheria ambazo ni rafiki kwa wananchi wa tabaka la chini, kwa sababu siku zote tunaposema tunapomuwekea mtu sheria rahisi basi inakuwa rahisi kuzifuata, lakini ukiamua kumuwekea sheria ngumu utamuona yule mtu adui. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana kuzingatia mahitaji halisi ya utungwaji wa sheria. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Simai Hassan, tunaendelea na Mheshimiwa Ramadhani sasa baadaye Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda Na Mheshimia Aida Khenani na Dkt. Pindi Chana, wajiandae.

**MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kupata fursa hii ya kuchangia kwenye hoja iliyoletwa mezani leo kutoka Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabla ya kutoa mchango wangu napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama kwenye Bunge lako Tukufu leo kutoa maoni yangu pia nimuombe Mwenyezi Mungu huyo huyo aendelee kumpa nguvu Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassain anapotekeleza majukumu yake ya

kitaifa akiwa nje ya nchi muda huu akiwa Misri Mungu ampeleke salama na amrejeshe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wachangiaji waliopita kama watatu kuanzia Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa *Advocate* Swalle na Kaka yangu Simai umeshaanza kuona picha kubwa ya jinsi sheria ndogo zinavyoleta changamoto. Bahati sijui niseme nzuri au mbaya kwa utaratibu wa kanuni za nchi yetu sisi Sheria zetu ndogo zinaanza kutumika kabla hazijaja kwenye Kamati ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake zinatolewa kwenye gazeti baada ya kutungwa halafu zinaingia mtaani zinaanza kufanya *operation* ya matumizi yake halafu baadaye zinakuja kwenye Kamati ya Sheria Ndogo kwa ajili ya uchambuzi ya kuona kwamba yale tuliyoelekeza watunga sheria yameendana na maelekezo ya Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida inapotokea ni kwamba sheria zinaweza zikawa zimeanza kufanya *operation* mtaani na zimeanza kutumika halafu sisi tunakuja kuona madhahifu yaliyomo mpaka tukiwaambia Serikali wakaribishe baadhi yao tayari zimeshaumiza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapotoa msisitizo wa kipekee kwa Serikali kuwa makini mara mbili zaidi wanapotunga Sheria Ndogo ndiyo tunatakiwa tueleweke hapo. Kwamba tunatoa msisitizo kwamba sheria hizi zitaenda kutumika kabla hazijapita kwenye Kamati za Bunge kwa ajili ya kuzi- *scrutinize,* kuzichunguza kwa makini na sisi kutoa mapendekezo ya yale tunayoyaona yanakosewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba Serikali kwa sababu wamepewa mamlaka na Sheria za Bunge katungeni Sheria Ndogo kwenye mambo haya. Kwa hiyo, wanakuwa Kamati zao Ndogo wanakaa kwanza, wanakaa na wadau zinaandikwa zinapita kwa Waziri anazisoma, anazisaini kwa hiyo tunawaomba makini mara tatu zaidi ya kuhakikisha kwamba Sheria Ndogo hizo

zinakuwa, zinapokuja kutumika kwenye jamii haziji kumi za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikutana na sheria moja ilikuja kwenye kamati yetu kwa ajili ya uchambuzi hii ya uhifadhi wa wanyamapori ni kanuni ya uhifadhi ya wanyamapori ya mwaka 2021. Kwenye kifungu cha 31 cha kanuni hiyo imekuja kuwapa mamlaka hili Jeshi Husu, Jeshi la Uhifadhi la Wanayamapori, mamlaka ya kufanya upelelezi kukamata, kufanya *searching* za kwenye majumba na watu ku-*secure* maeneo ya matukio kufanya *surveillance* kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati tunachambua tulikuwa tuna wasiwasi haya mamlaka kwa mujibu wa *criminal procedures* yamewekwa kwa vyombo maalum vinavyofanya upelelezi kwa mfano Polisi. Leo tunayachukua mamlaka haya haya tunaenda kuwapa Jeshi Husu wafanye na wao, siyo shida lakini umakini wa kuhakikisha tuna-*control behavior* za majeshi yetu wakati wa kufanya haya tunatakiwa tuwe makini mara mbili zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wanaenda kuingia kwenye haki za watu, unapopewa haki ya kumkamata mtu na kumfanyia upelelezi maana yeke utakaa naye, utamuoji lakini kwenye *criminal procedure* utaratibu wa jinsi polisi na vyombo vingine vya upelelezi vimepewa mamlaka kwa kwa mujibu wa *criminal procedure* na utaratibu mzuri ambao wao wanaufuata na baadhi ya wakati vyombo hivyo vingine vinampaka ma-*PGO*, wana *code of ethics* na *conduct* za kuhakikiha kwamba hawavuki, na hawaharibu haki za watu wakati wakitekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja katika vitu tunavyowaisitiza ni kwamba wahakikishe michakato ya kuwatungia *code of ethics* iende kwa haraka ili kuhakikisha kwamba hao waliopewa mamlaka sasa haya sasa hawaendi kuya-*abuse* haiendi kuyatumia kinyume na yanavyotakiwa kutumiwa kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda baadaye Mheshimiwa Aida Khenani,Dkt. Pindi Chana, na Mheshimiwa Santiel Kirumba, wajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na nilitaka nijielekeze moja kwa moja katika yale tuliyoyaona kwenye Sheria Ndogo hizi. Wenzangu waliotangulia wameeleza vizuri juu ya tatizo linaloonekana la Sheria Ndogo kuanza kutumika kabla ya kupita kwenye mamlaka ya Bunge na wanataka, mamlaka zinazotunga Sheria hizi ndogo ziwe makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuongeza neno jingine kwamba lazima Bunge lifikirie kubadili utaratibu huu uko mbele na kwamba Sheria ndogo zote ziwe kwanza zinadhibitishwa na ndiyo zinakwenda kutumika. Maana inawezekana umakini wengine wakaukosa na mkazusha malalamiko. Kwa hiyo, huko mbele mpaka sasa Sheria bado inatoa mamlaka ya kutunga kwa Sheria Ndogo na kuanza kutumika lakini huko mbele tunaweza tukafikiria kwamba mpaka ifike kudhibitishwa na kukubaliwa na Bunge ndiyo ianze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo tuliyo *experience* kwenye masuala ya Sheria Ndogo ipo vile vile Sheria Ndogo ya Uhifadhi na Usambazaji wa Madawa yaani *The Tanzania Medicine and Medical Devices Good Storage and Distribution.* Hapa napo tumekuta kuna tatizo na changamoto, moja ya changamoto tuliyoiona kwamba Sheria hii Ndogo kwanza inampa mamlaka mhifadhi na msambazaji wa dawa yeye mwenyewe kupokea malalamiko ya dawa zinapokuwa na matatizo, na wakati yeye ni mdau katika jambo hilo, wakati mwingine *manufacturer* wa hiyo dawa yuko nje ya nchi lakini huyu aliyepokea na kuzihifadhi katika uhifadhi na ushasafirishaji dawa inaweza ikapoteza

ubora na baadaye ikaenda kuleta madhara yeye mwenyewe Sheria Ndogo ilikuwa inampa nafasi ya kusikiliza malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni tofauti na Sheria nyingine, leo hii ikifika mahali ambapo kuna malalamiko ya mamlaka za kutoa mawasiliano kama vile vyombo, *Voda* sijui *Airtel* na wengine kuna *regulatory authority* ya kwao ambayo ni *TCRA* ndiyo itapokea malalamiko. Kwa hiyo, tulitaka mamlaka haya ya kupokea malalamiko ya juu ya *storage* ya madawa yanayopoteza ubora ya baki *TMDA* na yasiende kwa wale ambao ni *owner* wa *premises* za kuhifadhi. Kwa hiyo hilo ni moja la tatizo tuliloliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jingine ni suala la dawa kupoteza ubora wakati zikiwa katika maeneo ya *storage* na usafirishaji. Na kwamba lazima huko mbele hizi Sheria Ndogo zifikirie kuwe na utaratibu wa ku-*recall* yaani ambao unaweza ukafika mahali kukawa na utaratibu maalumu wa kuzirudisha dawa zilizoharibika kutoka kwa hawa ambao ni *owner* wa *premises* na wale ambao wana- *distribute* hizo dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika jambo jingine ambalo tume-*experience* ni kwamba utungaji wa hizi Sheria Ndogo vilevile wakati mwingine unakumbana na changamoto za kiutafiti. Kwa mfano; Sheria za Uvuvi hizi Sheria Ndogo za Uvuvi zimeweka mambo mengi ambayo yanakinzana na hali halisi ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, lakini unachunguza unakuta Wizara yenyewe ya Uvuvi na Mifugo inapewa bajeti ndogo sana. Kwa hiyo, katika masuala ya utafiti wanapata shida. Kwa hiyo, wanatunga kanuni kwa kuzingatia jinsi ambavyo wao wanavyofikiria zaidi kulikoni kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Ziwa Tanganyika ambalo lina kina cha zaidi ya mita elfu moja na kidogo, lakini eneo la *oxygen* ambalo linaweza linakaa viumbe kama Samaki ni mita 150. Lakini ukiangalia katika kanuni walizozitunga wanamkataza mvuvi kuvua kwa zaidi

ya mita 20. Kwa hiyo, kuna mita 150 nzima ambayo ipo pale ambalo ni eneo linaweza likavuliwa na hao wakapata mazao ya uvuvi na ambalo lina *oxygen,* lakini kanuni ile wala haifikii mita 20. Sasa hivi ndiyo tulikuwa tunafikiria wafikie mita 20, lakini kanuni ile ilikuwa inataka nyavu ziwe na macho 144 ambayo ni sawa sawa na mita 16. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunaona yanakinzana na mahitaji ya wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo tuliliona hili si la kiutafiti ni la kimlamlaka tu kwenye suala la uvuvi, wavuvi wameongezewa mzigo sana chombo chenyewe cha uvuvi kinalipa leseni. Lakini mvuvi mmoja mmoja anayeingia kwenye uvuvi naye kwenye kanuni hizi amewekewa leseni kila mvuvi awe na leseni. Na mbaya zaidi wavuvi hawa wanahama kutoka chombo kimoja kwenda chombo kingine akihama kutoka chombo kimoja kwenda chombo kingine ile leseni yake haitambuliki akifika kwenye chombo kingine lazima akate leseni nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeona katika utungaji wa Sheria hizi Ndogo kuna maeneo ambayo yanakinzana na hali halisi na kwa maana hiyo yanaleta ugumu katika kupata tija kwa watu wanaofanya shughuli kwenye sekta hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda tunaendelea na Mheshimiwa Aida Khenani baadaye Dkt. Pindi Chana pamoja na Mheshimiwa Santiel na Mheshimiwa Kasalali wajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi ambayo

wameifanya na kutuletea taarifa ambayo kweli inaoneka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa sheria ambazo zinawakuta wananchi moja kwa moja hasa wa kule chini ni Sheria Ndogo. Kazi ya Bunge ni kutunga sheria na baada ya kutunga sheria kabla haijaanza kutumika zinatungwa kanuni na hapo ndipo kumekuwa na shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mjumbe wa Kamati kwa Bunge lililopita Kamati ya Sheria Ndogo kulikuwa na makosa mengi sana yakiwepo ya uchapaji, kulikuwa na makosa ya uandishi wa sheria. Lakini nimpongeze kipekee Mheshimiwa Jenista alichukua hatua kubwa sana, lakini katika mambo ambayo tumekuwa tunashauri kila wakati ni pamoja na semina elekezi kwa wanasheria wetu wa halmashauri na hili jambo bado Mheshimiwa Waziri halijafanyika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ugundue kwamba kuna shida bado kumekuwa kuna tatizo aidha la uwezo mdogo wa wanasheria wetu kwenye halmashauri inafikia mahali yaani mtu anachukua sheria ya Tabora anaipeleka Nkasi ya Nkasi anapeleka Kalambo yaani imekuwa ni ku-*copy* na ku-*paste* hawana tena muda wa kufanya *research. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja sasa ya kutokuwa na haraka ya kutunga kanuni zetu tuwape muda wa kutosha wakafanye tafiti kuangalia uhalisia kabla hawajatunga kanuni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sheria itungwe kunakuwa kuna uhitaji sasa sasa hivi kumekuwa na shida kidogo ukizungumzia ukusanyaji wa mapato kila mtu anataka aonekane amefanya vizuri na hapo ndipo shida inapoanzia. Zinatungwa sheria ambazo ni kandamizi zinaenda kuwakandamiza wananchi ili mradi tu mtu aweze kukusanya vizuri kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kwenye hizi sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Sheria za Ushuru, miongoni mwa Sheria ambazo ni kero kwa watanzania tena wananchi wa kawaida ni Sheria za Ushuru, Tozo pamoja na Ada. Kuna haja ya kupitia eneo hili tuliangalie upya, lakini sheria nyingine ni Sheria za Wavuvi. Nilikuwa najiuliza hivi kuna wakati tunatunga hizi kanuni kumfurahisha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza wavuvi kwa mfano haya maziwa mawili tu; Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ukitazama Ziwa Tanganyika kuna nchi zaidi ya moja wanaotumia kwa ajili ya uvuvi hilo Ziwa Tanganyika, lakini tunatunga sheria za kuwaumiza wavuvi wetu halafu wavuvi wengine ziweze kuwanufaisha kwenye nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuachane na mfumo wa kufikiri sheria za kikoloni kama tunataka kukusanya mapato, kama tunataka tuongeze pato la Taifa kwenye uvuvi lazima tutengeneze mazingira rafiki kwa wavuvi ni pamoja na sheria zetu ambazo zitawasaidia wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kanuni ambazo ni za ajabu nani za hovyo za mwaka 2009 zimeletwa hapa baadhi tunashukuru Mheshimiwa Waziri amechukua hatua kwa baadhi ya kanuni kuziondoa na kutolea matamko na nini. Lakini matamko haya kama hayatawekewa msingi hayana maana yeyote. Shida ipo kule kwenye utendaji kwa mfano kama waliokuwa wanatunga kanuni walifanya *research* kwenye Ziwa Victoria ukapeleka hizo kanuni ziende Ziwa Tanganyika ni kwenda kuwandamiza wavuvi wa Ziwa Tanganyika ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, kuna haja kabla hatujatunga kanuni zetu wao wanapewa muda wa kwenda kuangalia mazingira halisi kabla ya kutunga kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili suala litakwenda vizuri hasa kabla hatujatunga tukiwashirikisha wadau, wahusika wa hiyo kanuni inayokwenda kuitunga kumekuwa na shida ya ushirikishwaji. Ukimshirikisha mtu siku moja mtu anayetoka Nkasi, anayetoka Kigoma si rahisi kuja Dodoma hapa kutoa maoni yake tutoe muda wa kutosha ili

tuwashirikishe na wale wakitoa maoni yao maana yake nini, utekelezaji wake wa hiyo sheria inakuwa ni rahisi kwa sababu wameshiriki kikamilifu, wameshiriki kutoa maoni yao kulingana na uhalisia wa mazingira ambayo wanatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dosari za uandishi wa sheria, kabla sheria haijafika mwisho kuna hatua kadhaa. Sasa mpaka inakuja kuonekana mwishoni kazi ya kamati hii si kwenda kuangalia makosa ya kiuandishi si kazi yake Kamati ya Sheria Ndogo. Lakini saa hizi wamekuwa wanatumia muda mwingi kuangalia makosa yaliyopo kwenye Sheria wakati wapo watu ambao hizi sheria zimepita mikononi mwao. Lazima tuangalie tatizo lipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye Sheria hizi ukiangalia tunajikita zaidi kwenye kuweka adhabu kwenye Sheria Ndogo kwa nini tunajikita kwenye adhabu? Na imekuwa shida sana ya uandaaji wa hizi kanuni tunajikita zaidi kwenye kuweka adhabu kwenye Sheria Ndogo kwanini tunajikita kwenye adhabu, na imekuwa ni shida ya uandaaji wa hizi kanuni, tunajikita zaidi kwenye kwenda kukusanya na adhabu kwa mwananchi. Lakini hakuna sehemu ya uwajibikaji wa Serikali wanapokuwa wanatunga hizo sheria lazima tubadilishe fikra zetu tunapokuwa tunatunga hizo kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zaidi Sheria kukiuka haki za binadamu hizi kanuni. Sheria yeyote inapokiuka haki za binadamu au kukiuka Katiba kwa maana Sheria Mama inakosa sifa ya kutumika. Lakini huko vijijini wananchi wetu wanaumia sana unakuta Sheria au Kanuni bado haijawa *Gazetted* imeanza kutumika na imeanza kuadhibu wananchi. Nani anawajibika kwenye jambo hilo si wananchi wote wanaweza kujua kwamba hii bado haina sifa ya kutumika hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Jenista amejitahidi makosa yale ya mwaka 2016 mpaka sasa tayari Sheria zile ambazo zimekuwa zimefuata utaratibu zinakuwa *gazetted* na analeta ndani ya Bunge

mambo ambayo yanakuwa yanaeleweka unapokwenda huko unakuwa unajua kwamba hiki ni sawa hiki hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kwenye suala la uwajibikaji linahitajika kwa sababu anapoumizwa mwananchi wa kawaida kwa makosa ya uandishi, kwa makosa ya sheria kutokuwa *gazetted,* lazima Serikali ianze kuwajibika kwenye mambo hayo. Na ili wawajibike lazima wawe wanapitia kule chini kwenye halmashauri waone mazingira yalivyo, lakini jaribuni kuangalia kweli uwezo wa wanasheria wetu kwenye halmashauri unajitosheleza? Hapo bado kuna shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilijikita kwenye ushauri nakushukuru kwa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana baadaye Mheshimiwa Santiel Kilumba, Mheshimiwa Kasalali ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kupongeza Kamati kwa uchambuzi wa taarifa yao ambayo imesomwa hapa leo. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa kazi nzuri ya kusimamia masuala haya ya sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kabla ya kuchangia nilikuwa naongea na wananchi wangu, nikawaambia kule Njombe nakwenda kuchangia masuala ya *by-laws.* Sasa wakaniuliza sisi watu wa Makambako, Makete, Njombe, Ludewa, Lupemba hizo *by-laws,* yaani unaposema kwamba zinapaswa kuwa *gazetted,* hizo *Government Gazettes* tunazipata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikiwa kama mwakilishi wa wananchi naomba nililete swali hili; wananchi wa kule Ludewa na maeneo mengine, hizi *Government Gazettes* wakitaka kuziona, ku-*access* wanazipataje? Maana zinatolewa kwa *Government Printers,* labda zinapelekwa

halmashauri; je, kule ngazi ya chini, siku hizi tumeshasomesha, Bodi ya Mikopo inatoa watoto wengi, wasomi wengi, sasa wakitaka kuziona wanazipataje? Kwa hiyo nitashukuru nikipata maelekezo, wananchi wakitaka kuzisoma zinapatikanaje kwenye ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napongeza sana hizi sheria ndogo, zina faida sana; kudhibiti magonjwa mbalimbali, mambo ya kipindipindu, kutotupa taka ovyo, ukataji miti; kwa hiyo hizi sheria ndogo zina manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo naomba kusisitiza tu ni suala zima la ushirikishwaji wa wananchi. Tunapowashirikisha wananchi, kwa mfano, tunasema tusikate miti ovyo, kutakuwa na jangwa; tusitupe taka ovyo, kutakuwa na kipindupindu, kwanza tuwape uelewa, tukishawapa uelewa ile *awareness creation* wao wenyewe watatusaidia kuelimisha jamii na watoto na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipowapa uelewa, ukamwambia mwananchi usikate miti, atakuuliza sasa nitapata wapi kuni za kupikia na huku vijijini; Ludewa, Makete, tunatumia kuni? Bado masuala mengine ya umeme na gesi baadhi ya vijiji hatujaboresha kupata gesi na umeme kwa sasa, viko kwenye mpango. Kwa hiyo ni muhimu sana kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale makatazo yote, *by-laws* zinazohusu kuacha kutupa taka ovyo, lazima tumwambie mwananchi usitupe taka, dampo hili hapa, au ukitaka kutupa taka *dustbin* hili hapa, lakini tukiwa tunasema tu labda usitupe taka, lakini hatuwaoneshi mbadala; usikate miti lakini hatumwoneshi kuni atachukua wapi; hayo ni maeneo ambayo ninaomba tuone namna ya kuboresha.

Kwa hiyo ushirikishwaji una faida na wao wenyewe wataendelea kuhubiri hiyo Injili kwa jamii, kwamba hapana, ni marufuku kutupa taka, ni marufuku kukata miti na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu suala zima la kupishana ambalo Kamati imeelezea vizuri, wakati mwingine sheria ndogo inapishana na ile sheria mama. Unakuta wakati mwingine sheria mama labda inasema faini isizidi laki moja na kifungo labda cha miezi sita, lakini sheria ndogo inaweza ikasema faini isizidi laki moja na nusu, kumbe sheria kubwa yenyewe inasema faini isizidi laki moja na ile ndogo imekwenda zaidi. Kwa hiyo hilo ni eneo ambalo ni muhimu tukaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kupongeza maeneo yote wanakotunga sheria ndogo, Serikali za Mitaa *(Local Government)* wanafanya vizuri sana na kwa kweli sheria hizi zina manufaa sana kwa wananchi wetu. Kwa sababu inategemea na *culture* ya hilo eneo, inategemea na jiografia ya hilo eneo. Kwa hiyo zile sheria ndogo zinasaidia kuratibu eneo hilo husika kutokana na jinsi wananchi wanavyoishi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusiana na suala zima la muda. Wakati tunapitisha hizo sheria, kwa kawaida, tuchukulie mfano za halmashauri zinapaswa kwenda mkoani na baada ya mkoani kwa kweli zinaenda ngazi ya Taifa. Kwa hiyo, wakati mwingine zikifika pale mkoani ninaweka ombi tu kwamba zisikawie, ule uchambuzi na kupitishwa. Kwa sababu zinapochelewa unakuta sasa utekelezaji wa hiyo sheria pia unaweza ukacheleweshwa. Kwa hiyo, niombe sana, zinapotoka halmashauri zinapokwenda mkoani, zisicheleweshwe, zikienda TAMISEMI pia zisicheleweshwe, zipate kurudi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichangie maeneo hayo ambayo nimeya-*table* na nitashukuru kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana. Tunaendelea na Mheshimiwa Santiel Kirumba,

Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa Joseph Tadayo wajiandae.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hii Kamati ya Sheria Ndogo nikiwa kama Mjumbe. Kuna mambo madogomadogo, kwanza katika sheria hizi zinazotungwa ni sheria ambazo zinaweza kutuingizia mapato sisi katika halmashauri zetu na sheria hizi zinagusa mwananchi *directly.* Kwa hiyo tunapozitunga lazima tuangalie sheria hizi zinaendana na uhalisia wa maisha ya mwananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kuishauri Serikali iwe inapitia kwa karibu sheria hizi kabla hazijafika mbali na kabla hazijaanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala moja; katika *GN* ya tarehe 9, Julai, Na. 589 ya *The Wildlife Conservation,* sheria hii kifungu cha 12(4) hakimpi mamlaka Waziri kutunga sheria na badala yake kinakinzana na sheria mama ambayo imemruhusu katika Kifungu cha 121(a) ambayo Waziri anapewa mamlaka kutunga sheria zozote ambazo zinamhusu. Kwa hiyo tunapenda kama Waziri husika afanye marejeo anapotunga sheria zake, aangalie kifungu hicho mama kinamwelekeza nini ili aweze kufanya kazi yake hii kwa ufasaha. Hata hivyo, ni watu ambao wanafanya kazi vizuri na tumeshirikiana nao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyohiyo *GN* ya Julai 9, 2021 Na. 589, hili ni jambo lingine la kushangaza, *The Wildlife Conservation Act* inaelezea kwamba mtu yeyote aliyeajiriwa katika Jeshi Usu haruhusiwi kufanya kazi nyingine yoyote, unapomaliza kazi uende ukapumzike. Wanaelewa kabisa hawa watu tulivyowaajiri vipato vyao ni vidogo, unapomwambia asijihusishe na kazi yoyote, ile sheria uliyotunga inakinzana na sheria mama ya *Labour Act, unless* uwe na *conflict of interest* katika lile jambo, lakini hakuna, unamwambia anapomaliza kazi yake asiende kufanya shughuli yoyote, sidhani kama hili liko sawa. Wabunge

wanaelewa vipato vyetu ni vidogo, uambiwe usijihusishe na jambo lolote au na shughuli yoyote, unapomaliza shughuli zako za Bunge uende ukapumzike; kweli itaweza kufaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri arudie tena hiki kifungu, akipitie. *Unless* kama haipingani, haina *conflict of interest,* awaruhusu hawa watu waweze kuendelea kufanya kazi zao nyingine. Kwa sababu mnaelewa hawa Jeshi Usu mishahara yao jinsi ilivyo midogo. Tukiendelea kufanya sheria ambazo zinawabana wananchi wetu wasijiingizie kipato, wasifanye shughuli nyingine, hiki kitu ni changamoto sana. Halafu kingine, inatengeneza hali ya uchonganishi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vitu ambavyo vinaongeleka, ni vitu ambavyo vinasaidika na ni vitu ambavyo vinawezekana. Naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako hapa na tulikuwa nao kwa pamoja, waipitie hii kanuni ya 24 iweze kuwapa uhuru hawa Jeshi Usu kufanya kazi nyingine. Naelewa wanaelewa kazi ngumu ambayo wanaifanya na hawa watu wanafanya kazi ngumu sana, lakini kama haiathiri sheria zao, naomba waruhusiwe hawa watu kufanya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu ni hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kirumba. Tunaendelea na Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mheshimiwa Joseph Tadayo na Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk wajiandae.

Mheshimiwa Kasalali hayupo. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Tadayo, baadaye Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote niipongeze sana Kamati, kwa kweli taarifa ya Kamati ni nzuri

sana, imeturahisishia kazi na imetufungulia vizuri jinsi ya kuchangia. Kamati imefanya kazi nzuri, tunaipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kusema ni kwamba sheria ndogo ni sheria kama sheria nyingine. Kwa bahati zenyewe zinagusa zaidi maisha ya kila siku ya wananchi. Kwa hiyo tunapozungumzia juu ya utungaji wa sheria ndogo nadhani tunahitaji kuwa makini sana kwa sababu zina umuhimu kwa vile zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi. Kwa hiyo hata tunapozungumza suala la utawala wa sheria, ambayo katika hiyo pia nataka kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali, suala la sheria ndogo ni sehemu ya sheria kwa hiyo utungwaji wa sheria ndogo nzuri na usimamizi wake unachangia sana katika suala la utawala wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naipongeza Serikali kwa sababu ukiona utulivu mitaani, haiwezi kuwa asilimia 100 ya utulivu, lakini ukiona hali ya utulivu mitaani, ukiona haya mambo ya kukua kwa uchumi na mambo mengine yote, hayo yote yanatokana pia na kuwepo kwa utawala wa sheria kwa sababu kila jambo ambalo linafanyika linapaswa lifanyike kwa mujibu wa sheria. Sasa ni sheria za namna gani, ndiyo hili ambalo tunalizungumza kwamba lazima ziwe ni sheria bora ambazo zimezingatia viwango katika utungaji wake na zinaweza kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema, kwamba Kamati imezungumza mambo mengi mazuri na wachangiaji wamezungumza vizuri, nizungumzie labda mambo matatu tu. La kwanza ni jambo ambalo limesisitizwa juu ya hizi sheria ndogo kuzingatia sheria mama na kuzingatia Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli yako mambo mengine ambayo ukiyatazama unaweza ukafikiri ni madogo, lakini yanatisha kidogo. Kwa mfano hili suala la ombaomba ambalo kumekuwa na utaratibu wa kusema haya, wamekamatwa warudisheni kwao. Sasa unajiuliza kwao ni wapi? Maana Katiba ya Nchi inasema una haki ya kuishi

mahali popote ilimradi huvunji sheria. Sasa nikivunja sheria hapa Dodoma nitahukumiwa tu, lakini sitaambiwa nirudi kwetu. Sasa hii ya kusema warudi kwao, najiuliza hivi kwao ni wapi? Kwa hiyo nadhani hizi sheria ndogo kuna haja ya kuzipitia kila wakati kuhakikisha kwamba hazivurugi mambo katika misingi kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuzingatia uhalisia pamoja na utafiti. Kwa mfano, kwenye Jimbo la Mwanga, kuna Bwawa la Nyumba ya Mungu pale; sheria na hata ukisoma kwenye leseni zao wanasema kwamba huruhusiwi kuvua samaki ambaye ukubwa wake ni chini ya inchi tatu. Sasa kwa miaka karibu 20 pale sasa hivi samaki wa pale hawavuki inchi tatu, wako hivyohivyo, wanataga mayai, wanajukuu hivyohivyo wakiwa wadogo. Kwa hiyo ina maana ukiamua kufuatisha hiyo sheria ni kwamba pale mahali hapatavuliwa kabisa na ukiifuatisha matokeo yake kila siku tutakamata wavuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi haramu nasema kwenye *inverted commas* kwa sababu nashindwa kusema ni haramu wakati ambapo huwezi kupata halali kwa vile samaki hawavuki kile kiwango. Ndiyo maana nikasisitiza kuangalia uhalisia na utafiti, kwamba sasa hapa tumefika mahali ambapo hatuwezi kupata hao samaki ambao umewaweka kwenye leseni.

Kwa hiyo, ni lazima kuwe na *exemption* kwa sababu haiwezekani sheria hiyohiyo ika-*apply* Ziwa Victoria, iende Ziwa Tanganyika, bado iende kwenye kabwawa kadogo kama kale ka kwangu ka Nyumba ya Mungu. Kwa hiyo kuzingatia uhalisia na pia utafiti wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu; ni vizuri *by-laws* zetu nyingi zikawa zinazingatia kwenye kuwezesha kuliko kuzuia. Nitoe tu mfano, hapa katikati kulikuwa na shida kubwa sana kwamba mtu alikuwa anakatazwa hata kukata mti ambao aliupanda yeye mwenyewe. Sasa unarudi kwenye Katiba ya Nchi, kwamba mtu ana haki ya kupata kipato halali kutokana na kazi halali aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu amepanda mti wake ili ukiiva auvune apeleke mtoto wake shule, siku ya kuukata unamkataza kwa sababu ya sheria. Nadhani sheria zingekuwa zimesisitiza zaidi kwenye kuwezesha upandaji wa miti ili tusije kugombana na mtu anayekata kamti kake kamoja shambani wakati kuna maeka na maeka ya maeneo ambayo haya miti ambayo yangeweza yakawekewa sheria yakapandwa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tukizingatia hayo; kwanza tukizingatia huo uandishi bora uliozungumzwa na Kamati, tuzingatie kwamba hizi *by-laws* zifuate sheria mama, zifuate Katiba; pili, utafiti pamoja na uhalisia; na tatu, kwenda kwenye uwezeshaji zaidi kuliko kuzia, nadhani tutakwenda vizuri na faida ya sheria ndogo tutaiona na utulivu wa nchi utaendelea kuwa vizuri na watu wataendelea kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu ni hayo mafupi, nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Tadayo. Tunaendelea na Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk na baadaye Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii iliyotolewa na Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yoyote duniani ipo kwa ajili ya kudhibiti hisia za wanadamu kwa kuwa mwanadamu anaweza kuamka leo vizuri, kesho vibaya, anaweza kukasirika, anaweza kufurahi sana akatoa maamuzi ambayo siyo sahihi. Sasa baadhi ya sheria ndogo zinaeleza kabisa kwamba jambo hili lililokosewa ataachiwa Mkurugenzi labda wa halmashauri fulani aamue kwa namna atakavyoliona kosa. Sasa nadhani tuiombe Serikali ifikirie kipengele hiki. Mwanadamu yeyote anaweza akamhukumu mtu vibaya kwa sababu tu hata ya mwonekano wake. Kwa hiyo tukiruhusu kwamba tumuache tu Mkurugenzi ahukumu

atakavyoona naona haitakuwa sahihi. Kwa hiyo naiomba sana Serikali jambo hili wafikirie kwamba lengo la sheria ni kudhibiti hisia za wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba kuna sheria hii ya madawa yaliyoharibika au yaliyo-*expire,* yasiyofaa, kufanya *recall,* kwamba labda yameathiri huko au yanaonekana yana madhara yakarejeshwa, Serikali ikaamua kurejesha zile dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria mama, mtu aliyefanya kosa hili anatakiwa alipe faini ya shilingi milioni moja. Hata wale wadau wa sheria hii walikuwa wanaona kwamba adhabu hii ni ndogo sana kulinganisha na kosa hili kwa sabbau hapa ni maisha ya mtu. Anaweza akala dawa ikamgharimu kuondoa maisha yake duniani au akapata athari kubwa ikamsababishia ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anaweza kulifanya kosa hili kwa sababu tu hakutegemea kwamba atapigwa faini ya shilingi milioni moja ambayo dawa ile ikiuzwa anaweza kupata hata milioni 100 ya faida. Ni vyema sasa sheria hii ikaangalia vizuri au ikaangaliwa upya ili sheria ndogo zinazotungwa zikaweza kupata unafuu wa adhabu angalau watu wakapata hofu ya kujali maisha ya wengine ambao ni wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii naihisi kama vile ni kama sheria ile ya mpira, mtu mpirani anaweza kuvunjwa mguu kabisa, lakini aliyevunja mguu hukumu yake aoneshwe tu kadi nyekundu, yaani anaoneshwa tu. Sasa nadhani Waziri na Serikali ifikirie maslahi ya wanaotumia dawa, kwamba wanaweza kuondoa maisha kwa sababu ya sheria kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naiomba Serikali ione huruma sana juu ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Chama hiki ni chama kinachopenda wanyonge sana, kinachopenda kuondoa kabisa ubaguzi, hakina ubaguzi kabisa; watu wenye ulemavu, wasio na ulemavu, wanadamu wote ni sawa. Sasa inapotungwa sheria ya kuwadhibiti

ombaomba halafu ukaainisha kabisa mtu mwenye ulemavu, sijui unawafikiriaje hawa ambao ni viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi, viongozi wenye busara, viongozi mashujaa, mahiri sana, unawafikiriaje hawa na Ndiyo chama kinachoongoza Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najiuliza mpaka tunafikia kutunga sheria ya kudhibiti ombaomba, hawa Maafisa wa Serikali waliopo pale wilayani, kuna Mkurugenzi na wasaidizi wake, kuna Mkuu wa Wilaya na wasaidizi wake, hawa wote wana maafisa wanaowasaidia. Sasa malengo ya kuweko maafisa wengi hawa ni nini kama siyo kuwasaidia hawa wengine ambao ni wanyonge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo dogo tu. Kama ni ombaomba, wewe ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, fanya utafiti; hawa ni ombaomba kwa uzururaji, kwa ulemavu, kwa ugonjwa au kivipi? Maana yake mpaka unafika kutoa hii sheria ya kuwadhibiti ni kwa sababu gani unafanya hilo jambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ombaomba wamo walemavu ambao sheria ya halmashauri inasema kwamba wewe uwapatie asilimia mbili ili kuwawezesha. Tungetegemea sasa halmashauri imwombe Waziri au itengeneze sheria kuliomba Bunge kwamba sasa hawa ile ruzuku wanayopewa kwa mkopo basi wapewe tu bila kurejesha kwa sababu ni walemavu, lakini leo halmashauri inasema inataka kuwadhibiti. Inakuwaje Serikali yetu ya wapenda wanyonge inayoongozwa na viongozi wenye busara sana, leo unasema kwamba ombamba wadhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sheria kama itatekelezwa, maana yake haitamalizia hapo. Kuna watu wataharibikiwa na safari njiani, wataenda kwenye taasisi za dini; kuna mtu ataenda Kanisani, mwingine ataenda Msikitini ataomba, jamani nimekuja hapa nimeharibikiwa na safari; na watu wakiwa na roho mbaya wanaweza kumshitaki, kwa sababu ni ombaomba pia. Kuna watu wanaojenga taasisi za dini kwa kupitia michango ya wanadini wenzao, watu wakiwa na roho

mbaya wanaweza kumshitaki kwa sababu sheria hii ya kudhibiti ombaomba ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana waliotunga sheria hii watuonee huruma sana, hasa Chama chetu cha Mapinduzi kinachopenda wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk. Sasa tunamalizia na Mheshimiwa Ndaisaba na baadaye nitampa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro kwa dakika chache na baadaye Mheshimiwa Jenista Mhagama ili waweze kufafanua yale machache ambayo yalitakiwa yatolewe ufafanuzi.

Karibu Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nitumie sekunde chache sana kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Kwa kuridhia na kutoa leseni ya kuchimba madini ya *Nickel* yaliyoko kwenye Jimbo la Ngara. Wananchi wa Ngara wana imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais, wanampenda; na siku akitua Ngara tutayabeba yale magari ya msafara anayokuja nayo Rais. Kwa kweli tunamshukuru sana Rais kwa kuweza kutoa leseni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye mchango wangu na niende moja kwa moja kwenye mgongano wa masilahi. Wakati tunafanya uchambuzi, tuliletewa sheria kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kwenye sheria ile Kifungu cha 32(2) kinaruhusu Maafisa wa Serikali na wale waliopo kwenye ofisi hiyo ya Makamu wa Rais, (Mazingira) kuweza kushiriki kwenye zabuni za kufanya tathmini ya masuala ya mazingira *(environmental impact assessment)* pamoja na *audit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari na kuichambua kwa umakini ile sheria tuliyoletewa, tuligundua kwamba Mkurugenzi wa Taasisi ya Serikali ambaye ameajiriwa kama mtaalam wa kutoa huduma za mazingira, ana uwezo wa kushiriki kwenye zabuni, na kitakachotokea ni mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mkurugenzi wa Kampuni hiyo hiyo ama Taasisi ya Serikali imetangaza zabuni, halafu naye akaomba *tender*, halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Manunuzi akamnyima *tender* bosi wake, kitakachotokea pale ni kwamba yule mtu atapangiwa kazi ya kufagia, *consequence* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kama huyu mtumishi wa Serikali ameshiriki naye kuomba *tender* ambayo imetangazwa na Serikali, kitakachotokea pale, *quality* ya ile kazi inaweza kuwa *jeopardized.* Kwa sababu, kwa mujibu wa Sheria ile ya Mazingira, wataalam hawa wa Serikali wanaofanya *EIA*, wanatakiwa kwenda kuhakiki taarifa iliyoandikwa na mtu aliyepewa kazi ya kwenda kufanya *EIA*. Sasa kama tuna sheria inawaruhusu nao kwenda *ku-compete* na kuomba kazi hizo, hawawezi kusimamia vizuri kule wakati nao wanatakiwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitafakari sana eneo hili tukagundua kwamba wataalam hawa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira walioweka Kanuni hii, waliongozwa na uroho na ndiyo maana wakaweka Kanuni *inayowa-favour* wao wenyewe ili waweze kuomba kazi wanazozitangaza wao wenyewe na waweze kuzifanya wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba wewe na Serikali, kazi hizi tuwaachie *private sector* na twende tukafanye marekebisho ya kipengele hiki kuhakikisha kwamba tunaondoa kabisa mgongano wa masilahi kwenye shughuli zote zinazohusiana na masuala ya *environmental impact assessment* pamoja na *environmental audit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunafanya uchambuzi, Mezani kwetu ilitua Sheria Ndogo kutoka Halmashauri ya Bumbuli. Sheria hii inahusu ada na ushuru mbalimbali wa mazao kwenye Halmashauri ya Bumbuli. Kanuni ya 9(8) inasema mtu yeyote haruhusiwi kubeba ama kununua mazao kama hana kibali na risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliitafakari sana hii sheria, tukagundua kwamba sisi Watanzania muda wote hatuna mahitaji ya kutosha. Ukiamua kununua kilo mbili za karanga, unakwenda dukani unachukua karanga zako unarudi nyumbani. Sasa Maafisa wa Serikali hasa wa Halmashauri wana uwezo wa kutumia vibaya vifungu hivi vya sheria na kuanza kuumiza wananchi. Katika hali ya kawaida, hakuna mwananchi anayeweza kupata kibali kwenda kununua mazao gunia moja, debe mbili au debe tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba kwa unyenyekevu mkubwa, Kanuni hii ifutwe kabisa, isipite kwa sababu Kanuni hizi tunapozipitisha ndizo zinakwenda kuleta kero kwa wananchi na matokeo yake wananchi wanaichukia Serikali yao, wanachukia viongozi wao kwa sababu ya hizi sheria tunazozipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Sheria ya Kudhibiti Ombaomba ambayo wenzangu wameshaisema kidogo. Nami nijielekeze kwenye *concept* inaitwa *anthropology.* Huu ni utaratibu wa kusaidiana kama binadamu. Dunia nzima ombaomba wapo, sema wenzetu *wame-advance* na kuita *Homeless, American Beggars*, *Tanzanian beggars, all are beggars*. Halmashauri ya Wilaya ya Chunya wametengeneza Sheria ya Kudhibiti Ombaomba kabisa. Tena wameenda mbali, Mkurugenzi amkamate ombaomba ampeleke kwa *RAS*. Sasa tukajiuliza *RAS* ana utaratibu wa kupokea ombaomba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli hawa watu ni ombaomba au ni watu wenye uhitaji? Ifike mahali kama nchi tubadilishe baadhi ya *terminology* ambazo ndani yake

zinaleta *ambiguity*. Kunaweza kukawa na tafsiri hasi kwenye baadhi ya maneno tunayoyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuomba Wizara husika ikiwezekana wapige marufuku kabisa hili neno ombaomba na badala yake tubadilishe tuseme ni watu wenye uhitaji. Kwa sababu watu hawa badala ya kusaidiwa, sisi tunaona ni ombaomba, sasa tunatunga sheria tuwakamate tuwarudishe walikotoka. Sheria hii ni ya kibaguzi na tunaomba isipite kabisa kwa sababu madhara yake ni kufanya wananchi waichukie Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameshazungumza mambo mengi tuliyokutana nayo wakati tunachambua hizi sheria ndogo ndogo. Nikuhakikishie kwamba sheria inapotua kwenye Kamati yetu, tunaichambua neno kwa neno, mstari kwa mstari na tunakwenda mbali kuchambua maana halisi iliyopo kwenye vifungu vile tulivyoletewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingi tulizozipokea kama ambavyo nimekuonyesha hapo, zina vipengele vya ovyo ovyo ambavyo vinaweza kutuchonganisha na wananchi na kufanya wananchi waweze kuichukia Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa Bunge lako Tukufu lisipitishe maeneo yote tuliyokwishaonesha kwamba vifungu hivi havifai, vitafanya wananchi waichukie Serikali. Lengo la sheria hizi ni kuchochea maendeleo na siyo kukusanya ushuru tu hata kama wananchi wana hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisaba. Huyo ni mchangiaji wetu wa mwisho kabla sijamwita mtoa hoja, basi naomba nimkaribishe Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro kwa dakika mbili, halafu baadaye Mheshimiwa Jenista naye pia kwa dakika chache aweze kuweka sawa baadhi ya maeneo. Karibu Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Rweikiza; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ridhiwani na Wajumbe wote wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa michango yao kwa mawazo yao, kwa maelekezo yao ambayo wameitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee eneo moja linalohusu zuio au katazo kwa askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu wasiweze kufanya shughuli nyingine. Hili ni moja kati ya Jeshi Jipya ambalo limeanzishwa mahususi kabisa ili kulinda rasilimali ambazo tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo inasifika sana kwa kuwa na rasilimali za maliasili bora kabisa duniani. Rasilimali hizo zinapaswa kuendelea kulindwa na ndiyo maana Serikali iliona umuhimu wa kuanzishwa kwa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokifanya kwenye Kanuni hiyo ni kujaribu kuimarisha utendaji na nidhamu ya Jeshi, kwa kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa kimasilahi. Kwa sababu, askari hawa ambao wanafanya kazi katika maeneo ya maliasili na utalii, wasije wakashawishika na wao kujiingiza katika shughuli zinazofanana na maliasili na utalii. Tukiruhusu hilo, baada ya kulinda rasilimali hizo watakuwa wao wanazitumia kupitia shughuli zao za ziada wanazozifanya. Kwa hiyo, hatuwazuii kufanya shughuli nyingine kama za kilimo au biashara nyingine yoyote ili mradi isiingiliane na masuala ya uhifadhi na utalii na isiwe na mgongano wa kimasilahi na mwajiri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashukuru kwa Kamati kuibuka na hoja hiyo. Tumejadili na Kamati na tumewaeleza kwamba nia ya Serikali siyo kujaribu kuwakomoa askari hao; siyo kujaribu kuwatoa kabisa na kuwaongezea umasikini, la hasha, ni kuleta nidhamu na

kuondoa uwezekano wa kuwepo mgongano wa kimasilahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba askari hawa wanapewa silaha, wanakabidhiwa kulinda hayo maeneo. Sasa ukiwaruhusu wafanye shughuli za kibiashara, kwenye maeneo ambayo wamekabidhiwa kulinda, kwanza *wata-take advantage* dhidi ya *private sector* nyingine, kitu ambacho tutakuwa tunakwenda kuua *private sector* yetu; na pili, kutakuwa na uhujumu wa rasilimali hizo kwa sababu anayelinda unamruhusu pia aweze kuzivuna au kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro kwa ufafanuzi huo. Karibu sasa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hiii nafasi, lakini sitakuwa nimetenda haki kama nami sitaungana na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho, kumshukuru sana sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya na wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho wamesema kwa kweli wanamshukuru sana sana kwa fedha nyingi alizozipeleka kwenye Jimbo la Peramiho, kwa ajili ya kuleta maendeleo. Tunamwambia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Peramiho wamesema kwa kweli wanakubaliana na ule usemi unaosema, unapokutana na mtu ambaye yuko *strong,* kazi yako wewe ni *kum-support*. Kwa hiyo, sisi *tunam-support* Rais yetu kwa sababu yuko *very strong,* ameamua kuleta mabadiliko kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, *tunam-support* lakini wananchi wa Jimbo la Peramiho wanasema, Mheshimiwa Rais kwa sababu ameamua kuwa *hard worker,* Waswahili

wanasema, mtu wa namna hiyo anatakiwa kuwa *encouraged*. Kwa hiyo, nasi *tunam-encourage* Mheshimiwa Rais kwa kazi yake nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa niyaseme hayo kwa sababu nisingewatendea haki wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye Kamati yetu ya Sheria Ndogo. Kwa niaba ya Serikali naomba nichukue nafasi hii kwa kweli kumshukuru sana sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Rweikiza, Wakili msomi. Pia namshukuru sana Wakili msomi mwingine, Mheshimiwa Ridhiwani ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo; na Wajumbe ambapo Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kweli ni wabobezi na ni wataalam kabisa kwenye mambo haya ya sheria na wamekuwa ni msaada mkubwa sana kwa Serikali katika kufanya mapitio ya hizi Sheria Ndogo na kutushauri mambo ya msingi sana. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ninaomba niwashukuru sana, ahsanteni sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tunayo safari ndefu katika kufanya mageuzi ya kutosha katika uandishi wa Sheria Ndogo.

Naomba niwakumbushe tu watumishi wa Umma na hasa hawa ambao wamekuwa wakitusaidia kutuandikia hizi Sheria Ndogo kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na Taifa kwa ujumla. Ibara ya 35(1) inaeleza wazi kwamba shughuli za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zitatekelezwa na watumishi wa Serikali, lakini wanatekeleza shughuli hizo kwa niaba ya mwenye Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana, wanapokuwa kwenye kazi hii ya kutunga Sheria Ndogo wajue wamekasimiwa jukumu hili na mwenye mamlaka ya Serikali hii. Kwa hiyo, umakini katika utungaji wa Sheria Ndogo unahitajika kwa viwango vya juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kama hatutakuwa tunaelewana ndani ya Serikali na hasa hawa watumishi wa Serikali ambao wamekasimiwa madaraka ya kutusaidia kutunga Sheria Ndogo kwa mujibu wa Bunge; limekasimu madaraka kwa Serikali ili kutunga Sheria hizi Ndogo kwa ustawi wa Watanzania. Sasa wanapokiuka misingi bora ya utungaji wa sheria, kwa kweli hawatendi haki kwa Serikali yetu. Kama makosa hayo yanajirudia siku kwa siku, nawaomba sana wakae chini, watafakari na kufanya marekebisho ya kutosha kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Sheria Ndogo ambao wamekuwa wakiutoa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafanya nini sisi ndani ya Serikali? Tunafikiri tufanye mapitio kwa ujumla wake. Kwanza, tunataka sasa tuangalie hivi ni sekta zipi ambazo zinaongoza kwa kuwa na Sheria Ndogo mbovu, ambazo zinakataliwa kila siku ndani ya Kamati ya Sheria Ndogo? Ni lazima ifike mahali sasa tunakubaliana ndani ya Serikali tujue sekta hizo ambazo zinarekebishwa kila siku lakini bado hazina umakini katika utunzi wa Sheria Ndogo. Ni sekta zipi zinazoongoza? Tukijua hivyo, tutajua je, ni makusudi ama je, wataalamu wetu kwenye sekta hizo wanaotusaidia kutunga Sheria hizi Ndogo umahiri na ubobezi katika kazi hiyo ni wa chini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeamua sasa kwa kweli hebu tujitafakari tutazamane kwanza sisi wenyewe kwenye hizi sekta. Ni sekta ipi inayoongoza? Tukijua hilo, itatusaidia kutoka mahali hapo. Vinginevyo itakuwa ni marudio, marudio. Kamati ya Sheria ya Ndogo itakuwa inasema tunapokutana makosa ni hayo hayo, ni hayo hayo. Lazima tutafute mwarobaini na jambo hili liishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ninapongeza Wabunge wamesema hapa, ukiangalia *trend* kwa sasa hivi, makosa yanazidi kupungua, siyo kama tulivyoanza huko nyuma. Huko nyuma akina Mheshimiwa Aida wanajua, ilikuwa Kamati ikija kusoma hapa taarifa yake, makosa hayo yanaweza kufika 400 mpaka 500. Sasa hivi tunapopongezwa

leo Serikalini, kwa kweli juhudi imefanyika na wala siyo ya kwetu sisi kama Serikali tu, Bunge limetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mwenyekiti anapokuja kusema makosa yako 70, hiyo kwa kweli kwangu mimi ambaye ninajua historia, tulikotoka mpaka tulikofika, ni *achievement* kubwa. Hatuwezi kujipongeza peke yetu, tunawashukuru sana Bunge na tunaishukuru sana Kamati ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, uko usemi wa Kiswahili kwamba mgema akisifiwa tembo analitia maji. Tusingependa tufike hapo, kwamba tumepunguza hayo makosa mpaka kufika 70 leo kwenye ripoti ya Kamati, tungependa yaishe kama inawezekana. Ila yakiisha Kamati ya Sheria Ndogo sasa kazi itakuwa…, lakini tungependa yaishe. Ikiwezekana yaishe yote na hilo ni kazi yetu kama Serikali lazima tujitahidi tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba kwa kuwa hali ni hiyo, ni lazima tuungane pamoja na Kamati ya Bunge kuona ushauri wanaotupatia unaweza kutekelezwa kwa kiwango kikubwa ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii ndani ya Bunge lako Tukufu, kwanza ninapokea maelekezo ya Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo kama yalivyowasilishwa hapa kama hoja ya msingi na mtoa hoja atakuja kuhitimisha, lakini nitumie nafasi hii mbele ya Bunge hili kuwaagiza Watendaji wa Serikali wote huko ambako wanatutungia hizi Sheria Ndogo, wale waliokasimiwa hayo majukumu yetu ya kutunga Sheria Ndogo mambo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kuhakikisha sheria zote zilizopitiwa na Kamati Ndogo na zikaonekana zina dosari na hasa zile zinazokinzana na Sheria Mama yaani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wafanye marekebisho hayo haraka sana wawasilishe kwa Waheshimiwa Mawaziri ili sheria hizo ziweze kurudi kenye Kamati ya Sheria Ndogo zikiwa zimeondoa tatizo hilo la

ukinzani kati ya Sheria Ndogo, Sheria Mama na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni Sheria Mama yenyewe. *(makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niwaombe sana wajitahidi kuondoa tatizo hilo la ukinzani wa Sheria Ndogo na Sheria ya Msingi ambayo imeruhusu uwepo wa hiyo Sheria Ndogo yenyewe, kwa hiyo mimi naomba nichukue hilo agizo na niseme hapa na mimi nitakwenda kufatilia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu tuko hapa Mawaziri wote tutakwenda kufatilia kwenye sekta zetu kuangalia tatizo hilo linaondoka. Pia liko tatizo hili la uandishi bora wa sheria kwa kutumia vifungu vya Sheria Mama na maudhui yake ambavyo vinakwenda kujiwakilisha kwenye tafsiri ya Sheria Ndogo, kwa hiyo jambo hilo pia tumelichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana tunapokea huo muktadha uliooneshwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni namna gani Sheria Ndogo imetungwa ambayo haiakisi uhalisia wake wa kutumika nchini, lakini inavunja pia matakwa ya kikatiba ya usawa wa binadamu kwa kubagua makundi ya watu, kwa hiyo jambo hilo kwa kweli siyo jambo jema tutarudi tutaona ndani ya sheria hizo zilizorudishwa na Kamati Ndogo kuona namna gani tunafanya. Tutaendelea kushughulikia na niendelee kuwakumbusha wale Waandishi wetu wa Sheria ambao sheria zao zimerudishwa kwa sababu majedwali yanatofautiana na Sheria Ndogo na Sheria Mama, jambo hilo pia tutakwenda huko kulifanyia kazi ili kuhakikisha linafanyiwa marejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa michango ya Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Pindi Chana alitaka kujua magazeti ya Serikali kama yanapatikana na kama yanapatikana yanapatikana wapi. Huko nyuma Magazeti ya Serikali yalikuwa yanauzwa shilingi 1,000 kwa nakala moja, Mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan na Serikali yake ya Awamu ya Sita, imeamua tufanye marekebisho makubwa katika mfumo mzima wa upatikanaji wa Magazeti ya Serikali. Jambo la kwanza ambalo tumelifanya Ofisi ya Waziri Mkuu

imekwishakutoa maelekezo, magazeti haya sasa yatakuwa yanapatikana bure nchi nzima ya Tanzania bila ya kulipiwa, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Pili Mheshimiwa Pindi Chana ameeleza jambo la msingi sana, haya magazeti tunao vijana sasa hivi wasomi mikopo hii ya elimu bure wasomi wetu wapo wengi huko kwenye maeneo yetu, wangeweza kuyapata na kuyatafsiri na kuwasaidia wananchi kulelewa magazeti ya Serikali yanasema nini. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kupitia Mheshimiwa Pindi Chana aliyetoa hoja hapa, sasa hivi kuanzia tarehe Mosi Mwezi Novemba, magazeti haya yote ya Serikali yanapatikana kwenye *website* ya ofisi ya Waziri Mkuu na *website* ya ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa hiyo, yanapatikana huko bure hawa vijana wetu wasomi wanaweza kuyapata huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wako wananchi wengine hawawezi kufikia kwenye hayo maeneo ambayo wanaweza kuyapata kwenye *website*, tumeagiza mamlaka zetu kwenye Serikali za Mitaa wanao uwezo pia wa ku *download* hayo magazeti na kuyaweka kwenye ofisi zao, kwa hiyo sasa hivi magazeti haya yatakuwa yanapatikana na kigezo cha kuuzwa haya magazeti kwa sasa hivi hakipo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu ninaomba niwashukuru sana Wabunge na niendelee kutoa *commitment* yetu kama Serikali, kwanza Mawaziri wote mimi na wenzangu pale tutakapohitajika mbele ya Kamati ya Sheria Ndogo, tutakuja kupokea na kutoa maelezo katika kila sheria ambayo Sheria Ndogo wanataka tuje tuitolee maelezo. Pili tutakwenda kusimamia kuhakikisha sheria hizo zinafanyiwa mabadiliko zile ambazo zilikuwa zina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nikuombe, Kamati ya Sheria Ndogo itusaidie wanapopitia Sheria Ndogo zile sekta ambazo zimeonesha kufanya vizuri katika utunzi wa

Sheria Ndogo tungeomba kwenye ripoti ya Mheshimiwa wa Kamati sekta hizo basi na zenyewe zingekuwa zinatajwa ili tujue akina nani angalau wameweze sasa kubadilika na kufanya vizuri katika utungaji wa Sheria Ndogo, ambazo zinakidhi maudhui na mawanda ya uwepo wa Sheria Ndogo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikia na ofisi ya AG basi tutayatekeleza hayo yote kwa ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kwa kuchukua *commitment* hiyo kubwa kwa niaba ya Serikali, sasa naomba nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo ili aweze kuja kuhitimisha hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata jumla ya wachangiaji 13 kwenye hoja yetu na niwashukuru sana wote waliochangia kwa umakini mkubwa na ufasaha mkubwa kiasi kwamba hoja imeeleweka vizuri kwa wote na imeonesha ufanisi mkubwa. Kipekee niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri Mheshimiwa Damas Ndumbaro na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa majibu ya mwisho hapa ambayo yamezidi kuweka sawa sawa hoja nzima na kujibu zile hoja ambazo Wabunge wamezionesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapochambua sheria hizi ndogo tunachoweza kusema hapa ni kwamba tunaweka mazingira safi ya utawala bora, kama alivyosema mmoja ya wachangiaji Sheria Ndogo hizi zinawahusu sana wananchi wote siku kwa siku, ni sheria kama sheria nyingine zina nguvu

sawa na sheria nyingine na niseme labda wakati mwingine kuzidi sheria nyingine, kwa sababu ziko huko chini kwenye *grass root* watu walipo na zinatumika kila siku iwe kwenye usafi wa mazingira kwenye kutunza miti na mazingira kwa ujumla uvuvi boda boda yaani ndiyo zinazohusika hasa katika maisha ya kila siku ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi zina nguvu sana kwa sababu zinatoa faini zinatoa vifungo kwenda jela kwa fidia ndogo unaweza kwenda jela, zinaweka mazuio na mipaka mbalimbali, zinahalalisha mambo mbalimbali na kuharamisha mambo mbalimbali kwa hiyo zina nguvu nyingi kama sheria nyengine za nchi, hakuna tofauti kwamba ile neno kwamba Sheria Ndogo basi ni Sheria Ndogo siyo ndogo ni sheria zenye nguvu kama sheria nyengine.

Kwa hiyo, zikitungwa hovyo hovyo zinaathiri sana maisha ya watu ya kila siku na tunayopitia kila siku hivyo inabidi zitungwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba inatoa maelekezo mbalimabli na mamlaka mbalimbali sheria zitungwe vipi, kwa hiyo siyo sahihi kwa Sheria Ndogo kuja na mazingira ambayo yanakinzana na Katiba. Kwa mfano, amesema mchangiaji mmoja hapa Mheshimiwa mmoja amesema Katiba inatoa haki na wajibu wa kufanya kazi kwa mtu yoyote awe kampuni awe mtu binafsi, lakini wanasema kwamba ukitaka kufanya biashara ya samaki sharti uwe kampuni sasa hii inakiuka Katiba, siyo sahihi kuwepo na lazima ishughulikiwe na ifanyiwe masahihisho. Mfano mwingine anasema Mhifadhi wa Misitu anaweza kusitisha kibali cha kushughulika na mazao ya misitu na hana kikomo hana ukomo inaweza kuwa miaka 10 miaka 20 yaani daima dumu anakufutia tu kibali, sasa hii siyo sawa inakinzana na masharti ya Katiba na Sheria nyingine zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongea Wabunge wengi kuhusu Sheria ya Ombaomba katika Wilaya ya Chunya, wameeleza vizuri ni sheria ambayo kwa kweli ni ya kibaguzi, unambagua mtu kwa ulemavu siyo jambo zuri,

unamwambia apelekwe Mkoa wa kwao akabidhiwe kwa *RAS* na *RAS* ampeleke kwa *RAS* wa kwao, sasa *RAS* huyu ampeleke wapi na kwao ni wapi ameuliza Mheshimiwa mmoja. Je, ina maana Chunya pale hakuna raia ambao ni ombaomba ambao wanafanya kazi za ombaomba pale pale, kwa hiyo Sheria hii ni ya kibaguzi na haifai kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika wamesema lina kina kirefu zaidi ya mita 1,000 lakini samaki anaweza kuishi kwenye mita 150, unaporuhusu tu mita 20 ndiyo wavue hizi nyingine mita 130 avue nani? Samaki kama walivyosema hazina mipaka znaweza kwenda Congo zinawaza kwenda nchi nyingine jirani na watu wakafaidi kule na sisi tunajinyima uchumi ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema Waheshimiwa Wabunge kwamba inasikitisha kwamba sheria hizi zinatumika huko kabla kuja Bungeni, kwa kweli hili ni jambo la msingi sana, bahati mbaya ni nyingi sana, ni nyingi kweli kwa maelfu kwa maelfu sasa ukisema zije kabla zitakuwa hazitumiki zitachukua muda mrefu sana kutumia kwa huko kwa wananchi, lakini kwa kweli ni jambo zuri la kufikirika ni la kufikirisha kwa sababu zikitungwa sheria mbovu anaelaumiwa ni Bunge nani anaelaumiwa, mtunga sheria ni mmoja ni Bunge wale wengine wote wamekasimiwa *delegated* awe Mkurugenzi awe ni shirika gani amekasimiwa na Bunge, Bunge ndiyo mwenye lawama kama sheria hiyo itaonekana kwamba ina kasoro au mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomruhusu mtu ambae ni *interested part* ana maslahi binafsi kwenye sheria fulani, halafu hashiriki humo tunafahamu kwa mfano katika Halmashauri Madiwani hawaruhusiwi kushiriki zabuni za ujenzi wa barabara mle za ndani kwa sababu wana maslahi binafsi, sasa unaporuhusu hawa wasimamizi wa mazingira washiriki kwenye ile kazi ya kusimamia mazingira ina maana umeruhusu *conflict of interest* mgongano wa maslahi, haiwezekani lazima sheria kama hiyo ifanyiwe kazi ya kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa na tumeiona kwenye uchambuzi wetu, uvuvi katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, mwenye chombo ana leseni mvuvi ana leseni, chombo chenyewe kina leseni na huyu mvuvi akihama kazi kwa mwenye chombo akaenda chombo kingine leseni ile inaisha nguvu haina kazi tena, akienda kwa chombo kingine alipie leseni nyingine na anaelipa ni mwenye chombo, sasa ni mateso ambayo tunawapa wenye vyombo na kuwaongezea gharama ambazo hazina maslahi wala hazina faida kwa nchi yetu, tunawatesa, tunawakosesha mapato tunawakosesha kazi na siyo jambo ambalo lina busara yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa ya uchapaji unapochapa sheria ovyo ovyo unainyima uhalali wa sheria, mkienda Mahakamani Wanasheria utaangushwa chini mara moja, kwa sababu watakwambia hii umeitungia chini ya sheria gani? uliyoweka umekosea! Kwa hiyo lazima uwe makini unapoandika sheria iwe ndogo iwe kubwa isikinzane na Sheria Mama au sheria nyingine kubwa au ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mheshimiwa mmoja hapa sheria Kubwa inaweza ikawa inasema faini ni Shilingi Laki Moja, Sheria Ndogo inasema faini Shilingi Laki Moja na Hamsini, hii ni kinyume kabisa na utaratibu wa utungaji wa sheria na haifai kuwepo, ni lazima hiyo ifutwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema na walivyosema Wabunge wengine sheria hizi zinahusu maisha ya wananchi wetu, wananchi wenzetu ya siku hadi siku, lengo lake ni kukuza utawala wa sheria, utulivu, amani na ustawi na maeneleo na si kinyume chake, siyo vinginevyo, amesema Mbunge mmoja kutoka Kilimanjaro pale nyumba ya mungu unasema samaki wasivuliwe chini ya nchi tatu, amesema kwa miaka 20 hao samaki hawajawahi kuwepo, sasa unashangaa unajiuliza hawa waliotunga sheria hii hawajui mambo haya walitunga kwa sababu gani? Unasema nchi tatu ndiyo kiwango cha chini lakini sasa hawajawahi kufika kwa miaka

20, kwa hiyo unakusudia nini unapotunga sheria ya namna hiyo na ili iwe nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazuia mtu kukata mti ambao aliupanda mwenyewe, sasa unashangaa kapanda mti mwenyewe ili aufaidi apate matunda yake unamzuia kuukata umekusudia nini? Kwa hiyo badala ya kusaidia watu kuwahimiza, hawatungi sheria ya kusema pandeni miti au boresha mazingira wanasema usikate mti ambao umepanda mwenyewe, kwa hiyo inazidi kuleta shida katika usimamizi wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yetu Kamati ya Sheria Ndogo kwamba sheria mbovu iwe Sheria Ndogo hasa hizi sheria ambazo sisi tunashughulika nazo zisiwe Sheria katika sheria za nchi hii zifutwe na zirekebishwe pale ambapo inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninalishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kuchangia na kwa Wabunge kuchangia kwa umakini mkubwa na kwa weledi mkubwa sana na kwa ufanisi wa hali ya juu sana, michango yao imekuwa ya manufaa makubwa na imesaidia kuweka jambo hili vizuri na hoja imezidi kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo Mheshimiwa Jasson Rweikiza kwa kuhitimisha taarifa yenu sasa ninalihoji Bunge wanaokubaliana na taarifa hii pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Mwenyekiti sasa hivi kuwa ni Azimio la Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waliosema ndio wameshinda, kwa hivyo natoa tamko rasmi kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati ya Sheria Ndogo sasa yamekuwa ni Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo sasa nitumie fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Makamu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya, ambayo pia sasa inasaidia Serikali kujua changamoto zilizopo kwenye sheria zetu ndogo.

Pia naishukuru Serikali kupitia Mheshimiwa Jenista kwa *commitment* waliyotoa na niwatoe hofu tu kwamba hata kama sheria zote zitakuwa hazina changamoto bado Kamati ya Sheria Ndogo itahitajika, kwa sababu kadri dunia inavyokwenda uhitaji utakuwa mkubwa na sheria zitaendelea kutungwa na kurekebishwa kwa hivyo na Kamati ya Sheria Ndogo itakuwa bado ina jukumu lile lile la kuangalia, hata ikiwa hizo sheria zitakazokuja sasa zitakuwa ziko safi kabisa, tutakuwa tumejua kwamba lengo la kuweko kwa Kamati Ndogo hii ya Sheria itakuwa limefikiwa kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo niwashukuru sana wachangiaji wote ambao wameendelea kutoa maoni yao kwa Serikali, lakini tuelewe tu Serikali kwamba suala hili ni muhimu kwa sababu linamgusa mwananchi wetu mmoja mmoja huko alipo, kwa hiyo kuwa na wataalam ambao wanaelewa uhalisia wa jiografia ya nchi yetu na maeneo husika ni muhimu sana pamoja na kwamba watakuwa na taaluma ya sheria, kwa hiyo uhalisia wa kujua jiografia hii iko vipi na hali ya maisha ya watu yapo vipi, kutapelekea kutunga sheria ambazo siyo kandamizi ambazo hazikiuki Sheria Mama au Katiba na badala yake tutapata manufaa makubwa na wananchi wetu watakuwa wamefurahi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kabla sijaahirisha naomba nikumbushe, kesho kutakuwa na

semina ya Saa Tatu Asubuhi ambayo inahusu hali ya upatikanaji na udhibiti wa dawa nchini ambayo itatolewa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria bila ya kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa naahirisha shunguli za Bunge hadi kesho tarehe 11 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana.

*(Saa 11:40 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 11 Novemba, 2021, Saa Nane Mchana)*